# MIAKA 60 YA JESHI LA KUJENGA TAIFA



## Malezi ya Vijana, Uzalishaji Mali na Ulinzi kwa Ustawi wa Taifa

MIAKA 60 YA JESHI LA KUJENGA TAIFA

1963-2023

# Kaulimbiu:

## Malezi ya Vijana, Uzalishaji Mali na Ulinzi kwa Ustawi wa Taifa

Kitabu hiki kimetolewa na Jeshi la Kujenga Taifa,
Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa,
Sanduku la Posta 2963,
Dodoma, Tanzania.

Simu: +255 26 2962078.
Nukushi: +255 26 2962080
Barua pepe: info@jkt.go.tz Tovuti: www.jkt.go.tz

©Jeshi la Kujenga Taifa, Julai 2023
Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Jeshi la Kujenga Taifa.

ISBN 978-9912-41-253-8

Kimepigwa chapa na Jamana Printers Ltd,
Sanduku la Posta 5584,
Dar es Salaam, Tanzania.



**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
na Amiri Jeshi Mkuu



**Mhe. Innocent Lugha Bashungwa**
Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa



**Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe**

**Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**




# Jenerali Jacob John Mkunda

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi




# Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa

# YALIYOMO


**VIFUPISHO ............ xi**

**DIRA, DHIMA, TUNU ............ xv**

**TAMKO LA WAZIRI WA ULINZI NA JKT ............ xvi**

**TAMKO LA MKUU WA MAJESHI YA ULINZI ............ xviii**

**TAMKO LA MKUU WA JESHI LA KUJENGA TAIFA ............ xx**

**DIBAJI ............ xxiv**

**UTANGULIZI ............ xxvi**

**SURA YA KWANZA ............ 1**

**KUASISIWA KWA JESHI LA KUJENGA TAIFA ............ 1**

Dhana ya Kuandaa Vijana Kutumikia Taifa ............ 1
Kijana wa JKT ............ 6
Historia ya Jeshi la Kujenga Taifa ............ 7
JKT 1963 hadi 1973 ............ 12
Sheria ya Kuanzishwa kwa JKT ............ 19
Viongozi wa Kitaifa Waliofanya Mafunzo ya JKT ............ 26
Uongozi wa JKT Mwaka 1963 ............ 28
Mawaziri Mwaka 1963 – 1973 ............ 33
Mafanikio ............ 36
Changamoto ............ 39
JKT Mwaka 1973 hadi 2001 ............ 39
Ushirikiano kati ya JKT na JKUZ ............ 47
Vita vya Kagera ............ 48
Mawaziri wa Ulinzi na JKT Mwaka 1973 – 2001 ............ 50
Mafanikio ............ 54
Changamoto ............ 57
JKT Mwaka 2001 hadi 2013 ............ 58

Mafanikio ........ 67
Changamoto ........ 68

**SURA YA PILI ........ 70**

**KUIMARIKA KWA JKT ........ 70**

Kundi la Kujitolea ........ 72
Kundi la Lazima ........ 73
Kundi Maalum ........ 75
Wadau katika Malezi ya Vijana ........ 77
Fikra kwa Vijana wa JKT ........ 79
Kitaifa ........ 79
Kimataifa ........ 83
Malezi ya Vijana wa JKT ........ 86
Tofauti ya Aliyelelewa na Asiyelelewa JKT ........ 87
Mawaziri wa Ulinzi na JKT Mwaka 2013 hadi Sasa ........ 106
Mafanikio ........ 108
Changamoto ........ 118

**SURA YA TATU ........ 121**

**MPANGO MKAKATI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI . 121**

Malengo ya Mkakati ........ 123
Utekelezaji wa Mkakati ........ 123
Mafanikio ........ 127
Changamoto ........ 129

**SURA YA NNE ........ 130**

**SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA JESHI LA KUJENGA TAIFA ........ 130**

Chimbuko la SUMAJKT ........ 130
Muundo wa SUMAJKT ........ 136
Wakurugenzi Watendaji SUMAJKT Mwaka 1981 hadi Sasa ........ 137
Maendeleo ya Shirika ........ 138
Kazi za SUMAJKT ........ 145

Sekta ya Ujenzi ........ 146
Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ........ 153
Sekta ya Viwanda ........ 158
Huduma ya Elimu ........ 176
Mafanikio ........ 179
Changamoto ........ 187

**SURA YA TANO ........ 190**

**MIPANGO YA BAADAYE ........ 190**

**HITIMISHO ........ 201**

**ORODHA YA OPERESHENI ZILIZOFANYWA NA JKT TANGU 10 JULAI 1963 HADI 2023 ........ 203**

**MAREJEO ........ 207**

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACP | Assistant Commissioner of Police |
| ASP | Assistant Superintendent of Police / Afro-Shirazi Party |
| BAMMATA | Baraza la Michezo ya Majeshi Tanzania |
| BB | Builders Brigade |
| BRELA | Business Registration and Licensing Agency |
| CBA | Chemistry, Biology and Agriculture |
| CBG | Chemistry, Biology and Geography |
| CC | Conservation Corps |
| CEO | Chief Executive Officer |
| CRB | Contractors Registration Board |
| CUJKT | Chuo cha Uongozi Jeshi la Kujenga Taifa |
| CWT | Chama Cha Walimu Tanzania |
| DRC | Democratic Republic of Congo |
| DSM | Dar es Salaam |
| ED | Executive Director |
| EGM | Economics, Geography and Mathematics |
| FAT | Football Association of Tanzania |
| GPS | Global Positioning System |
| HGE | History, Geography and Economics |
| HGK | History, Geography and Kiswahili |
| HGL | History, Geography and Language |
| HKL | History, Kiswahili and Language |
| IMF | International Monetary Fund |

| | |
|---|---|
| JKT | Jeshi la Kujenga Taifa |
| JKUZ | Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar |
| JNHPP | Julius Nyerere HydroPower Project |
| JWTZ | Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania |
| KAR | King's African Rifles |
| KPL | Kilombero Plantation Limited |
| MD | Managing Director |
| MMJKT | Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa |
| MMJKU | Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Uchumi |
| MoU | Memorandum of Understanding |
| MV | Motor Vessel |
| NACTE | National Council of Technical Education |
| NEC | National Electoral Commission |
| NEEC | National Economic Empowerment Council |
| NHC | National Housing Corporation |
| NIDA | National Identification Authority |
| NiRC | National Irrigation Commission |
| NS | National Service |
| NSA | National Service Act |
| NSCD | National Service Construction Department |
| NYS | National Youth Service/National Youth Scheme |

| | |
|---|---|
| PCB | Physics, Chemistry and Biology |
| PCM | Physics, Chemistry and Mathematics |
| PGM | Physics, Geography and Mathematics |
| RAS | Recirculating Aquaculture System |
| SCBCL | SUMAJKT Consultancy Bureau Company Limited |
| SCCL | SUMAJKT Construction Company Limited |
| SECL | SUMAJKT Electrical Company Limited |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi Zanzibar |
| SPCL | SUMAJKT Pharmaceutical Company Limited |
| SSP | Senior Superintendent of Police |
| SUA | Sokoine University of Agriculture |
| SUMAJKT | Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa |
| SUMAJKT MM | Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa Makao Makuu |
| TAHA | Tanzania Horticultural Association |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TANU | Tanganyika African National Union |
| TANZASINO | Tanzania United Pharmaceuticals Company Limited. |
| TARI | Tanzania Agricultural Research Institute |

| | |
|---|---|
| TAZARA | Tanzania and Zambia Railway Authority |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TEMESA | Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Agency |
| TFF | Tanzania Football Federation |
| TIN | Tax Identification Number |
| TMA | Tanzania Meteorological Authority |
| TOSCI | Tanzania Official Seed Certification Institute |
| TPA | Tanzania Ports Authority |
| TR | Tanganyika Rifles/Treasury Registrar |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TYL | TANU Youth League |
| UBM | Ultimate Building Machine |
| UDSM | University of Dar es Salaam |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNO | United Nations Organization |
| USA | United States of America |
| VAT | Value Added Tax |
| VET | Vocational Educational Training |
| VETA | Vocational Education and Training Authority |
| VRN | VAT Registration Number |
| VVU | Virusi Vya UKIMWI |
| WB | World Bank |
| YLO | Youth Labour Organization |

## DIRA YA JKT

Kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, hatimaye Tanzania iwe jamii yenye nidhamu, umoja, uzalendo, udugu, ukakamavu na kupenda kazi.

## DHIMA YA JKT

Kulea Vijana wa Tanzania ili kuwajengea nidhamu, uzalendo, ukakamavu na kuwafundisha ujuzi hatimaye kuchangia katika ulinzi wa Taifa na maendeleo ya kiuchumi.

## TUNU ZA JKT

- Uadilifu
- Uzalendo
- Umoja
- Mshikamano
- Kujitolea
- Nidhamu
- Kupenda Kazi



## TAMKO LA WAZIRI WA ULINZI NA JKT

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) ni chombo kilichokasimiwa jukumu la malezi ya Vijana, uzalishaji mali na ulinzi wa Taifa.

Katika kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Sura ya Tano, Ibara ya 105 (i) na (j), Wizara ya Ulinzi na JKT imeendelea kuiwezesha JKT kuboresha miundombinu, ikiwamo kujenga mahanga kwa ajili ya malazi ili kuwezesha Vijana wengi zaidi kupata fursa ya mafunzo. Wizara itaendelea kuongeza bajeti ya JKT kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Katika kuhakikisha mafunzo ya JKT yanakuwa na tija, Wizara kwa kushirikiana na wadau imekamilisha kupitia mitaala kwa ajili ya kuboresha mafunzo yanayotolewa na JKT kwa Vijana yakilenga kuwawezesha kujiajiri wanapomaliza mafunzo. Mafunzo ya JKT huandaa Vijana kufahamu wajibu wao katika jamii likiwamo

jukumu la ulinzi wa Taifa, kwa kuwa Vijana ndio nguvukazi ya Taifa.

Wizara imeendelea kusimamia shughuli za Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT) ili kutoa huduma bora, kutekeleza miradi ya kimkakati na kuchangia uendeshaji wa shughuli za JKT yakiwamo mafunzo kwa Vijana.

Katika miaka 60 ya JKT, chombo hiki kimekuwa tegemeo kwa Taifa katika kuandaa Vijana wenye uzalendo, uadilifu, ukakamavu, nidhamu, mshikamano na umoja wa Taifa.

Kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuwezesha JKT kutimiza malengo ya kuasisiwa kwake. Wizara tunamwahidi Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwamba tutaendelea kusimamia maelekezo yake kwa ubunifu na weledi ya kuona JKT inatekeleza majukumu yake ya msingi ya malezi kwa Vijana, ulinzi wa Taifa na uzalishaji mali, ili kuwezesha JKT kujitosheleza kwa chakula kambini na ziada kusaidia Taifa letu.

Nihitimishe kwa nukuu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere inayosema: *"Umuhimu wa JKT unatokana na Taifa kuhitaji Vijana, na Vijana kuitikia mwito huo wa kulitumikia Taifa lao kwa jukumu lolote."*

**Mhe. Innocent Lugha Bashungwa**

**Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**



## TAMKO LA MKUU WA MAJESHI YA ULINZI

JAMHURI ya Muungano wa Tanzania ni Taifa huru lenye mipango yake na kujitawala. Miongoni mwa mipango hiyo mahususi ni ulinzi wa nchi, rasilimali zilizopo na mipaka yake.

Ulinzi ni jukumu muhimu kwa Taifa kwani unawezesha shughuli za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni kutekelezwa kwa matakwa na mipango ya nchi.

Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na majukumu ya malezi ya Vijana na uzalishaji mali linatekeleza pia jukumu la ulinzi chini ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

pamoja na kuandaa Jeshi la Akiba kupitia mafunzo yanayotolewa na JKT.

Pamoja na changamoto za kiuchumi, kiteknolojia na kijamii zilizopo, JKT inaendelea kuandaa Vijana kuwa wazalendo na tayari kutumika katika nyanja mbalimbali kwa maslahi ya Taifa.

Nashukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuijengea uwezo JKT kama sehemu kamili ya JWTZ na kuweka mazingira rafiki ya kiutendaji ili kuhakikisha jukumu la ulinzi wa Taifa hili linatekelezwa kwa kiwango kinachostahili.

Tangu kuunganishwa kwa JKT na JWTZ mwaka 1975, Wakuu wa Majeshi wote tumekuwa tukihakikisha utekelezaji wa majukumu ya JKT unafanyika kwa ufanisi. Hivyo, JWTZ itaendelea na jukumu hilo kwa maslahi ya Taifa.

**Jenerali Jacob John Mkunda**

**Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi**



## TAMKO LA MKUU WA JESHI LA KUJENGA TAIFA

MIAKA 60 ya Jeshi la Kujenga Taifa tangu kuasisiwa kwake, inadhihirisha nia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha utamaduni wa Taifa unarithishwa kwa vizazi kadri vinavyofuatana pamoja na nguvu kazi ya Taifa inajengwa na kutumika kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Ufanisi wa JKT umetokana na jitihada za waasisi wake walioongozwa na Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa muktadha huo, nitumie nafasi hii kutoa shukurani za dhati kwa jitihada hizo za kuanzishwa

JKT Julai 10, 1963 kwani ndio msingi wa uzalendo katika Taifa letu.

Kwa niaba ya Maafisa, Askari, Vijana na Watumishi wa Umma wa JKT, nawashukuru Viongozi wote wa Serikali awamu zote kwa kuendelea kuthamini na kuimarisha JKT. Nawashukuru Marais wa Awamu ya Kwanza, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere; Awamu ya Pili, Mhe. Ali Hassan Mwinyi; Awamu ya Tatu, Mhe. Benjamin William Mkapa; Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete; Awamu ya Tano, Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na Awamu ya Sita Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kwa moyo wa dhati, nakiri na kutambua mchango wa Serikali katika awamu zote, kwani JKT ilivyo sasa ni picha halisi ya jitihada zilizowekwa katika kujenga uzalendo kwa jamii ya kitanzania.

Vilevile, namshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT, Mhe. Innocent Lugha Bashungwa(Mb), Katibu Mkuu Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe, mawaziri wote, makatibu wakuu wa wizara zote na watendaji wengine waliowahi kuhudumu na wanaoendelea kuhudumu katika Wizara

ya Ulinzi na JKT kwani ufanisi wa JKT tangu 1963, ni matokeo ya sera na miongozo bora iliyotolewa na inayotolewa.

Kwa namna ya pekee, namshukuru Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Jacob John Mkunda na Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi wastaafu kwani maono yao mazuri ndiyo yaliyoifikisha JKT tunayoiona leo hii.

Pia, nawashukuru Wakuu wa JKT waliopita kwa kuwataja; Kamishna Msaidizi wa Polisi David Nkulila, Kamishna Msaidizi wa Polisi Robert Kaswende, Mrakibu Msaidizi wa Polisi Laurence Gama, Meja Jenerali Nelson Mkisi, Meja Jenerali Makame Rashid, Meja Jenerali Davis Mwamunyange, Meja Jenerali Abdulrahman Shimbo, Meja Jenerali Martin Madata, Meja Jenerali Samwel Kitundu, Meja Jenerali Samweli Ndomba, Meja Jenerali Raphael Muhuga, Meja Jenerali Michael Isamuhyo, Meja Jenerali Martin Busungu, Meja Jenerali Charles Mbuge ambao walifanya kazi kubwa iliyonirahisishia utendaji kazi wangu kutokana na mazingira mazuri waliyoyaweka kwenye utekelezaji wa majukumu ya JKT.

Pia, namshukuru Mkuu wa Tawi la Utawala JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, Mkuu wa Tawi la Mafunzo, Kanali Aisha Matanza; Mkuu wa Tawi la Huduma za Kisheria; Kanali Projest Rutaihwa na Mkuu wa Tawi la Usalama na Utambuzi, Kanali Aloyce Chagula; Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT, Kanali Petro Ngata; Wakurugenzi, Maafisa Wanadhimu, Makamanda Vikosi, Askari na Vijana kwa michango yao katika ufanisi wa JKT.

Mwisho, shukurani zangu ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya JKT, Kanali George Kazaula na wajumbe wa Kamati hiyo kwa kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha maadhimisho yanafana.

**Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele**

**Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa**

# DIBAJI

KITABU hiki kimeandikwa ili kusaidia hadhira kulifahamu Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) linapotimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake rasmi Julai 10, 1963. Vilevile, kinafafanua chimbuko la JKT na uhalisia wake nchini Tanzania.

Kwa kuzingatia mageuzi ya kisayansi na kiteknolojia, kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa miaka 60, Kitabu hiki ni mwendelezo wa vitabu vilivyotangulia ambavyo ni vya miaka 10 ya JKT (1963–1973), miaka 25 (1963 – 1988) na miaka 50 (1963–2013).

Madhumuni ya Kitabu hiki ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu JKT kama chombo adhimu cha Taifa chenye dhamana ya kujenga uzalendo, umoja na mshikamano thabiti kwa Watanzania, bila kujali itikadi za kidini, kikabila, kipato, kisiasa na kijinsia.

Kwa kusoma Kitabu hiki, jamii itaipambanua JKT kama chombo adhimu cha kuandaa Vijana kuwa tayari kulitumikia Taifa kupitia malezi bora yenye tija,

uzalishaji mali na ulinzi. Vilevile, walengwa wataelewa dhima na dira ya JKT, historia, kukua kwake, SUMAJKT, mafanikio, changamoto na mipango ya baadaye. Hivyo, Kitabu hiki ni hazina inayotoa elimu kwa jamii ya Kitanzania na wasomaji wengine kwa ujumla.

**Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele**

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa

# UTANGULIZI

*"LEO ziko nchi duniani, watu wanakwenda kuona jinsi watu wanavyojenga nchi zao. Viongozi na wananchi wote wameshikana moja kwa moja, wanajenga nchi yao kwa faida ya nchi yao. Matumaini yangu, wananchi, ni kwamba kesho na kesho kutwa watu watasema; Nendeni, muone Watanzania wanavyojenga nchi yao".* **Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.**

*"JKT ni mahali pazuri pa kuanzia kuvunja fikra iliyopandikizwa na Wakoloni, iliyofanya wananchi kupeleka watoto wao shuleni, ili waondokane na kazi ngumu kama ya kilimo, lakini sasa wasomi wameelewa kuwa kilimo humpa mtu fedha kila siku, badala ya mfanyakazi anayepata mshahara mara moja kwa mwezi."* **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Pili, Mhe. Ali Hassan Mwinyi.**

*"Na pengine niongeze kusema kuwa hakuna ushahidi unaozidi ushahidi wa mtu kuona na kushuhudia mwenyewe. Ushahidi wa uhakika wa manufaa ya Jeshi la Kujenga Taifa wanao wale wote waliopitia mafunzo yake na kulitumikia Taifa kwa njia hii. Mimi ni mmoja wa walioshuhudia. Leo nimekuwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu. Mnaweza kuwa na uhakika kuwa natambua, kwa kuwa mimi mwenyewe ni shahidi, manufaa ya JKT. Hivyo nitaunga mkono Jeshi hili siku zote za maisha yangu."* **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Tatu, Mhe. Benjamin William Mkapa.**

*"Serikali na Taifa kwa jumla limetiwa moyo sana na mwitikio mkubwa wa vijana wanaojiunga na JKT. Ni jambo la faraja kubwa kuona kuwa katika vijana wa kujitolea, wapo wengine wana elimu ya vyuo vikuu na taaluma mbalimbali … Hivyo basi inazipa JKT na JWTZ fursa nzuri ya kupata Maafisa na Askari … Lakini, hata wale ambao hawatajiunga na vyombo vya ulinzi na usalama, kwa malezi na maandalizi waliyopata JKT watakuwa raia wema na wenye kutoa mchango unaostahili na unaohitajika sana katika Taifa."* **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.**

*"Vijana hawa ambao wamegawanyika katika makundi mbalimbali, wapo vijana ambao wamekuja kujitolea na wana degree (shahada), ni wasomi wazuri tu … imefikia mahali kila kazi ninayowapa JWTZ chini ya JKT inakuwa na uhakika … endeleeni kusimamia vijana wetu waendelee kuchapa kazi na nina uhakika kwa kutumia hawa, Tanzania itaenda mbele sana."* **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Tano, Dkt. John Pombe Magufuli.**

*"JKT ni chombo ambacho kimejifafanua kwenye malezi ya vijana wetu sababu inawezekana kwamba vijana wetu wanalelewa wakiwa majumbani, wanalelewa shuleni, wanalelewa kwenye taasisi zao za kidini, lakini JKT kuna malezi ya aina yake. Mtu anaweza akapata malezi kote huko lakini bado asisimame kuwa raia madhubuti wa nchi yake … JKT imefanya hii kazi kwa muda mrefu na wote ni mashahidi kwamba waliopitia JKT wanapokuwa kwenye nafasi zozote zile ndani na nje ya Serikali, mwenendo wao hauwi kinyume na matakwa ya Taifa."* **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Sita, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.**

Kabla ya Ukoloni, jamii za Kiafrika zilichukulia malezi kama fursa nyeti kwa wanajamii wote iliyotumika kufunza, kuandaa na kurithisha utambulisho, majukumu, mila na desturi kwa kizazi kijacho.

Ukoloni ulienea Tanzania mwaka 1885 (wakati huo Tanganyika) baada ya Afrika kugawanywa na kutawaliwa,[1] na ulidumu hadi Tanganyika ilipopata Uhuru Desemba 9, 1961. Katika kipindi chote Taifa lilipokuwa chini ya utawala wa kigeni, dhana ya malezi ya mtoto au kijana wa kitanzania, ilibadilika na kujikita katika kufanikisha malengo ya watawala wa wakati huo.

Vijana walilelewa kwa misingi ya kupewa elimu ya darasani, ili kutumika kwa maslahi ya Wakoloni, na utaratibu huo ulisababisha Vijana kupotoka na kubeza mila, desturi na utamaduni wa asili, hali iliyochangia ubaguzi wa rangi, kipato, dini, kabila, elimu, jinsia, n.k.

Hata hivyo, malezi yaliendelea kufanyika katika jamii za kitanzania kupitia familia, dini, shule, koo, kabila, n.k., na lengo la malezi lilibaki kuwa la kuandaa Kijana

1 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Chimbuko, Misingi na Maendeleo, Mkuki na Nyota Publishers Ltd, 2022.

kukua na kuwa na uwezo wa kushiriki shughuli za kiuchumi, kijamii na kitamaduni japokuwa yaliathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukoloni.

Baada ya Uhuru, athari hii iliendelea na baadaye Taifa likabaini mahitaji ya kuwa na chombo kitakachohusika na kulea Vijana kwa kuwafundisha kupenda kazi za mikono, kuondoa athari mbaya zilizoachwa na utawala wa kikoloni wa kuchagua kazi za ofisini tu na kuchukia kazi za mikono na kutumia nguvu mfano kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara.

Vilevile, kutoa maarifa muhimu ya kulifahamu Taifa lao, historia na utamaduni na kufanya walipende na kulitumikia, kuifahamu miiko na makatazo kupitia ufahamu wa sheria na Katiba ya nchi, uhuru na mipaka yake, demokrasia, utawala bora, vyama vya siasa na itikadi za kisiasa. Hali kadhalika, amani na utulivu, huduma za jamii, mafunzo dhidi ya athari za ubaguzi, rushwa na ufisadi na kutambua maslahi ya Taifa na kuwa tayari kuyalinda.

Mwaka 1963, Taifa likaanzisha JKT kama itakavyofafanuliwa katika Sura ya Kwanza ya Kitabu

hiki, ili chombo hicho kibebe jukumu la malezi ya Vijana wa kitanzania watakaolelewa katika mazingira yenye tofauti za kipato, elimu, utamaduni, mila na imani za kidini licha ya utofauti wao.

Tangu kuanzishwa kwa JKT nchini, Vijana wengi wamefanya mafunzo kwa utaratibu wa kujitolea na kwa lazima, ili kuhakikisha wanapata malezi bora na wamalizapo warudi katika jamii kushirikiana nayo kujenga Taifa.

Katika miaka hii 60 ya kuwapo kwa JKT, Taifa linajivunia amani na utulivu uliopo nchini, uzalendo, mshikamano na mchango katika uchumi wa Taifa kupitia nyanja mbalimbali. Na hii inatokana na mafunzo wanayopata Vijana wakiwa JKT, kwani wanajengwa kwa maslahi ya Taifa.

Vilevile, tumeshuhudia SUMAJKT ikitekeleza majukumu ya uzalishaji na huduma kwa jamii, kiasi cha kupunguza pengo la huduma ambazo zilitarajiwa kutolewa na Serikali moja kwa moja. Kwa mfano, kupunguza gharama za uendeshaji kwa JKT, kushiriki

katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama vile ujenzi wa ukuta kuzunguka mgodi wa madini ya tanzanite ulioko Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, ujenzi wa Ikulu Chamwino na mingine.

Kuwapo kwa JKT pia kumevutia mataifa mengine Afrika na duniani kwa kuanzisha programu kama hizo za kukusanya Vijana na kuwaweka pamoja na kuwaandaa kwa ajili ya kutumikia Taifa lao. Taifa linashuhudia miaka 60 ya JKT yenye mafanikio kijamii, kiuchumi na kisiasa katika kupambana na maadui ujinga, umasikini na maradhi.

Yote hayo yamewezekana kutokana na ushirikiano wa dhati uliopo kati ya JKT na Serikali, JWTZ na jamii kwa kuzingatia ukweli, kuwa Taifa hili ni moja na lenye mwelekeo mmoja kwa maslahi mapana ya watu wake.

Hivyo, JKT bado ni nyenzo muhimu ya malezi kwa Vijana, na bado itaendelea kuwa muhimili muhimu wa kuwaandaa kuwa wazalendo kulitumikia Taifa lao.

# SURA YA KWANZA

## KUASISIWA KWA JESHI LA KUJENGA TAIFA

*"WANANCHI, National Service hatukuanzisha sisi. Mataifa mengi duniani yana National Service. Taifa linawaambia vijana wake; tunataka vijana mlitumikie Taifa lenu. Taifa linadai utumishi toka kwa vijana, linadai huduma kwa vijana, na vijana wanaitika. Taifa linawadai huduma vijana na vijana wanaitika mwito huo kwenda kuhudumia Taifa kwa kazi yoyote ambayo Taifa linahitaji ifanywe. Narudia nikisema mipango kama hiyo hatukuanza sisi. Mataifa mengi duniani yana National Service.".* **Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.**

### Dhana ya Kuandaa Vijana Kutumikia Taifa

"National Service" ni maneno ya Kiingereza yanayomaanisha Huduma ya Taifa au Huduma kwa Taifa au Kutumikia Taifa. Maneno hayo yanatumika katika nchi nyingi duniani, yakimaanisha taasisi ya kuandaa Vijana kutumikia Taifa lao.

Maneno hayo yalitumika rasmi kisheria kwa mara ya kwanza mwaka 1939, baada ya kutungwa sheria maalumu nchini Uingereza kurasimisha mafunzo ya

kijeshi kwa Vijana kama sehemu muhimu ya kutoa huduma kwa Taifa. [2]

Shinikizo hilo liliwekwa Uingereza baada ya kujifunza kutokana na Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia (1914–1918) na baadaye Vita Vikuu vya Pili vya Dunia (1939–1945).

Pamoja na maneno hayo ya Kiingereza kutumika katika nchi nyingi kwa maana ya taasisi ya kuandaa Vijana kutumikia Taifa lao, jamii nyingi duniani tayari zilikuwa na mifumo ya kutoa mafunzo ya aina hiyo kwa Vijana kulingana na vipaumbele katika jamii husika.[3]

Kumbukumbu za Fasihi Andishi hudhihirisha kuwa katika karne ya tano, Dola ya Kirumi iliyokuwa imetawala sehemu nyingi duniani ilianzisha mifumo ya kushirikisha na kuandaa Vijana kutoa huduma kwa pamoja katika makoloni yake.

Katika mifumo hiyo Vijana kutoka tabaka masikini, na wenye kipato, watawaliwa na watawala, walipewa

2 UK. National Service (Armed Forces) Act, 1939.

3 Bala Achi (1988), Arms and Armour in the Warfare of Pre-Colonial Hausaland. The Center for African Area Studies, Kyoto University.

mafunzo ya pamoja ya ulinzi na maendeleo ya jamii, maridhiano na urafiki.[4]

Dhana na mfumo huu wa kujenga uzalendo, maridhiano na urafiki katika maeneo yote ya utawala wa Dola ya Kirumi kupitia mafunzo hayo kwa Vijana wa kada zote, ulipata umaarufu katika nchi nyingi za Ulaya kama Ugiriki, Ujerumani na Ufaransa, na hatimaye bara la Amerika Kaskazini.

Mtaalamu wa historia, Thomas Hippler anarejea dhana na mfumo huo kama 'Romanticism' (Urumi) uliochukua taswira ya aina yake Ujerumani na Ufaransa enzi za mapinduzi ya miaka 1789 hadi 1930.[5]

Mfumo wa mafunzo ya aina hiyo ulitumiwa vema na Napoleon Bonaparte (mtawala na kamanda wa kijeshi wa Ufaransa) kabla na baada ya mapinduzi ya Ufaransa, katika kubainisha uhusiano wa mtu mmoja mmoja, Dola na Taifa kwa ujumla.[6]

---

4 Plutarch, (1992), "Plutarch's life of Coriolanus", plutarch's lives, Vol I (Dryden translation ed), Random House.

5 T. Hippler, (2008), *Citizens, Soldiers and National Armies: Military Service in France and Germany, 1789 – 1830* (*War, History and Politics*), Routtledge, New York, www.amazon.Com

6 Kama ilivyorejewa hapo juu.

Baadhi ya nchi za Ulaya kama Sweden na Finland zina historia ya mafunzo hayo kwa Vijana wa jinsia zote kwa mujibu wa sheria kwa karne nyingi.[7] Pia, nchini Marekani (USA) mjadala wa kujenga Taifa hilo kwa kushirikisha Vijana ulisisitizwa baada ya uhuru mwaka 1776.

Rais wa zamani wa Marekani na mtaalamu wa sheria, Thomas Jefferson alisisitiza mafunzo kwa Vijana akisema: "Ukweli lazima uwe wazi, kuwa bila kufuata mfumo wa Kirumi na Kigiriki wa kumfanya kila raia kuwa Askari, Marekani haiwezi kujilinda."[8] Hivyo alisisitiza mitaala ya kijeshi ifundishwe vyuoni mwaka 1813.

Barani Asia, mafunzo hayo yalitolewa kwa jamii za wakulima, wakazi wa mijini na watu wa kawaida vijijini, chini ya machifu. Mfano, nchini China yalitolewa karne nyingi kabla ya Kristo chini ya tawala za kinasaba, kama vile nasaba za Shang, Wei, Shuhan, Wu na Jin.[9]

7 A. Persson and F. Sundeval, (2019), "Conscripting Women: Gender, Soldiering and military Service in Sweeden 1965 – 2018" in the women History Review, 28:7, 1039 – 1056, DOI: 10. 1080/09612025. 2019.1596542.

8 R. Leenhard, (2006), *Elightened Defense: The National Security Policy of Thomas Jefferson*, West Virginia University, West Virginia.

9 P. Ebrey etal (eds), (2006), *Pre – Modern East Asia: To 1800 : A cultural, Social and Political History*, Houghton Mifflin Company, Boston and New York, pp 61 – 63, 72.

Mafunzo haya yalikuwa ya kujitolea au ya lazima ikitegemea na urithi kutoka familia za makamanda wa kijadi.[10]

Katika nchi nyingi za Afrika kulikuwa na mifumo ya kuandaa Vijana kutumikia jamii kupitia mifumo ya ulinzi na usalama wa kijadi au kiasili.[11]

Nchini Tanzania makabila mengi yalikuwa na mifumo ya mafunzo na malezi ya asili kwa Vijana kwa kuakisi maendeleo na ulinzi wa jamii husika.

Hivi sasa nchi nyingi duniani zina utaratibu wa kuandaa Vijana kwa majina na mifumo tofauti, kwa mfano JKT/JKUZ kwa Tanzania na 'National Youth Service' kwa Sudani Kusini, Korea Kusini na Kenya.

Mifumo hii ya huduma ya Vijana kwa Taifa, inaweza kuwa na taswira kutegemea mikakati na malengo ya kila jamii husika, katika kutatua changamoto zake. Kwa mfano, kwa Tanzania JKT ni taasisi iliyoundwa na Serikali kwa ajili ya kutoa mafunzo ya malezi,

10 P. Ebrey etal (eds), (2006), *Pre – Modern East Asia: To 1800 : A cultural, Social and Political History*, Houghton Mifflin Company, Boston and New York, pp 61 – 63, 72.

11 Bala Achi (1988), Arms and Armor in the Warfare of Pre-Colonial Hausaland. The Center for African Area Studies, Kyoto University.

uzalishaji mali na ulinzi kwa Vijana ili kujenga Taifa lenye uzalendo.

**Kijana wa JKT**

Kijana wa JKT anatafsiriwa kuwa Mtanzania mwenye umri wa miaka 16 hadi 35,[12] aliyeandikishwa JKT kwa kundi la kujitolea, lazima au kuteuliwa na Serikali kwa sababu maalumu za kimkakati. Kijana huyu ni aliyelelewa na JKT na kuwa mzalendo halisi asiyetiliwa shaka kwa maslahi ya Taifa.

Kwa mujibu wa Sheria ya JKT, Kijana ni mtumishi aliyeandikishwa, ambaye Waziri wa Ulinzi na JKT, kwa amri ya Serikali, anaweza kuteua Afisa yeyote wa umma au wa chuo, shule au taasisi nyingine ya elimu kufanya mafunzo ya JKT.[13]


Vijana hawa ni wanaojiunga na JKT, Serikali inapobaini kuwapo haja ya kundi hilo kupata mafunzo ya uzalendo ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao. Watumishi wa Bunge, Wizara ya Mambo ya Nje na viongozi wa siasa ni mifano ya waliowahi kufanya mafunzo ya JKT.

12 JKT (1973) Miaka 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

13 Sheria ya JKT Namba 16 ya mwaka 1964

## Historia ya Jeshi la Kujenga Taifa

Historia ya kuanzishwa JKT inaanzia mwaka 1958 wakati wa ziara ya viongozi wa Taifa nchini Ghana, ambapo Baba wa Taifa Mwl. Nyerere na Mhe. Rashid Kawawa (Simba wa Vita) walikwenda kuhudhuria sherehe za kuadhimisha mwaka mmoja wa uhuru wa nchi hiyo.



*Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.*

Mhe. Kawawa (Simba wa Vita) alikuwa akiwakilisha Chama cha Wafanyakazi wa Tanganyika (TFL) na Mwalimu Nyerere Chama cha Tanganyika African National Union (TANU).



*Mhe. Rashid Mfaume Kawawa*

Wakiwa nchini humo, Mhe. Kawawa alialikwa chakula cha jioni pamoja na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Israel, Bi. Golda Meir.

Mhe. Kawawa alipata fursa ya kuzungumza na kiongozi huyo, ambaye alitanabaisha namna Taifa la Israel linavyowaandaa vijana wake kutumikia Taifa lao kwa moyo wa uzalendo.

'Simba wa Vita' alivutiwa na maelezo yaliyotolewa na Bi. Meir, namna ya utaratibu unaotumika na Taifa la

Israel kuwakusanya na kuwaandaa Vijana kijeshi na baadaye kufanya majukumu mengine ya kitaifa kwa ujasiri, uvumilivu, ushirikiano na nidhamu.[14]

Aliporejea hotelini walikofikia na Mwalimu Nyerere, Mhe. Kawawa alimweleza juu ya mazungumzo yake na Bi. Meir, ambayo yalimvutia na kumwagiza ayafanyie kazi atakaporejea nchini.[15]

Waliporejea, Mhe. Kawawa aliyawasilisha mawazo hayo kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama cha TANU (TYL), Joseph Kizurira Nyerere, akisaidiwa na Nangwanda Lawi Sijaona. Viongozi hao waliafiki mawazo hayo na kuyapeleka katika Mkutano Mkuu wa TYL uliofanyika Tabora Agosti 25, 1958 ili kujadiliwa zaidi na wajumbe.

14 Rwamkoma Daima (2017), Toleo Na. 1

15 P.Bjerk,(2015) Building A Peaceful Nation; Julius Nyerere and Establishment of Sovereignty in Tanzania, 1960-1964.



*Bi. Golda Meir*

Hata hivyo, mkutano wa TANU ulishindwa kuidhinisha uanzishwaji wa mafunzo hayo, kwa kuwa Tanganyika ilikuwa inatawaliwa na Uingereza chini ya uangalizi wa Umoja wa Mataifa (UNO). Baada ya Uhuru wa Tanganyika Desemba 9, 1961 wazo hilo liliwasilishwa kwa mara ya pili kwenye Mkutano Mkuu wa Vijana wa TANU Agosti 25, 1962 mjini Tabora.[16]

Mkutano huo uliazimia kutekeleza wazo la kuanzishwa rasmi kwa taasisi ya kuandaa Vijana kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Wajumbe wa kikao hicho

16 JKT, (1973), Miaka 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

walikuwa Joseph Nyerere (Mbunge na Katibu Mkuu TYL), Isack Malecela (Katibu Mkuu wa Mambo ya Fedha TYL), Moses Nnauye, H.S.J. Zingaro (Katibu Mkuu Mtendaji TYL) na Meja Yaffer Ben Amots wa Israel (mshauri mtaalamu wa mpango huo).[17]

Baada ya mkutano huo, mapendekezo ya kuanzishwa chombo rasmi cha kitaifa cha kuandaa Vijana kuwa Wazalendo, yaliwasilishwa serikalini na kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri Aprili 1963.

Serikali iliridhia chombo hicho kiitwe Jeshi la Kujenga Taifa chini ya Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana. Wizara hiyo iliongozwa na Waziri Nangwanda Sijaona (Mwenyekiti TYL), Joseph Nyerere (Naibu Waziri na Katibu TYL) na Mzee Harubu Saidi (Katibu Mkuu wa Wizara).[18]

## JKT 1963 hadi 1973

Julai 10, 1963 JKT ilianzishwa rasmi bila kutungwa sheria na Bunge la Tanganyika.[19] Kwa mara ya kwanza, mafunzo ya JKT yalitolewa kwa Vijana wa

17 JKT, (1973), Miaka 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

18 JKT. (2013). Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

19 Kama ilivyorejewa hapo juu.

TYL kwa kutumia eneo na majengo ya Mgulani, Dar es Salaam yaliyokuwa kituo cha kuwavua uaskari baadhi ya askari wa Mwingereza (KAR) waliopigana Vita vya Pili vya Dunia (1939—1945) kabla ya kurejeshwa katika mikoa yao ya asili.[20]

Vijana wa kwanza kujiunga na mafunzo ya JKT walikuwa viongozi (makatibu) wa TYL kutoka wilaya

11 nchini, wengi wao walishahudhuria mafunzo ya uongozi wa Vijana Yugoslavia mwaka 1962.[21] Aidha, katika juhudi za kuandaa uongozi wa JKT, Vijana 30 walipelekwa Israel Mei 19, 1963 kufanya mafunzo ya uimarishaji.

Kundi la kwanza kujiunga na mafunzo katika kambi ya JKT Mgulani Julai 10, 1963 lilikuwa na Vijana wafuatao:[22]

- Sebastian Chale (TYL – Kilosa)
- Peter Lwegarulira (TYL – Bukoba)
- John Ndimngwango (TYL – Kasulu)
- Hashim Ngaliwason (TYL – Mtwara)

20 JKT. (2013). Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

21 JKT. (1973). Miaka 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

22 Kama ilivyorejewa hapo juu.

- Dismass Msilu (TYL – Iringa)
- Zainab Kiango (TYL – Dar es Salaam)
- Athuman Msonge (TYL – Musoma)
- Rupho Kamba (TYL – Mwanza)
- Reginald Mitande (TYL – Masasi)
- Eslei Mwakyambiki (Mwalimu Dar es Salaam)
- Saidi Desai (Mwalimu Dar es Salaam)



*Joseph Nyerere (kushoto) akizungumza na baadhi ya Vijana 11 waliojiunga na JKT mwaka 1963 katika Kambi ya Mgulani.*



***Bi. Zainab Kiango aliyekuwa msichana pekee miongoni mwa Vijana 11 wa kwanza kujiunga na mafunzo ya JKT mwaka 1963.***

Ilipofika Agosti 1963 Vijana wengine watano walijiunga na mafunzo hayo na hivyo kundi la kwanza kuwa na Vijana 16. Vijana hao watano ni:

- John Mwakilulele
- Adam Mwakyoma
- Magreth Mhando
- Aloys Moyo
- Edson Simkonde

Kundi hilo lilifuatiwa na makundi mengine matatu kabla ya kutungwa Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa mwaka 1964. Katika makundi hayo, kundi la kwanza lilijiunga Oktoba 1963 na kuitwa Kombania 'A' lenye Vijana 130 wakiwamo Amos Mawazo ambaye baadaye alikuwa Mkuu wa Kambi ya JKT Mbweni na Makame Rashid ambaye baadaye alikuwa Mkuu wa JKT. Kundi la pili lilijiunga Novemba 1963 na kuitwa Kombania 'B' lenye Vijana 179.



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kulia) akiwa na Mhe. Abeid Aman Karume (kushoto) wakikagua Vijana wa JKT katika mafunzo yaliyofanyika kwenye Kambi ya Mgulani JKT.*

Vijana waliendelea kuhamasika na kundi la tatu lililoitwa Kombania 'C', la Vijana 170 kujiunga Januari 17, 1964. Baadhi ya Vijana waliokuwa kundi hili ni Christopher Khamsini (baadaye alikuwa Kamanda Kikosi JKT Makutupora na Mkurugenzi wa Kwanza wa Usalama na Utambuzi JKT), Tumainieli Mlay ambaye baadaye alikuwa Kamanda Kikosi JKT Mafinga, Edmund Mjengwa ambaye baadaye alikuwa Mkuu wa Wilaya na Mbunge wa Mbarali. Makundi haya yalilenga kuandaa viongozi wa JKT.[23]



*Vijana wa JKT wakiwa mafunzoni eneo la Ubungo, 1963.*

23 JKT. (2013). Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Wakati huo, JKT ilikuwa na malengo yafuatayo:[24]

- Kuelekeza nguvu ya Vijana katika miradi ya ujenzi wa Taifa, na kuwa kichocheo katika maendeleo ya jamii kwa kuwa mfano wa kizalendo, uraia mwema na moyo wa kujitolea kwa Taifa.
- Kupitia JKT, Vijana wapate maarifa na moyo wa kupambana na maadui ujinga, umasikini na maradhi.
- Kuhamasisha Vijana wa kada mbalimbali, wataalamu na wasio wataalamu ili kujenga nidhamu, ufahamu, utu na tabia njema ya uongozi katika jamii.
- Kuandaa Vijana kuwa tayari kusaidia Taifa kukabiliana na majanga ya asili au dharura, kama vile mafuriko, moto, magonjwa ya mlipuko na mengineyo.
- Kuwezesha Vijana kushiriki kudumisha utamaduni wa Taifa, malikale, mila na desturi za jamii na kuhamasisha watu kufikia malengo ya Taifa.
- Kuwaleta pamoja Vijana na kuwaelimisha, kuwaandaa kuwa raia wema, na wazalishaji mali katika muktadha wa udugu, umoja na uzalendo kwa Taifa.

24 The Government of Tanganyika, (1963), Tanganyika National Service Directives



*Miongoni mwa ofisi za kwanza zilizotumika JKT Mgulani 1963.*

**Sheria ya Kuanzishwa kwa JKT**

JKT ilianzishwa kwa Sheria Namba 16 (National Service Act, 1964) iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002 kifungu 3(1). Sheria hii ilipitishwa kuwataka vijana kujitolea kwa hiari kujiunga na JKT ili kulitumikia Taifa. Vijana hao walitakiwa kuwa angalau wawe wamehitimu elimu ya msingi, wanachama wa TYL,

wasiwe wameoa au kuolewa na wawe tayari kujitolea kutumikia Taifa kwa muda wa miaka miwili.[25]

Baada ya kupitishwa sheria hiyo, Novemba 1964 kundi la kwanza liliripoti Mgulani JKT na kuitwa **Operesheni Maendeleo,** likiwa na Vijana 486 akiwamo Kanali Agustino Sanga ambaye baadaye alikuwa Mkuu wa Kikosi cha JKT Mgulani na Meja Gerald Oddo ambaye baadaye alikuwa Mkuu wa Kikosi cha JKT Mgambo.

Operesheni zingine zilizofuata ni **Motomoto 'A'** na **'B',** kozi za makatibu wa TYL za Machi 15, 1965–Mei 1965 na Agosti 2, 1965–Oktoba 19, 1965 Mgulani JKT. Operesheni Jamhuri ya Oktoba 1965 na Umoja yenye Vijana 300 wakiwamo wenye elimu ya sekondari waliojiunga kwa mara ya kwanza Novemba 1965.[26]

Baadhi ya Vijana wa kundi hili walipelekwa Bulgaria kusomea Uhandisi, wengine Uandishi wa Habari Nyegezi, Mwanza na wengine Ualimu wa Elimu ya Watu Wazima katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.[27]

25 Sheria ya JKT Namba 16 ya mwaka 1964.

26 JKT. (2013), Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

27 JKT. (2013), Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Katika mfumo huo wa kujitolea, Vijana wengi, hususan wenye elimu ya msingi na viongozi wa TYL, waliendelea kujiunga na JKT kwa ridhaa yao. Mfano, Elly Anangisye (Katibu Mkuu TYL) na Fortunatus Masha (Katibu Mkuu Msaidizi Ofisi ya TANU Lumumba).

Pia, wataalamu wa fani mbalimbali kama Fredrick Rutakyamirwa (kutoka Wizara ya Ardhi kuja kuongoza idara ya siasa), Francis Mbena (kutoka Wizara ya Elimu kuja kutoa elimu ya kawaida) na Dkt. Justine Omari (kutoka Wizara ya Afya kuja kutoa huduma ya afya), waliazimwa kuongeza ufanisi JKT.[28]

Huduma za afya pia zilitolewa kwa Maafisa, Askari, Vijana na wananchi walioishi jirani na kambi za Jeshi kwa mfano, zahanati ya kwanza ilianzishwa mwaka 1965 katika kikosi cha JKT Mgulani.[29]

Kutokana na kukua na kuenea kwa JKT katika mikoa mingine na mwitikio mdogo wa wasomi kujitolea, Serikali iliona umuhimu wa kurekebisha sheria namba

---

28 JKT. (2013), Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

29 Kama ilivyorejewa hapo juu.

16 ya 1964 ili kuweka ulazima kwa Vijana wenye elimu ya sekondari na vyuo kutumikia Taifa kupitia JKT.

Akihutubia Vijana wa JKT Mgulani mwaka 1964, Mwalimu Nyerere alieleza kuwa Wakoloni walifundisha Watanzania jambo baya la kutenga kazi za nchi kati ya wavaa tai na wasiovaa tai. Alisisitiza kuwa sheria ni sharti ibadilishwe, ili kushinikiza wasomi na wenye kazi kupita JKT kwa miaka miwili.[30]

Aliona kuwa, kimsingi ni vema Vijana wote wa kitanzania wakapata mafunzo ya JKT kabla ya kuendelea na majukumu ya kijamii, kitaifa na kimataifa, hivyo alisisitiza, "Serikali imeunda kundi la kujenga Taifa, ili watu wa aina yote wapite, kesho na kesho kutwa, na JKT ndio uwe mlango mkuu, na kama mtu hakuupita, haingii mahali pengine, hivyo sharti apite kwanza mlango huo". [31]

Kwa mantiki hiyo, jamii ikiwa na Vijana waliopitia JKT, Taifa litakuwa na uhakika wa jamii yenye uzalendo; tunu ambayo ni muhimu kwa mataifa mengi

30 Hotuba ya Mwl. JK Nyerere aliyoitoa kwa Vijana wa JKT Mgulani tarehe 31 Machi 1964, Dar es Salaam.

31 JKT (1973) Miaka 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

duniani na ndiyo maana, baadhi ya nchi zina utaratibu kama huu wa kulea Vijana.

Mataifa hayo ni kama vile Zambia (National Service), Kenya (National Youth Service), Ghana (National Service Scheme), China (Poverty Alleviation Relay Project), New Zealand (Conservation Corps), Nigeria (National Youth Service), Namibia (National Youth Service), Malaysia (National Youth Scheme), Israel (National Youth Scheme) na Bulgaria (Youth Labour Organization).

Kabla ya marekebisho ya sheria ya JKT, kundi la pili lilipelekwa nchini Israel Novemba 1965 kujifunza utaalamu wa fani mbalimbali zilizokuwa zinahitajika kuimarisha mafunzo ya JKT.

Wengine walipelekwa Chuo cha JWTZ Mgulani.[32] Makundi hayo matatu yaliyofanya mafunzo katika kambi za Mgulani (Dar es Salaam), Ruvu (Pwani), Mafinga (Iringa), Makutupora (Dodoma) na Oljoro (Arusha) ndiyo yalizalisha viongozi wengi wa JKT na kuimarisha Jeshi hilo.

32 JKT. (1973). Miaka 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mwaka 1966 sheria hii ilifanyiwa marekebisho na kuwataka wasomi kujiunga na JKT kwa lazima lakini Vijana wasomi hawakujiunga kwa wingi kama ilivyotarajiwa.

Baada ya mafunzo ya JKT kuwa ya lazima kwa mujibu wa sheria, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Tiba Muhimbili, Chuo cha Ufundi cha Dar es Salaam na Chuo cha Ualimu Chang'ombe, waligomea mwito wa kisheria na kuandamana hadi Ikulu Oktoba 22, 1966 kupinga sheria mpya, jambo lililomkasirisha Mwalimu Nyerere na kufukuza wanafunzi 393 ili wakajirekebishe.

Kesho yake, Oktoba 23, 1966 Mwalimu alihutubia wananchi na kuwaelimisha nia njema ya sheria hiyo akisema:

> *"Lakini tuliona kwamba vijana waliokwisha kuingia katika National Service hivi sasa ni vijana ambao au wana elimu ndogo, au hawakusoma kabisa au hawana kazi au hawakusomea kazi yoyote. Hao ndiyo wanaoingia katika National Service. Na National Service ni kazi ya vijana, ni mahali pa vijana kwenda kutumikia Taifa. Tukaona vijana wenye elimu hawaji. Waliosomea kazi maalumu hawaji. Mwenye kitumbua na kazi*

*yake mahali, haji. Tukaona kuwa jambo hili lina kasoro. Vipi waliokwishatumikia vizuri sana na Taifa, wao ndio hawaji kuhudumia Taifa katika National Service, ila wale ambao hawakugharimiwa na Taifa wao ndio wanakuja? Tuligundua kwamba mpango huu una walakini."* **Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.**

Baadaye Mwalimu alisamehe wanafunzi waliogoma na wakarejea vyuoni kuendelea na masomo isipokuwa wanafunzi saba waliokuwa viongozi wa mgomo huo. Hilo lilikuwa fundisho kwa wanafunzi wengine wa vyuo vikuu na vijana wengine kwa ujumla.

Baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967 kama Sera ya Taifa ya Ujamaa na Kujitegemea, JKT ilibaki kuwa chombo mahususi cha Serikali cha kuhamasisha na kuwaleta Watanzania pamoja, ili kuwajengea moyo wa uzalendo, umoja, kupenda kazi, kujitegemea na kuandaa viongozi wa Taifa.[33]

JKT ilifanya juhudi kubwa ya kuandaa Vijana kuwa wazalendo kuwapa elimu kamili ya siasa. Mafunzo hayo yalikuwa muhimu katika kuwafanya watambue vizuri maadui wa ndani na nje ya nchi, na pia kujihadhari na

33 Azimio la Arusha la Mwaka 1967 (Tafsiri ya lugha ya Kiingereza)

viongozi wenye fikra za udini, ukabila, rangi na tofauti za elimu.[34]

**Viongozi wa Kitaifa Waliofanya Mafunzo ya JKT**

Kuanzia mwaka 1968,ViongoziwaKitaifa walihamasika kufanya mafunzo ya JKT. Miongoni mwao ni;

- Mwalimu Nyerere — Operesheni Mwenge JKT Mafinga mwaka 1968.
- Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi (Makamu wa Kwanza wa Rais)
- Mhe. Kawawa (Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais)
- Mhe. Adam Sapi Mkwawa (Spika wa Bunge)
- Mhe. Edward Moringe Sokoine (Waziri wa Ulinzi)
- Mhe. Job Lusinde (Waziri wa Mawasiliano)
- Mh. Abdulrahman Mohammed Babu (Waziri wa Mambo ya Nje) na wengineo ambao wote walipata mafunzo JKT Ruvu Operesheni Kazi 'B' mwaka 1968.

34 JKT. (1988). Miaka 25 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

- Mhe. Mkapa (Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Uhuru baadaye Rais wa Tanzania) alifanya mafunzo JKT Ruvu, Operesheni Tekeleza mwaka 1971.
- Mhe. Benard Membe (Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mstaafu) alifanya mafunzo JKT Oljoro, Operesheni Muungano (JW & JKT) mwaka 1975/76.

Aidha, Vijana wengi wa kitanzania walipata fursa ya kutumikia Taifa kupitia JKT na baadaye kuwa viongozi. Miongoni mwao ni:

- Mhe. Othman Chande (Jaji Mkuu Mstaafu) Operesheni Utii mwaka 1967.
- Mhe. Zakhia Meghji (Waziri wa Fedha Mstaafu) Operesheni Utamaduni mwaka 1969
- Mhe. Fredrick Sumaye (Waziri Mkuu Mstaafu) Operesheni Mwangaza mwaka 1970.
- Mhe. Edward Lowassa (Waziri Mkuu Mstaafu) Operesheni Mikoa JKT Ruvu mwaka 1970.
- Mhe. Mizengo Pinda (Waziri Mkuu Mstaafu) Operesheni Mikoa JKT Ruvu mwaka 1970.
- Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete (Rais wa Awamu ya Nne)

Operesheni Tumaini, JKT Ruvu, mwaka 1972.

- Jenerali Salvatory Venance Mabeyo (Mkuu wa Majeshi Mstaafu) Operesheni Usafi, JKT Mafinga, mwaka 1978.
- Meja Jenerali Michael Isamuhyo (baadaye alikuwa Mkuu wa JKT) Operesheni Mazoezi JKT Ruvu, mwaka 1978.
- Mhe. Dkt. John Magufuli (Rais wa Awamu ya Tano) Operesheni Mshikamano JKT Makutupora mwaka 1984.
- Mhe. Jenista Mhagama (Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu) Operesheni Kambarage JKT Mlale mwaka 1990/91.
- Meja Jenerali Rajabu Mabele (Mkuu wa JKT) Operesheni Kambarage JKT Ruvu mwaka 1990/91.
- Jenerali Jacob Mkunda (Mkuu wa Majeshi) Operesheni Vyama Vingi, JKT Ruvu mwaka 1992.

**Uongozi wa JKT Mwaka 1963**

JKT ilikuwa Jeshi jipya ambalo halikurithiwa kwa Wakoloni. Hivyo, lililazimika kuchukua viongozi kutoka majeshi mengine, hususani Jeshi la Polisi. Kwa

utaratibu huo wafuatao walikuwa viongozi waanzilishi wa JKT mwaka 1963:

- Kamishina Msaidizi wa Polisi (ACP) David Nkulila. Aliteuliwa na Rais Nyerere kuwa Mkurugenzi wa JKT.
- Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Laurence Gama. Aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Msaidizi – Utawala.
- Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Gladstone Mwamlima. Aliteuliwa kuwa 'Senior Master' na Mkuu wa Kambi ya JKT Mgulani.
- Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Saidi Magambo. Aliteuliwa kuwa 'Senior Master' na Mkuu wa Maghala JKT (Mgavi Mkuu).

Majukumu ya msingi ya JKT tangu kuanzishwa ni malezi ya Vijana, uzalishaji mali na ulinzi. Katika kutekeleza majukumu hayo, JKT ilitoa mafunzo kwa makundi matatu ambayo ni Kundi la Kujitolea, Lazima na Kundi Maalumu ambalo lilihusisha watumishi wa taasisi mbalimbali.

**Malezi ya Vijana** yalilenga kuwajengea uzalendo wa kutumikia Taifa. Masomo waliyofundishwa Vijana

yalikuwa ni Siasa (TANU na ASP), Uchumi, Historia, Jiografia, Uhasibu, Kiswahili, Sanaa, Michezo na Ufundi.[35]

Hata hivyo, fani za umakanika, uhunzi, uchomeleaji vyuma, useremala, ufundi viatu, ushonaji na ufundi bomba zilipewa kipaumbele ili kusaidia Taifa kuongeza wafanyakazi wenye ujuzi wa ufundi viwandani.[36]

Pia, michezo, sanaa na utamaduni vilitiliwa mkazo katika kuibua na kuendeleza vipaji ili kukuza Taifa. Katika michezo zilianzishwa timu za mpira wa miguu, mpira wa kikapu, netiboli, ngumi na riadha. Pia, kikundi cha muziki wa Jazi kilianzishwa mwaka 1965, 'Brass Band' mwaka 1968 na vikundi vya ngoma na kwaya mwaka 1969.

Mwaka 1972 wanamichezo na wasanii wote walihamishiwa Kikosi cha JKT Mgulani chini ya Kamanda Kikosi Luteni Kanali Venance Nhg'onge. Lengo la kuanzishwa Kikosi hicho lilikuwa kurahisisha shughuli na utendaji katika michezo, sanaa na utamaduni.

35 JKT (1973) Miaka 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

36 Kama ilivyorejewa.

JKT ilitumia vikundi hivyo kuhamasisha, kuburudisha na kuelimisha Maafisa, Askari, Vijana na Watumishi wa umma na familia zao kwenye kambi za JKT na sherehe za kitaifa.

Vilevile, Vijana walifundishwa uzalishaji mali kama vile kilimo na ufugaji kwenye kambi zote ili kuwasaidia Vijana waweze kutumia ujuzi huo kujitegemea kwa maendeleo ya jamii baada ya kumaliza muda wao katika JKT.

Hata hivyo, wakati JKT inaasisiwa hali ya uzalishaji mali ilikuwa duni kutokana na idadi ndogo ya Vijana na ukosefu wa wataalamu.

Umuhimu wa JKT katika jukumu la ulinzi ni wa kihistoria baada ya maasi ya Jeshi lililokuwa na taswira ya kikoloni Tanganyika Rifles (TR) yaliyotokea mwaka 1964[37]. TR ilivunjwa na kuanzishwa JWTZ ambamo Vijana wa TYL na ASP waliandikishwa. Maasi hayo yalitoa msukumo kwa Serikali kuona umuhimu wa JKT kupewa jukumu maalumu la kufundisha Vijana ulinzi na kuandaa Askari wa kujiunga na Jeshi hilo.[38]

37 Tanzania. Peoples Defence Force (1993), Tanganyika Rifles Mutiny: January 1964. Dar es Salaam University Press.

38 JKT (1988) Miaka 25 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Vijana wa TYL walipewa mafunzo ya ulinzi na kujengewa uzalendo katika kambi ya Mgulani JKT na baadaye walijiunga na JWTZ. Baada ya uundwaji wa JWTZ, JKT ilirejea katika majukumu yake ya msingi ya malezi ya Vijana na uzalishaji mali.



*Mwalimu Julius Nyerere, akipata ushauri kutoka kwa mtaalamu wa kijeshi baada ya maasi ya mwaka 1964.*

Katika kipindi cha miaka kumi ya mwanzo (1963–1973), JKT iliendeshwa kwa ushauri wa wataalamu kutoka Israel wakiongozwa na Luteni Kanali Ben Yaah. Wakati huo mafunzo ya JKT yalishabihiana na

mfumo wa maandalizi ya Vijana katika kambi zilizojulikana kama 'Kibutz' nchini Israel.[39]

Kuanzia mwaka 1963 hadi 1973, JKT ilikuwa chini ya wizara tofauti zifuatazo:

- Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana mwaka 1963—1964.
- Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Utamaduni wa Taifa mwaka 1964—1967.
- Wizara ya Ulinzi na JKT mwaka 1967 hadi sasa.

**Mawaziri Mwaka 1963 – 1973**



*Mhe. Nangwanda Sijaona*
Waziri wa Utamaduni wa Taifa na Vijana
**(1962 – 1964)**



*Mhe. Sheikh Kaluta Abedi*
Waziri wa Maendeleo ya Jamii na Utamaduni wa Taifa
**(Apr – Okt 1964)**

39 JKT. (2013). Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.



*Mhe. Chidiel Mgonja*
Waziri wa Maendeleo ya Jamii na Utamaduni wa Taifa

**(1965 – 1967)**



*Mhe. Rashid Kawawa*
Waziri wa Ulinzi na JKT

**(1967-1972)**



*Mhe. Edward Sokoine*
Waziri wa Ulinzi na JKT

**(1972-1977)**

# Wakuu wa JKT Mwaka 1963 – 1973



*ACP David Nkulila*
**(1963-1967)**



*ACP Robert Kaswende*
**(1968-1970)**



*ASP Lawrence Gama*
**(1970-1973)**

**Mafanikio**

Katika kipindi cha miaka 10 ya awali, JKT ilifanikiwa katika yafuatayo:-

- Kuandaa Vijana wa TYL kuwa na sifa za kuandikishwa JWTZ baada ya maasi ya TR mwaka 1964.
- Kushiriki kuanzisha mashamba ya pamba mkoani Mwanza katika maeneo ya Usagala, Ngunga na Mkula mwaka 1964.
- Mwaka 1965 Vijana wa JKT walishiriki katika ujenzi wa barabara ya Chalinze—Segera kwa kushirikiana na kampuni ya VIADUKT ya Yugoslavia.
- Kuanzisha chuo cha ufundi stadi katika Kambi ya JKT Mgulani mwaka 1967.
- Kuanzisha Kambi mpya, miongoni mwa hizo ni JKT Nachingwea, Lindi mwaka 1964; JKT Chita, Morogoro mwaka 1965; JKT Mafinga, Iringa na JKT Ruvu, Pwani mwaka 1967; JKT Makutupora, Dodoma na JKT Oljoro, Arusha mwaka 1968 pamoja na JKT Mlale, Ruvuma mwaka 1970.

- Mwishoni mwa miaka ya sitini, Vijana wa JKT walishiriki katika ujenzi wa nyumba za wasiojiweza na majengo ya huduma za jamii kama vile hospitali, shule, nk. Vijiji vilivyonufaika na mpango huu ni Rusende, Kilimani, Ngorongo, Ndandunyikanza, Kipo 'A', Kipo 'B', Chumbi, Utungi, Ikwiriri, Mbunyu na Mnyuyu katika mkoa wa Pwani.

- Uanzishwaji wa vikundi vya sanaa na utamaduni ambavyo ni ngoma, kwaya, muziki wa Jazi, 'Brass Band' na michezo ya mpira wa miguu, kikapu na netiboli kati ya mwaka 1965 na 1969.

- Kusaidia kufyatua matofali na kujenga shule, hospitali na visima vya maji wakati wa mafuriko yaliyotokea Handeni, Tanga mwaka 1969. Vijiji vilivyonufaika ni Mkata, Kitumbi, Kwa Mkono, Kwa Ndonja, Kabuku, Kwedizinga, Segera, Mgambo, Sua na Mazingara.

- Kuanzisha Kikosi cha Ujenzi mwaka 1969/70 ambacho kazi zake za mwanzo zilikuwa ni kujenga majengo ya Jeshi.

- Kuanzisha madarasa ya kisomo cha watu wazima

katika Kambi na maeneo jirani ili kuunga mkono jitihada za Serikali kuondoa adui ujinga mwaka 1970.

- Kuongeza shule za ufundi katika kambi za JKT Ruvu, Buhemba na Mlale mwaka 1971 na kufanya idadi ya shule za ufundi kuwa nne pamoja na Mgulani.
- Kujenga na kuanzisha viwanda vya ufundi ambavyo vilijishughulisha na utengenezaji wa viatu, vifaa vya nyumbani, ofisini na ushonaji nguo mwaka 1972.
- Kuchimba mifereji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika shamba la mpunga Ruvu JKT mwaka 1973.
- Kuimarisha uhusiano na nchi jirani ambazo ni Zambia na Burundi kwa kutoa mafunzo kwa Vijana wa nchi hizo.
- Ujenzi wa Ikulu ndogo Chamwino, jumba la maendeleo na starehe, uwanja wa gwaride (futi 400 x 200) na nyumba 66 za kuishi wananchi Julai hadi Oktoba 1971.

- Ujenzi wa kituo cha afya, shule ya msingi, nyumba za kuishi wasiojiweza, uwekaji wa taa za umeme na maji Butiama Novemba 1971 hadi Machi 1972.
- Ujenzi wa vijiji vya Ujamaa Rufiji, Songea, Dodoma, Iringa na Mbeya mwaka 1972.

**Changamoto**

- Upungufu wa wataalamu wa kilimo na mifugo katika Vikosi. Katika kutatua changamoto hiyo, JKT iliazima Maafisa wa kilimo wa Wilaya ili kutoa msaada wa kitaalamu.
- Upungufu wa wataalamu wa ufundi katika Kikosi cha Ujenzi. Hata hivyo, walichukuliwa wataalamu wenye ujuzi serikalini kutoka Wizara ya Mawasiliano na wengine kutoka Kambi mbalimbali za Jeshi ili kuongeza nguvu.

**JKT Mwaka 1973 hadi 2001**

JWTZ na JKT ziliunganishwa mwaka 1975 kutokana na mabadiliko ya sera ya Ulinzi wa Taifa. Waraka wa Baraza la Mawaziri Namba 11 wa mwaka 1975 una maelezo ya ufafanuzi kuhusu suala hili[40].

40 JKT (1988) Miaka 25 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Kuunganishwa kwa vyombo hivyo kuliwezesha JWTZ kupata askari wa miguu kutoka JKT. Hatua hii ilisaidia Serikali kupunguza gharama za uendeshaji wa vyombo hivyo kwani Vijana hao waliishi kambini na kuhudumiwa kwa pamoja.

Kwa muktadha huo, JKT ilitakiwa kuandaa Askari wa muda mfupi na kuwa msingi wa Vikosi vya Askari wa miguu kwa JWTZ. Vijana wa kujitolea walitakiwa kutumikia JKT kwa miaka mitatu na mujibu wa sheria walitakiwa kutumikia kwa mwaka mmoja.

Baada ya kuunganishwa, JKT rasmi ikawa ni sehemu ya JWTZ. Maafisa wa JKT walipatiwa kamisheni na Rais na kutunukiwa vyeo kuanzia Mkuu wa JKT ambaye kutokana na mfumo wa vyeo vipya akawa Brigedia Jenerali na Afisa wa cheo cha chini kuwa Luteni.[41]

Jumla ya Maafisa waliopatiwa kamisheni ni 121 huku waliokuwa viongozi wa vyeo vya Chief Guide hadi Cadet Guide wakitunikiwa vyeo vya Afisa Mteule, Sajini Taji, Sajini, Koplo, Koplo Usu na Praiveti. Kwa

41 JWTZ (2014), Maadhimisho ya Miaka 50 ya JWTZ.

mabadiliko hayo, Maafisa na Askari walirekebishiwa mishahara na stahiki zingine za JWTZ.[42]

JKT iliendelea na malezi ya Vijana na kuwajengea uzalendo ili kutumikia Taifa. Masomo yaliyofundishwa yaliongezeka ambayo ni Kilimo, Ufundi na Ufugaji. Pia, huduma za afya ziliboreshwa ili kuhudumia Vijana kambini, Maafisa, Askari na familia zao na jamii kwa ujumla.

Katika kuunga mkono juhudi za Serikali kupandisha viwango vya elimu kwa watumishi kutoka elimu ya msingi hadi sekondari, JKT ilianzisha shule ya sekondari Mgulani, Dar es Salaam mwaka 1974 ili kuendeleza Maafisa na Askari. Mwaka 1994, ikaanzishwa sekondari ya Kawawa, Iringa ili zitoe elimu kwa familia za Maafisa, Askari na jamii.[43]

Pia, michezo, sanaa na utamaduni viliendelea kutekelezwa katika Kambi za JKT zilizoongezeka na kuwapo haja ya kuimarisha timu na vikundi vifuatavyo:

42 JKT(2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

43 JKT(2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

- **Timu ya JKT Kabambe** ilibadilishwa jina na kuitwa Ruvu Stars, Pwani mwaka 1975, kwa ushauri wa aliyekuwa Mkuu wa Elimu ya Siasa Jeshini, Brigedia Jenerali Moses Nnauye.
- **Timu ya Netiboli:** Timu hii ilianzishwa mwaka 1979 ikijulikana kama JKT Mbweni. Bingwa wa kihistoria wa Kombe la Muungano na Tanzania Bara.
- **Timu za mpira wa mikono wanaume, wanawake:** Timu ya kwanza kuanzishwa ni ya wanawake mwaka 1980 katika Kambi ya JKT Buhemba, Mara ikifuatiwa na timu ya wanaume JKT Mbweni, Dar es Salaam mwaka 1983.
- **Timu ya Mieleka na Judo:** Hii ilianzishwa mwaka 1982 JKT Mgulani.

Katika kuendeleza fani za muziki na utamaduni ndani ya JKT, Juni 18 hadi 28, 1977 Maafisa watatu; Kanali Francis Mbena, Luteni Agustino Sanga na Luteni Estinata Mwaka walizuru Guyana (Amerika Kusini). Wakiwa huko, walivutiwa na muziki wa mapipa (Steel Band), ambao asili yake ni Amerika Kusini.

Waliporudi, walipendekeza JKT iandae utaratibu wa kufundisha Vijana muziki wa mapipa.

Mapendekezo yalikubalika na mipango ilipokamilika, JKT ilipeleka wasanii Guyana kujifunza na baadaye kuanzisha kikundi. Kutokana na teknolojia yake ya kutengeneza vifaa vya muziki huo kuwa rahisi, Jeshi la Polisi na JKUZ nao walijifunza kutoka JKT.

Mwaka 1980 kikundi cha ngoma na nyimbo JKT Mgulani kilijizolea umaarufu hata kuitwa Kikundi cha Sanaa cha Taifa. Aidha, JKT iliendelea kutoa elimu ya muziki wa mapipa kwa JKUZ na Zambia National Service. Askari sita kutoka JKUZ na wengine sita kutoka Zambia, walijifunza muziki huo JKT Mgulani na Maramba kwa mwaka mmoja.

Katika kipindi cha mwaka 1974 hadi 1983 utamaduni uliendelea kuboreshwa. Vikosi vya JKT vilianzisha vikundi vya sanaa na utamaduni, kutumbuiza na kufundisha Vijana mila na desturi za makabila. Vijana waliojiunga na JKT walifundishwa ngoma na nyimbo za asili.

Uzalishaji mali uliendelea kuboreshwa na baadaye kuanzishwa SUMAJKT mwaka 1981 (Maelezo zaidi Sura ya Nne).

Mwaka 1985/86 chini ya Serikali ya Awamu ya Pili, JKT ilipata mafanikio makubwa katika uzalishaji mali ambapo JKT ilizalisha mahindi magunia 45,209 zaidi ya mahitaji. Ziada iliuzwa kwa wananchi na kwenye Vikosi vya JWTZ. Serikali ya Awamu ya Pili chini ya uongozi wa Mhe. Rais Ali Hassan Mwinyi ilitoa mchango mkubwa katika mafanikio ya JKT.



*Mhe. Ali Hassan Mwinyi,*
*Rais wa Awamu ya Pili.*

**Jedwali Na. 1: Uzalishaji katika Kilimo Miaka ya 1970 na 1980**

| Mavuno kwa Ekari | | |
|---|---|---|
| **Zao** | **1974/75** | **1985/86** |
| 1. Mahindi | Magunia 2.4 | Magunia 9.4 |
| 2. Maharage | Magunia 0.3 | Magunia 3.3 |
| 3. Mbogamboga na matunda | Kilogramu 867 | Kilogramu 2,351 |
| 4. Pamba | Kilogramu 69 | Kilogramu 475 |

**Jedwali Na. 2: Hali ya Uzalishaji katika Kilimo cha Mboga na Matunda 1989/90**

| | Jumla | Zilizoliwa JKT | Zilizouzwa JWTZ | Zilizouzwa kwingineko | Zilizoharibika |
|---|---|---|---|---|---|
| Kilogramu | 630,877 | 497,803 | 93,240 | 38,614 | 1,200 |
| Thamani (Shs) | 7,002,773 | 5,654,537 | 797,314 | 502,922 | 48,000 |

Baada ya kuanzishwa uzalishaji mali, kuliibuka haja ya kuongeza wataalamu ili kuzalisha kwa tija. Lengo la awali ni kuwa na wanajeshi wataalamu wenye uzoefu na mazingira ya Jeshi.

Hali hiyo ilisababisha kuanzishwa kozi za kuendesha mitambo ngazi ya cheti, kusimamia kilimo Mafinga na

ufugaji Mpwapwa. Hata hivyo, uzalishaji haukuridhisha. Hatua zifuatazo zilichukuliwa:

- Kuhifadhi maji, utunzaji vitalu, kilimo cha mzunguko, matumizi ya samadi na mpangilio wa bustani.
- Kuongeza ubora wa mifugo.
- Kuboresha uvuvi katika Vikosi vya Bulombora, Mbweni, Chita, Itende na Maramba.
- Kuboresha ufugaji nyuki katika Vikosi vya Mgambo, Makutupora, Mbweni na Nachingwea.
- Kushirikisha wataalamu waliopo katika Mikoa yenye Vikosi vya JKT ili kupata msaada wa kitaalamu.
- Kuwapa kipaumbele Maafisa na Askari kufanya mafunzo ya kilimo na mifugo.
- Kuboresha utunzaji kumbukumbu za kilimo, mifugo na uvuvi.
- Kuandaa mashindano ya Vikosi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo.

Ulinzi ulisisitizwa na kuwa jukumu rasmi na muhimu kwa JKT. Maafisa na Askari hushiriki ulinzi, mazoezi

ya medani na ulinzi wa amani na hutekeleza majukumu hayo.

Katika kutekeleza jukumu la ulinzi, JKT huandaa Vijana kuwa na sifa za kujiunga na vyombo vya ulinzi na usalama, kuwa Jeshi la Akiba kwa kuwapa mafunzo ya ujasiri na ukakamavu.

Pia, kushiriki uokoaji wa mali na maisha ya wananchi yanapotokea maafa kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kusaidia mamlaka za kiraia katika majukumu ya kitaifa na kuwa sehemu ya kuimarisha ulinzi wa maeneo yenye changamoto za kiusalama kwa kuanzisha Vikosi na Viteule.

**Ushirikiano kati ya JKT na JKUZ**

Ushirikiano kati ya JKT na JKUZ ulianza katikati ya miaka ya sabini (1975-76), wakati Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ilipoteua Vijana 100 kujiunga JKT kujifunza ukakamavu, uzalishaji mali, ulinzi na uongozi ili watakaporejea waanzishe JKUZ.

Hatua hiyo ilitokana na imani kubwa aliyokuwa nayo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa SMZ, Mhe. Jumbe,

aliyewahi kufanya mafunzo ya JKT, hivyo aliamini Vijana walioteuliwa watafunzwa uzalendo, uzalishaji mali na ulinzi, na kutoa mchango mkubwa kwa SMZ.[44]

**Vita vya Kagera**

Oktoba 1978, Taifa liliingia vitani dhidi ya Nduli Idi Amin wa Uganda aliyevamia ardhi ya Tanzania mkoani Ziwa Magharibi (sasa Kagera) na kujitangazia kuwa sehemu ya Uganda. JWTZ ilijibu mashambulizi na kufanikiwa kumuondoa Amin na kupata ushindi Juni 1979. Vijana wa JKT kama Jeshi la Akiba walishiriki kikamilifu vita hivyo.

Licha ya ushindi, Taifa lilipata changamoto za kiuchumi kwani lilitumia rasilimali nyingi kupigana vita hivyo. Wakati linapambana kuimarisha uchumi wake, kulitokea mtikisiko wa uchumi duniani kwenye miaka ya themanini na tisini ulioathiri pia Tanzania kiuchumi na kusababisha Serikali kusitisha baadhi ya shughuli kutokana na ufinyu wa Pato la Taifa.

Hali hiyo ilikuwa fursa kwa mataifa yaliyoendelea Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia

44 JKT (2013), Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

(WB), kutoa misaada na mikopo yenye masharti magumu na ya kinyonyaji kwa kivuli cha msaada kwa mataifa yanayoendelea.

Kutokana na masharti hayo Tanzania ililazimika kusimamisha shughuli na huduma katika baadhi ya taasisi zake ikiwamo mafunzo ya JKT ambapo mwaka 1992 mafunzo kwa Kundi la Kujitolea yalisitishwa na kufuatiwa na Kundi la Lazima mwaka 1994.

Hatua hiyo iliilazimu JKT kufunga baadhi ya Kambi, kwa mfano, Milundikwa na Luwa, Rukwa; Mpwapwa, Dodoma; Makuyuni, Arusha; Itaka, Songwe na Msange Tabora. Kufungwa kwa Kambi hizo kuliathiri miundombinu ya uzalishaji na malezi ya Vijana.

Uzalishaji mali Vikosini na SUMAJKT pamoja na ulinzi viliendelea kutekelezwa na Maafisa na Askari ingawa kwa kiwango kidogo kwani nguvu kazi iliyokuwa inategemewa ni Vijana. Hata hivyo, uhusiano wa JKT na JKUZ, taasisi za ndani na nje ya nchi uliendelea.

Kukosekana kwa mafunzo ya JKT kulisababisha kuongezeka mmomonyoko wa maadili na Taifa

likashuhudia tabia na mwenendo usiofaa katika jamii pamoja na kuanza kupoteza mila na desturi za utamaduni wa Taifa.

## Mawaziri wa Ulinzi na JKT Mwaka 1973 – 2001



*Mhe. Edward Sokoine*
*(1972 – 1977)*



*Mhe. Rashid Kawawa*
*(1977 – 1980)*



*Mhe. Jenerali Abdallah Twalipo*
*(1980 -1982)*



*Mhe. Brigedia Jenerali Muhidin Kimario*
*(1982 – 1985)*



*Mhe. Dkt. Salim Ahmed Salim*
*(1985 – 1989)*



*Mhe. Jackson Makweta*
*(1989 – 1991)*



*Mhe. Amrani Mayagila*
*(1991 – 1991)*



*Mhe. Kanali Abdulrahman Kinana*
*(1991 – 1995)*



*Mhe. Edgar Maokola-Majogo*
*(1995 – 2000)*



*Mhe. Prof. Philemon Sarungi*
*(2000 – 2005)*

## Wakuu wa JKT Mwaka 1973 – 2001



*ACP Nelson Mkisi*
***(1973-1975)***



*Meja Jenerali Nelson Mkisi*
***(1975-1989)***



*Meja Jenerali Makame Rashid*
***(1989 – 2001)***

**Mafanikio**

Katika kipindi cha 1973 hadi 2001, JKT ilifanikiwa ifuatavyo:

- Katika mwaka 1973 hadi 1980, Kikosi cha Ujenzi kilishiriki katika ujenzi wa miradi ifuatayo:
    - Ujenzi wa nyumba 46 za JWTZ Lugalo, soko la Nachingwea, ofisi ya TANU Musoma, vituo tisa vya afya Kigoma.
    - Ofisi za Makao Makuu ya Serikali Dodoma na kituo cha wenye ulemavu Nunge, Dar es Salaam.
    - Kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Cuba, walijenga shule za sekondari za kilimo Kilosa, Ifakara, Ruvu na Kibiti.
- Vijana wa JKT walishiriki uokoaji kwenye mafuriko wilayani Rufiji, Pwani mwaka 1974.
- Kuanzisha sekondari Mgulani mwaka 1974 iliyobadilishwa jina kuwa Jitegemee mwaka 1985
- Kuanzisha Kambi mpya za Mbweni mwaka 1974, Luwa 1977, Mgambo na Chita 1978.
- Kushiriki vita vya Kagera mwaka 1978/79.

- Kuongeza Vikosi vinne vya Ujenzi; Kinyerezi, Dar es Salaam; Veyula, Dodoma; Uyole, Mbeya na Kibiti, Pwani mwaka 1979/80.
- Kuanzisha shule ya msingi kwa Maafisa, Askari na raia mwaka 1980 hadi 1987 Mlale, Ruvuma.
- Kuanzisha SUMAJKT mwaka 1981.
- Kwa upande wa michezo JKT ilitoa mabingwa kitaifa na kimataifa kwa mfano:
  - Sajini Zakayo Malekwa, bingwa wa kurusha mkuki wanaume, mashindano ya "All African Games" mwaka 1977.
  - Sajini Catherine Nyamko, bingwa wa kurusha kisahani na tufe wanawake mashindano ya Taifa mwaka 1977.
  - Luteni Emmanuel Ndyemandoi bingwa wa mbio za marathoni mashindano ya Afrika Mashariki na Kati ya Somalia mwaka 1982.
  - Mteule II Josephine Nate Nangai (akiwa praiveti), bingwa wa riadha meta 3,000 wanawake, mashindano ya Taifa na mshindi wa nafasi ya tatu katika mashindano ya Afrika

Mashariki yaliyofanyika Nairobi, Kenya mwaka 1982.

- Sajini Taji Benjamin Mwangata, bingwa wa ndondi uzito wa 'fly' mashindano ya Taifa mwaka 1986 na 1987 na mshindi wa tatu mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Nairobi, Kenya mwaka 1987.
- Sajini Taji Matilda Kisava (akiwa praiveti), bingwa wa kurusha mkuki wanawake kitaifa mwaka 1986 na mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yaliyofanyika Nairobi, Kenya mwaka 1987.
- Kutoa wanamichezo wanne bora mwaka 1987 kati ya sita waliotangazwa kitaifa ambao ni:
  - ❖ Sajini Zakayo Malekwa
  - ❖ Sajini Kisava
  - ❖ Praiveti Mwangata
  - ❖ Praiveti Nangai
- Meja Hamad Mallesa (akiwa praiveti), bingwa wa riadha meta 200 mashindano ya majeshi Afrika yaliyofanyika Blantyre, Malawi mwaka 1996.

- Vijana 314 walipelekwa Makambako kwa kazi maalumu ya ulinzi wa reli ya TAZARA mwaka 1979/80.
- Katika kusaidia mamlaka za kiraia, mwaka 1980 hadi 1987 Vijana 5,851 walishiriki Operesheni Linda Jiji Dar es Salaam wakisaidiana na Jeshi la Polisi kufanya doria mitaani.
- Mwaka 1983 hadi 1984, Vijana walishiriki kwa mafanikio kupambana na wahujumu uchumi.
- Nidhamu kwa wanavyuo na watumishi wa umma ilidumishwa licha ya uchumi kutetereka kutokana na matukio kama vita vya Kagera mwaka 1978/79 na ukame mwaka 1984/85.
- Kuanzisha sekondari ya Kawawa mwaka 1994.
- Kuanzisha Chuo cha Ufundi Stadi (VET) Makutupora mwaka 1996 na Maramba 1997.

**Changamoto**

Licha ya mafanikio yaliyopatikana changamoto zifuatazo zilijitokeza:

- Mtaji mdogo wa kuendesha SUMAJKT. Licha ya changamoto hiyo, Shirika lilitekeleza uzalishaji na

kuongeza mtaji kadri rasilimali fedha ilivyopatikana.

- Kilimo cha kutegemea mvua. Hali hiyo ilitumiwa kama fursa ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji JKT Ruvu na kukiendeleza katika vikosi vingine.
- Upungufu wa wataalamu wa kilimo, mifugo na ufundi uliendelea. Kutatua changamoto hiyo, vyuo vya kilimo na mifugo Mpwapwa, Mafinga na ufundi Mgulani vilianzishwa.
- Kusitishwa mafunzo ya JKT kulikosababisha kupungua kwa uzalishaji mali vikosini na SUMAJKT. Hata hivyo, shughuli hizo ziliendelea kufanywa na Maafisa na Askari kuepusha uharibifu wa miundombinu.

## JKT Mwaka 2001 hadi 2013

Oktoba 2001, Serikali ya Awamu ya Tatu ilirejesha mafunzo kwa Vijana wa kujitolea kwa miaka miwili. Kundi la kwanza baada ya kurejeshwa mafunzo hayo lilipewa jina la Operesheni Mkapa likiwa na Vijana 2,491, baada ya hapo operesheni zingine zilifuata.



*Mhe. Benjamin William Mkapa,*
*Rais wa Awamu ya Tatu.*

Katika kuboresha mafunzo, JKT ilianzisha Chuo cha Uongozi (CUJKT) mwaka 2004 katika Kikosi cha Ruvu ili kuandaa Maafisa, Askari na Vijana viongozi watoe mafunzo yanayoendana na wakati husika, kwani malezi ya Vijana yanahitaji maadili maalumu. Mwaka 2011, Chuo hicho kilihamishiwa Kimbiji, Dar es Salaam.[45] CUJKT imeongozwa na Makamanda mbalimbali na sasa ni Kanali Stanslaus Mishako.

Hali ya usalama katika Wilaya za Kibondo na Kasulu ilitetereka miaka ya 2000 baada ya wakimbizi kutoka

45 JKT (2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa

nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) waliokuwa katika Kambi za Umoja wa Mataifa za Kanembwa na Mtabila kurejeshwa kwao kwa hiari, kwani kambi hizo zitumiwa na magenge ya kihalifu.

Mwaka 2008 Kanembwa ilikabidhiwa JKT na baadaye Mtabila ikafuata mwaka 2012 ili kufanya uzalishaji mali na ulinzi katika maeneo hayo.

Mwaka 2013 Serikali ilirejesha mafunzo ya Vijana wa kundi la lazima kwa miezi mitatu. Kundi la kwanza la mafunzo hayo lilipewa jina la **Operesheni Miaka 50 ya JKT** yakiwa na jumla ya Vijana **4,696,** baada ya hapo operesheni zingine zilifuata.

Faida za mafunzo ya JKT ziliendelea kuonekana dhahiri hali iliyochangia baadhi ya wanasiasa wakiwemo wabunge vijana kuhamasika na kuomba kufanya mafunzo hayo 2006.[46] Mwaka 2013 ombi hilo lilipata kibali na wabunge 22 kutoka vyama mbalimbali vya siasa walifanya mafunzo katika Vikosi vya Ruvu,

46 JKT (2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa

Bulombora, Mgambo na Msange kuanzia Machi 5-26 2013. Wabunge hao ni:

- Mhe. Mendrad Kigola
- Mhe. David Silinde
- Mhe. Easter Bulaya
- Mhe. Murtaza Mangungu
- Mhe. Yusuph Haji Khamis
- Mhe. Neema Hamis
- Mhe. Halima Mdee
- Mhe. Livingstone Lusinde
- Mhe. Said Mtanda
- Mhe. Sabreena Sungura
- Mhe. Seleman Jafo
- Mhe. Mariam Kasembe
- Mhe. Mariam Msabaha
- Mhe. Yahaya Kasim Issa
- Mhe. Zitto Kabwe

- Mhe. Raya Khamis
- Mhe. Dkt. Anthony Mbassa
- Mhe. Idd Azzan
- Mhe. Abdallah Hajji Alli
- Mhe. Meshack Mfukwa
- Mhe. Rita Kabati
- Mhe. Mwigulu Nchemba



*Vijana wakiapa baada ya mafunzo ya ukakamavu katika moja ya Kambi za JKT.*

Baada ya kurejeshwa mafunzo ya Vijana wa kujitolea, JKT ilianza uzalishaji kwa kutumia mbinu bora za kilimo, mifugo na uvuvi. Mafunzo hayo kulichangia ongezeko la uzalishaji Vikosini na SUMAJKT.

JKT iliendelea kujipambanua katika tasnia ya michezo kwa kuanzisha timu ya JKT Queens Football Club mwaka 2004. Timu hiyo ilianzishwa katika Kikosi cha Makutupora, Dodoma na mwaka huohuo ilishiriki mashindano ya majeshi Zanzibar na kutwaa ubingwa.

Ushirikiano wa JKT na JKUZ uliimarika mwaka 2001, baada ya aliyekuwa Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume kushiriki uzinduzi wa kiwanda cha TANZASINO akiwa mgeni rasmi na kuagiza kuimarishwa ushirikiano baina ya vyombo hivyo.[47]

Utekelezaji wa agizo hilo ulifuatiwa na kuundwa Kamati ya Ushirikiano kati ya JKT na JKUZ, kisha kuzinduliwa rasmi MMJKU Zanzibar Juni 19, 2001. Mwaka 2007 Katiba ya Kamati ya Ushirikiano ilizinduliwa na ndiyo inayoongoza ushirikiano huo hadi sasa.[48]

47 JKT (2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

48 Kama ilivyorejewa hapo juu.

# Mawaziri wa Ulinzi na JKT Mwaka 2001 – 2013



*Mhe. Prof. Philemon Sarungi*
(2000-2005)



*Mhe. Prof. Juma Kapuya*
(2005 – 2007)



*Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi*
(2007 – 2012)



*Mhe. Shamsi Vuai Nahodha*
*(2012 – 2014)*

# Wakuu wa JKT Mwaka 2001 – 2013



*Meja Jenerali Davis Mwamunyange*
*(2001 – 2006)*



*Meja Jenerali Abdulrahman Shimbo*
*(2006 – 2007)*



*Meja Jenerali Martin Madata*
*(2007 – 2008)*



*Meja Jenerali Samuel Kitundu*
*(2008 – 2012)*



*Meja Jenerali Samweli Ndomba*
*(Machi 2012 – Septemba 2012)*



*Meja Jenerali Raphael Muhuga*
*(2012 – 2016)*

**Mafanikio**

Katika kipindi hicho, mafanikio yafuatayo yalipatikana:

- Kurejeshwa mafunzo ya Kujitolea mwaka 2001 na Lazima mwaka 2013.
- Kurejeshwa Kambi ya Msange mwaka 2009.
- Kuanzishwa Kambi mpya za Kanembwa mwaka 2008 na Mtabila mwaka 2012.
- Kuanzisha CUJKT mwaka 2004.
- Wabunge 22 kutoka vyama vya siasa walihamasika na kufanya mafunzo katika Kikosi cha Ruvu mwaka 2013.
- Ari ya Vijana kufanya mafunzo kwa kujitolea iliongezeka na hadi mwaka 2013, Operesheni 12 zilifanyika kwa ufanisi.

## Jedwali Na. 3 Vijana Waliofanya Mafunzo 2001 hadi 2013

| Na. | Operesheni | Mwaka | Kujitolea | Lazima | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mkapa | 2001 | 2,491 | _ | 2,491 |
| 2. | Miaka 40 ya JKT | 2002 | 2,613 | _ | 2,613 |
| 3. | Utandawazi | 2004 | 2,794 | _ | 2,794 |
| 4. | Jiajiri | 2005 | 3,355 | _ | 3,355 |
| 5. | Kasi Mpya | 2006 | 2,454 | _ | 2,454 |
| 6. | Maisha Bora | 2007 | 3,905 | _ | 3,905 |
| 7. | Uadilifu | 2008 | 4,184 | _ | 4,184 |
| 8. | Kilimo Kwanza | 2009 | 4,414 | _ | 4,414 |
| 9. | Uzalendo | 2010 | 4,432 | _ | 4,432 |
| 10. | Miaka 50 ya Uhuru | 2011 | 5,596 | _ | 5,596 |
| 11. | Sensa 2012 | 2012 | 5,898 | _ | 5,898 |
| 12. | Miaka 50 ya JKT | 2013 | 6,818 | 15,201 | 22,019 |

## Changamoto

- Ukosefu wa umeme na maji kwa baadhi ya Vikosi na Kambi. Katika kutatua changamoto hiyo, JKT ilifanya mazungumzo na Mamlaka ya Usambazaji Umeme Vijijini (REA) ili kuweka umeme katika Vikosi na Kambi hizo. Hatua nyingine iliyochukuliwa ni ununuzi wa vifaa vya umeme jua na matumizi ya jenereta katika Vikosi. Aidha, katika kutatua changamoto ya maji, JKT ilichimba visima katika Vikosi vilivyokuwa na shida hiyo.

- Mabadiliko ya tabianchi yaliendelea kuathiri uzalishaji hasa katika sekta ya kilimo. JKT ilianzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kiwango cha wastani katika Kambi za Chita na Ruvu.
- Migogoro ya ardhi kwa baadhi ya maeneo ya Vikosi iliyotokana na uvamizi wa wananchi baada ya kusitishwa shughuli za JKT mwaka 1994. Juhudi za kutatua migogoro hiyo kisheria zilichukuliwa ikiwamo uwekaji wa mabango na alama za mipaka.

# SURA YA PILI

## KUIMARIKA KWA JKT

KUANZIA mwaka 2013 hadi 2023, JKT imeendelea kuimarika katika kutekeleza majukumu yake. Kuimarika huko kunazingatia umuhimu wa kushirikisha Vijana kwenye maendeleo ya Taifa kulingana na mabadiliko katika jamii.

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Tanzania ina idadi ya watu zaidi ya milioni 61 likiwa ni ongezeko la asilimia 3.2 kwa mwaka kuanzia mwaka 2012.[49] Kwa mujibu wa takwimu hizo, idadi kubwa ya wananchi wana umri chini ya miaka 45 ambao ndio walengwa wa JKT.

Ili kujenga nchi kimkakati kwa kuzingatia uwiano wa idadi ya watu kijinsia, umuhimu wa JKT ni mkubwa katika kulea kizazi cha sasa na kijacho.

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2019, hutambua mchango wa kijana katika maendeleo ya jamii na kumwainisha

49 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (2022), Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi, Ofisi ya Takwimu ya Taifa, Dodoma.

kama wa kiume au kike, mwenye umri wa kati ya miaka 18 - 35.[50]

Umri huo huenda sambamba na uliotajwa katika Sheria ya JKT Sura ya 193 kama ilivyorejewa mwaka 2002 (The National Service Act, Cap 193 RE 2002 – katika Kitabu hiki itarejewa kama NSA CAP 193).[51]

Na ndio umri mahususi wa Vijana unaotegemewa kwa kiasi kikubwa katika jamii na hivyo JKT kuwapa kipaumbele katika kupewa mafunzo ambayo baadaye watayatumia katika kuleta mabadiliko katika jamii.

Katika miaka 60, JKT inajivunia kuwa taasisi inayojenga uzalendo, kutafsiri kiuhalisia mifumo ya malezi bora, uchumi, ulinzi na usalama, kuwa moja ya mikakati na hatua muhimu ya Serikali kuandaa Vijana kwa maendeleo yao binafsi na Taifa kwa ujumla.

Uwepo wa mifumo ya ushirikishwaji Vijana kwenye ujenzi wa Taifa katika nchi nyingi, ni taswira ya mifumo ya kale ya ulinzi na ushirikishwaji Vijana kujenga jamii bora.

---

50 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (2007), Sera ya Maendeleo ya Vijana, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Dar es salaam.

51 The National Service Act, Cap 193 RE 2002. Rejea kifungu cha 4(2) (a) na (b) cha NSA Cap 193.

Nchini Tanzania mfumo wa kale ulikuwa chini ya machifu wa makabila uliotumika kupambana na Wakoloni. Mfano Chifu Mkwawa wa Wahehe (Iringa), Chifu Chaburuma wa Wangoni (Ruvuma) na Mtemi Mirambo wa Wanyamwezi (Tabora).[52]

Mifumo hiyo inaonekana dhahiri hata leo katika mila na desturi za makabila nchini. JKT kwa sasa inatafsiriwa kuwa jando na unyago jumuishi la Taifa kwa Vijana kutoka mikoa na makabila mbalimbali.

Jukumu hili nyeti, huhusisha Vijana waliogawanyika katika makundi matatu; la kujitolea, la lazima na maalumu.

**Kundi la Kujitolea**

Vijana wa kundi la kujitolea hupatikana baada ya Mkuu wa JKT kuutangazia umma nafasi za kujiunga, ambazo kwa uwiano hugawiwa katika mikoa yote nchini kwa kuzingatia elimu, jinsia na sifa zingine zinazoainishwa na Mkuu huyo.

Utaratibu wa kuandikishwa Vijana hao huanzia ngazi ya kata hadi mikoa, baadaye MMJKT hufanya usaili ili

52 JKT (2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

kujiridhisha, iwapo wanakidhi vigezo muhimu kama vile uraia, utimamu wa mwili na taaluma zao, kama inavyokuwa imeainishwa katika tangazo la Mkuu wa JKT.

Vijana wa kundi hili hufanya mafunzo kwa miaka miwili. Miezi minne ya kwanza ni ya ukakamavu na miezi 20 ni ya stadi za kazi na maisha. Baada ya kuhitimu hurejea nyumbani kujitegemea wakiwa raia wema na wazalendo katika jamii.

**Kundi la Lazima**

Vijana wa Kundi la Lazima ambalo lilizoeleka kama mujibu wa sheria, hupatikana baada ya Mkuu wa JKT kutoa mwito kwa Vijana wa Tanzania Bara waliohitimu elimu ya kidato cha sita kila mwaka, ili kujiunga na mafunzo.[53] Vijana hawa hufanya mafunzo kwa miezi mitatu kabla ya kujiunga na masomo ya elimu ya juu.

Mafunzo ya JKT kwa Kundi la Lazima yalirejeshwa rasmi mwaka 2013 na Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete ilipoona umuhimu wa

53 JKT. (2012) Mwongozo wa Malezi ya Vijana.

Vijana waliohitimu kidato cha sita kufanya mafunzo hayo.



*Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete,*
*Rais wa Awamu ya Nne.*

Katika kipindi cha mafunzo ya lazima, Vijana hujifunza ukakamavu na stadi za kazi kwa pamoja. Mafunzo hayo hufuata mtaala unaotumika kwa kundi

la Kujitolea na hufanikiwa kwa kiwango stahiki kwa miezi mitatu kwa sasa.

Hata hivyo, Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine iko kwenye mchakato wa kuangalia uwezekano wa kuongeza muda kwa kundi hili, kutoka miezi mitatu hadi mwaka mmoja, ili kuliwezesha kupata mafunzo haya muhimu kwa muda wa kutosha.

**Kundi Maalum**

Huhusisha viongozi au watumishi wa Serikali na wasio wa Serikali wanaoteuliwa kufanya mafunzo ya JKT kwa sababu za kimkakati. Muda wa mafunzo hutegemea maelekezo ya Serikali.



*Baadhi ya watumishi wa ofisi ya Bunge la Tanzania waliofanya mafunzo ya JKT katika Kikosi cha Makutupora, Dodoma mwaka 2021.*

**Jedwali Na. 4 Watumishi wa Taasisi Mbalimbali**

| Na. | Operesheni | Mwaka | Taasisi/Wizara | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Tanzania ya Viwanda | 2017 | Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (sasa Mambo ya Nje na Afrika Mashariki) | 32 |
| 2. | Uchumi wa Kati | 2020 | Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 39 |

**Wadau katika Malezi ya Vijana**

Malezi ya Vijana ni jukumu mtambuka likihusu wazazi, wizara, taasisi na asasi za Serikali na zisizo za Serikali, taasisi za kidini na kila Mtanzania kwa ujumla wake. Malezi huanza mtoto anapozaliwa, kukua, kujiunga JKT na baada ya kuhitimu mafunzo.

Wadau ni muhimu katika kulea Vijana kwa sababu JKT si kisiwa, inatekeleza majukumu yake kwenye jamii, hivyo ni muhimu kushirikiana na wadau wengine ili kuhakikisha matokeo ya mwisho ya malezi ya Vijana yananufaisha wote.

Ikumbukwe, kuwa baada ya kuhitimu mafunzo, Vijana hutakiwa kurejea kwao na wengine hujiunga na elimu za juu, baadhi huajiriwa na taasisi, mashirika ya Serikali na yasiyo ya Serikali. Lakini pia wapo wanaojiajiri wakitumia fursa zilizopo kwenye mazingira wanamoishi.

Taasisi zenye watumishi waliopitia mafunzo ya JKT, ni mashuhuda wa utendajikazi, uzalendo na uadilifu wa watumishi hao. Kwa umuhimu huo, ni vema taasisi za kidini, kiraia, kielimu, Serikali na wadau kuunga

mkono malezi ya Vijana na kufikiri jinsi ya kuwatumia baada ya kuhitimu mafunzo.

Baadhi ya taasisi zimeliona hilo na kuwajibika, kwa mfano Wizara ya Kilimo kuanzia mwaka 2021/22 ilianza mpango wa mashamba nundu na Vijana waliohitimu mafunzo ya JKT walipewa kipaumbele.

Hali kadhalika, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) linaendelea na mchakato wa kuwezesha Vijana waliohitimu JKT kwa kuwapa mitaji ili wajitegemee na kupunguza utegemezi wa ajira serikalini.

Vijana ni chachu ya mabadiliko hasa katika kipindi hiki ambacho Ulimwengu unapitia changamoto kubwa ya mmomonyoko wa maadili na kukithiri kwa vitendo vya rushwa, matumizi ya madawa ya kulevya, ukatili wa kijinsia, ushoga, ulawiti, ubakaji na mengine.

Kwa jinsi hiyo wanahitaji ufahamu wa kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kabla, wakati na baada ya kuhitimu JKT. Masuala mengine muhimu ni ufahamu kuhusu utii bila shuruti, utunzaji mazingira, kutoa

msaada katika majanga, ustawi wa jamii, kilimo, mifugo, afya na mengineyo.

Iwapo kila mmoja atabeba jukumu la malezi kama mdau na kushirikiana na JKT, kitatengenezwa kizazi bora kitakachobadilisha mtazamo na kuwa na mwelekeo mpya wa Taifa utakaodumisha mila na utamaduni, uzalendo, utu, udugu, utaifa na uzalishaji mali kwa maslahi ya Taifa.

**Fikra kwa Vijana wa JKT**

Vijana waliofanya mafunzo ya JKT wamekuwa wakitazamwa kwa fikra tofauti kitaifa na kimataifa, ikizingatiwa kuwa nchi zingine pia zina utaratibu wa kuandaa Vijana wao kama Tanzania na zisizo na mpango huu zinatamani kuuanzisha.

**Kitaifa**

Mwanasaikolojia na mwandishi maarufu wa Marekani, Wayne Walter Dyer, alisema: "Mtazamo ni kila kitu, kwa hiyo chagua ulio mzuri." Kimsingi kila jambo au uamuzi wowote uwe binafsi au wa kitaasisi, hutegemea mtazamo wa mhusika, ndiyo maana ni muhimu kutafakari na kuwa na mtazamo mzuri.

Kitaifa kuna mitazamo miwili; chanya na hasi. Mtazamo chanya unatambua thamani ya malezi kwa Vijana yanayojenga uzalendo. Madhara kwa Taifa lisilo na Vijana wazalendo ni makubwa.

Vijana waliofanya mafunzo ya JKT ni mfano dhahiri wa uzalendo, nidhamu, uchapakazi, uwezo wa kujitegemea, uaminifu, ushirikiano, umoja na ustahimilivu katika taasisi na jamii kwa ujumla. Hata Vijana wenyewe wanaona fahari kupata fursa hiyo adhimu.

Kijana wa kike 'Service Girl' AKM 0061 Kuruta Janeth Kabonge wa JKT Mpwapwa, Dodoma alithibitisha hayo alipohitimu mafunzo ya ukakamavu akisema: "Kuja kwangu JKT nimejifunza vitu vingi kama vile ukakamavu na ujasiri. Mimi si mwoga tena, nimejifunza pia ujasiriamali, kilimo na ufugaji ambavyo vimenijengea uzalendo na sasa hata nikimaliza mkataba nikarudi nyumbani, nina uwezo wa kuangalia fursa zilizopo na nikaendesha maisha yangu mwenyewe."

Baada ya Serikali kurejesha mafunzo ya Kundi la Lazima mwaka 2013, migomo kwa watumishi wa taasisi na wanavyuo wa elimu ya juu imepungua kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na kipindi ambacho mafunzo hayo yalisitishwa (1994 – 2013). Kwa sasa Vijana na watumishi wanapokumbana na changamoto wamekuwa wavumilivu na wenye subira wakati matatizo yao yanashughulikiwa.

Kwa mtazamo huu, mafunzo ya JKT ni fursa kwa Vijana kujengewa uzalendo, kujitegemea na kuwa tayari kupokea majukumu ya uongozi wa ngazi mbalimbali katika Taifa.

Mtazamo hasi ni wa kundi la wachache wanaodhani Vijana waliofanya mafunzo ya JKT lazima waandikishwe au kuajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama. Wengine hudhani mafunzo ya JKT ni magumu, hivyo kuzuia watoto wao kushiriki.

Kimsingi, JKT haiandai watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama pekee, bali huandaa Vijana kuwa tayari kwa kazi yoyote halali katika jamii.

Hayo yanathibitishwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere katika hotuba yake kwenye Mkutano Mkuu wa 15 wa TANU Taifa mwaka 1971 aliposema: "Kwa msingi wake, JKT si Jeshi la kivita. Kazi yake ni kusaidia katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu, na wakati huo huo kuwapa wanajeshi hao (Vijana) elimu ya kisiasa na ya ufundi, na kuwajengea tabia ya kujitawala, ambayo watakwenda nayo baada ya kumaliza mafunzo hayo."[54]

Rais na Amiri Jeshi Mkuu mstaafu, Mhe. Mwinyi katika hotuba yake kwa makamanda wa JWTZ kwenye ukumbi wa Msasani Beach Club, Dar es Salaam Novemba 25, 1986, alisisitiza, kuwa wajibu wa Mkuu wa JKT ni kufunza Vijana ukakamavu, kilimo, ufugaji, kutengeneza zana ndogo na kuwalea katika maadili bora ya Taifa.

Aliongeza, kuwa JKT ni mahali pazuri pa kuanzia kuvunja fikra iliyopandikizwa na Wakoloni, iliyofanya wananchi kupeleka watoto wao shuleni, ili waondokane na kazi ngumu kama ya kilimo, lakini sasa wasomi

54 Hotuba ya Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere akiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi katika Mkutano Mkuu wa TANU WA TAIFA wa 15 Mwaka 1971.

wameelewa kuwa kilimo humpa mtu fedha kila siku, badala ya mfanyakazi anayepata mshahara mara moja kwa mwezi.[55]

Kwa muktadha huo, JKT si daraja la kupitishia Vijana kupata ajira kwenye vyombo vya ulinzi na usalama pekee, bali ni mahali salama pa kuwapa mafunzo stahiki kulingana na mahitaji ya sasa, maadili bora na utaifa, ili kufaa katika hali zote kiuchumi, kijamii na kiuongozi.

**Kimataifa**

Mataifa yenye nguvu ni yaliyojengwa katika uzalendo, yaani kwenye nyoyo za watu, ndiyo maana mataifa mengi huhakikisha watoto, Vijana na jamii nzima zinajengwa katika msingi wa uzalendo kwanza, licha ya kuwa na Jeshi kubwa, uchumi mzuri, wasomi, diplomasia, demokrasia bora na uwezo wa kihabari. Taifa lisilowekeza kwenye nyoyo za watu ni Taifa lililoshindwa.

Nitin Namdeo, mwandishi na mbunifu maarufu wa India, alisema: “Nguvu ya Taifa haitokani na watu

55 Hotuba ya Amiri Jeshi Mkuu kwa Makamanda wa JWTZ katika Ukumbi wa Makamanda Msasani Beach Club Tarehe 25 Novemba 1986.

wenye bunduki, bali wenye maono ya kuleta mabadiliko." Kwa maana hiyo, watu wenye maono huandaliwa na kulelewa, ili wawe kama jamii husika inavyotaka.

Mtazamo wa kimataifa unaiona Tanzania kuwa nchi yenye amani, utulivu na uzalendo, unaotokana na msingi wa malezi yanayotolewa na JKT hata kufanya baadhi ya mataifa kuja kujifunza ili nao waanzishe taasisi zinazofanana na JKT.

Malezi ni njia ya ukuzaji mtoto akitarajiwa kufuata tabia na mwenendo mwema.[56] Pia, ni kutunza na kulinda mtu kwenye makuzi. Hali kadhalika ni matunzo, kutiwa moyo na usaidizi kwa mtu anapokua. Utafiti unaonesha kwamba malezi ni muhimu zaidi kuliko asili katika kujenga tabia ya mtoto.[57]

Malezi ni dhana pana, jukumu maalumu, muhimu na la muda mrefu ambalo hutolewa kwa Kijana katika kukabiliana na maisha.

56 Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (2013), Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la 3. Oxford University Press, East Africa Limited, 2013. Nairobi, Kenya.

57 Hornby, Albert Sydney, Oxford Advanced Learners Dictionary of Current English, Oxford University Press. 1995.

Jukumu hili ni mtambuka, ambalo familia au mlezi huhitaji msaada wa jamii na Taifa kwa ujumla ili kuhakikisha anayelelewa hatimaye anakuwa na maadili mema.

Nia ni kupata mafunzo kwa pamoja ili wakihitimu wasibaguane kwa makabila, dini, elimu, utajiri au umasikini wao, bali watambuane kama kundi moja lenye uzalendo kwa maslahi ya Taifa.

Hayo yamethibitishwa na hotuba ya Baba wa Taifa kwenye mkutano wa TYL, Dar es Salaam mwaka 1965 katika ukumbi wa Arnautoglu, aliposema: "JKT ni mfano wa jungu kubwa ambalo Vijana wa Tanzania wenye tabia na mwenendo tofauti, watalelewa na kuwa Vijana wa Taifa moja lenye nguvu, tabia na mwenendo sawa, akifafanua kuwa chombo hicho kitakuwa na jukumu la kutayarisha Vijana kuwa na ari ya kujitolea siku zote, kwa nguvu zao zote, ili kushiriki kuendeleza Taifa hili changa."[58]

Kwa muktadha huo, malezi ndani ya JKT, ni mchakato muhimu wa kitaifa wa kuandaa Vijana kuwa wazalendo

58 JKT (1973) Miaka 10 ya JKT

wenye uadilifu, ustahimilivu, ushirikiano, ubunifu, utayari, moyo wa kupenda kazi, uwezo wa kujitegemea, ukakamavu na ujasiri, ili kutumikia Taifa ipasavyo.

**Malezi ya Vijana wa JKT**

Malezi ya Vijana huanza siku ya kwanza wanapojiunga na mafunzo hadi mwisho wa mkataba wao.[59] Malezi haya ni mpango wa Serikali kuhakikisha Vijana wanakuwa Wazalendo na wanaojitegemea.

Kwa mujibu wa Mwanafalsafa maarufu wa Kigiriki, Aristotle, tabia njema kwenye ujana huonesha tofauti kubwa katika maisha ya mtu. Hivyo, mafunzo katika kipindi hicho ni muhimu kwani humjenga na kumtofautisha na wengine.

Vijana hawa ni wenye sifa za kujiunga na JKT kama itakavyokuwa imeainishwa na Mkuu wa JKT kwa maelekezo ya Serikali na hufanya mafunzo ya ukakamavu na utimamu wa mwili, masomo ya Uraia, huduma ya kwanza, ujasiriamali, kilimo, ufugaji wanyama, nyuki, samaki na uvuvi.

59 Jeshi la Kujenga Taifa (2012) Mwongozo wa Malezi ya Vijana.

Pia, hufunzwa ufundi umeme, uashi, kuchomelea vyuma, umakanika, ushonaji, kutengeneza majokofu, viyoyozi, n.k. kwenye Vikosi vyenye Vyuo vya Ufundi Stadi. Masomo mengine ni uhifadhi wa mazingira, kuzima moto na uokoaji, UKIMWI na magonjwa mengine ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

Kushiriki majukumu mengine ya kitaifa kama vile ujenzi katika miradi ya kimkakati, kutoa msaada kwa mamlaka za kiraia, majanga, maafa, sherehe kama magwaride, michezo, kuchangia damu salama, n.k. Pia, ni sehemu ya malezi kwa Vijana hao ili waelewe kuwa wao ni sehemu ya watekelezaji majukumu hayo na kufahamu wajibu wao katika jamii na Taifa.

**Tofauti ya Aliyelelewa na Asiyelelewa JKT**

Kuna tofauti kubwa kati ya kijana aliyefanya mafunzo ya JKT na ambaye hakupata fursa hiyo kama inavyothibitishwa na wadau wanaonufaika na matunda ya wahitimu wa mafunzo ya JKT kama vile familia, waajiri, jamii na wahitimu wenyewe.

**Uzalendo** ni tunu ya Taifa, ambayo ndilo lengo kuu la Serikali kwa Vijana. Mafunzo ya JKT hulenga

kumfanya Kijana kuipenda kwa dhati nchi yake, kuithamini, kujitoa kwa moyo wote na ikibidi kuwa tayari kufa kwa ajili ya nchi yake. Humfundisha Kijana kutanguliza maslahi ya nchi.



*Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajab Mabele akisisitiza umuhimu wa uzalendo kwa Vijana wa Kujitolea katika moja ya Kambi za JKT.*

Kijana aliyelelewa na JKT ni mzalendo, mwaminifu na mwenye upendo kwa Watanzania wenzake, aliye tayari kuitetea nchi yake na kuibua uozo kwenye jamii, kushirikiana na wenzake kufanikisha malengo bora. Pia, kutokuwa mharibifu au mfujaji mali, kupenda

utamaduni wake, asili yake, bidhaa au mazao ya nchini mwake na mengine yanayofanana na hayo.

Haya yanakamilishwa na usemi maarufu wa Plato, Mwanafalsafa mkongwe wa Kigiriki aliyesema kwamba elimu ni mafunzo ya ubora tangu ujana, ambayo humfanya mtu kuwa na shauku kubwa ya kuwa raia kamili, na kumfundisha kutawala na kutii kwa haki na hii ndiyo elimu pekee inayostahili.

Nidhamu ni sifa mojawapo ya kumtofautisha kijana aliyefanya mafunzo ya JKT na wengine. Kijana huyo ana adabu na nguvu inayomsukuma kufanya mambo kwa kujituma, kwa wakati, umakini, ujuzi na usahihi ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Mafunzo ya JKT humwondolea kijana msomi hali ya kujiona bora na kudharau wenye elimu ya chini na ubinafsi, hivyo kushirikiana na kuheshimu watu wote bila kujali elimu, cheo au kipato.

Vilevile, **ustahimilivu** kwa Vijana waliofanya mafunzo hayo, huwatofautisha na wengine, kwani humudu mihemko na hasira. Hii hutokana na mazingira ya mafunzo wanayopitia na huwafanya kuhimili changamoto na mikiki ya maisha, kukazana kujitafutia riziki halali na kutokuwa na tamaa.

Vijana hao wanapenda kufanya kazi na kuona matokeo ya wanachokifanya. Kijana wa aina hii anaweza

kutumwa kazi muda wowote na akaifanya bila malalamiko.

Hivi sasa Vijana wasomi wamekuwa wakizunguka kutafuta ajira baada ya kuhitimu elimu ya juu. Hata hivyo, baada ya Vijana wengi wasomi kufanya mafunzo ya JKT wameonekana kujishughulisha na kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara na ujasiriamali.





*Vijana wakishiriki mafunzo ya uzalishaji mali katika moja ya Vikosi vya JKT.*



*Kijana wa JKT Ruvu, Pwani akikusanya mayai kizimbani.*

Hali kadhalika Vijana waliofanya mafunzo ya JKT ni **wakakamavu** na wenye uwezo wa kuwa na tahadhari za kiusalama na kumudu majukumu ya kawaida.



*Vijana wa JKT wakifanya mafunzo ya ukakamavu.*

**Kujali muda** ni dhana inayotofautisha Vijana wenye mafunzo ya JKT na wasionayo. Muda jeshini ni jambo lenye thamani kubwa, kwani ni tafsiri ya ushindi vitani na katika mipango yoyote.

Mtumishi au mtu asiyejali muda, kufanikiwa kwake kuna walakini, kwani mara nyingi huchelewa kufanya uamuzi sahihi na kwa wakati sahihi.

Kwa miaka 60, JKT imekuwa chombo adhimu cha malezi ya Vijana kuwaandaa kuwa wazalendo na viongozi wa baadaye. Kwa sasa mtaala wa mafunzo umeboreshwa ili kwenda na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na kuongeza muda wa mafunzo ya stadi za kazi kutoka miezi 18 hadi 20.

Desemba 2016, JKT ilirejesha Vikosi vitano vya Makuyuni, Arusha; Milundikwa na Luwa, Rukwa; Mpwapwa, Dodoma na Itaka, Songwe na Oktoba 2019, ilianzisha kimoja kipya cha Kibiti, Pwani kwa juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano ikiongozwa na Mhe. Dkt. John Magufuli ili kuiwezesha JKT kutoa mafunzo kwa Vijana wengi zaidi.



***Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli,***
***Rais wa Awamu ya Tano.***

Pia, miundombinu katika Vikosi imekuwa ikiboreshwa ili kutoa mafunzo kwa Vijana wengi zaidi. Juhudi za kuhakikisha Vijana wote wahitimu wa kidato cha sita wanafanya mafunzo ya JKT zimefanyika kwani mwaka 2023 Vijana hao wameitwa wote kufanya mafunzo hayo.




*Jengo la Utawala JKT Luwa, Rukwa.*



*Jengo la Utawala JKT Mpwapwa, Dodoma.*



*Jengo la Utawala JKT Makuyuni, Arusha.*



*Jengo la Utawala JKT Itaka, Songwe.*



*Jengo la Utawala JKT Milundikwa, Rukwa.*




*Jengo la Utawala JKT Kibiti, Pwani.*

Vikosi vya JKT viko maeneo yanayotoa fursa kwa Vijana kujifunza na kupata ujuzi wa kuanzisha shughuli za kiuchumi wanapomaliza mafunzo. Vikosi vinaendelea kubuni miradi zaidi ili kuwapa Vijana ujuzi. Fursa hizo zinatokana na uwepo wa:-

- Ardhi ya kutosha kwa ajili ya mashamba darasa.
- Wataalamu wa kilimo, mifugo na fani za ujuzi.
- Miradiyakilimo,mifugo,uvuvi,hudumana biashara.
- Miundombinu ya mabwawa ya samaki na viwanda vidogo vidogo.

JKT inaendesha mafunzo ya Ufundi Stadi kupitia Vikosi vyenye vyuo vilivyosajiliwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Vikosi vinavyoendesha mafunzo hayo ni Mgulani, Dar es Salaam; Makutopora, Dodoma; Maramba, Tanga na Kanembwa, Kigoma. Katika vyuo hivyo, kozi za ujuzi hutolewa kwa Vijana zikiwamo useremala, uashi, umeme, umakanika, udereva, ushonaji na zingine.

Ili kuhakikisha Vijana wanaohitimu JKT wanapata mafunzo ya ufundi stadi, ambapo umeanza mchakato wa kuanzisha chuo kikubwa cha mafunzo

hayo wilayani Kongwa, Dodoma na hatimaye kuwezesha kila Kikosi kuwa na chuo cha aina hiyo.

Kwa kutambua kuwa michezo, sanaa na utamaduni ni nyenzo muhimu katika kuiunganisha jamii, kielelezo na utambulisho wa Taifa, JKT imeendelea kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo Jeshini ili kuendeleza ushindani na sifa kwa Taifa.

Kurugenzi ya Elimu, Michezo na Utamaduni ya JKT ndiyo huratibu michezo ili kuimarisha afya, ushirikiano, upendo, udugu, nidhamu, ukakamavu, burudani na elimu kwa umma.

Huduma za afya kwa Maafisa, Askari, Vijana, Watumishi wa umma na jamii hupewa kipaumbele ili kuboresha afya zao. Katika hilo, JKT imejenga zahanati, imenunua vifaa tiba na vitendanishi, na kuhakikisha uwepo wa wataalamu stahiki katika Vikosi vyote.

Kwenye uzalishaji mali, jitihada zimeendelea kufanyika kuwezesha JKT kuzalisha kwa ufanisi zaidi na kutekeleza shughuli zinazoongeza tija na matokeo makubwa katika dira na sera ya kilimo, mifugo na uvuvi mkakati.

### Jedwali Na. 5: Uzalishaji Misimu ya 2015/16 -2016/17

| Na. | ZAO | 2015/16 | | 2016/17 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ekari | Mavuno (Tani) | Ekari | Mavuno (Tani) |
| 1. | Mahindi | 1,802 | 711.83 | 1,702 | 1,200.87 |
| 2. | Mpunga | 500 | 300 | 600 | 166 |
| 3. | Maharage | 50 | 1.63 | 371 | 27.68 |
| 4. | Alizeti | 217 | 21.31 | 160 | 25.47 |

### Jedwali Na. 6: Uzalishaji Misimu ya 2017/18 - 2018/19

| Na. | ZAO | 2017/18 | | 2018/19 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ekari | Mavuno (Tani) | Ekari | Mavuno (Tani) |
| 1. | Mahindi | 2,531 | 1,167.30 | 2,957 | 1,224.84 |
| 2. | Mpunga | 490 | 58.10 | 620 | 273.84 |
| 3. | Maharage | 284 | 35.36 | 295 | 30.33 |
| 4. | Alizeti | 444 | 28.78 | 444 | 54.76 |

Msimu wa mwaka 2018/19 JKT ilifanya mageuzi ya kilimo kwa kuanzisha mpango mkakati wa kupanua wigo wa mashamba, kwa kutumia mbinu bora na ununuzi wa zana za kisasa. Ilifanya hivyo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Tume ya Taifa Umwagiliaji (NiRC), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na wadau wengine. **(Maelezo zaidi Sura ya Tatu).**

**Jedwali Na. 7. Mitambo, Zana na Magari Yaliyonunuliwa**

| Na. | Mtambo/Zana/Gari | JKT | JWTZ | Wizara ya Ulinzi na JKT | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Combined harvester | - | - | 02 | 02 |
| 2. | Planter | 02 | - | 08 | 10 |
| 3. | Boom sprayer | 03 | - | 08 | 11 |
| 4. | Harrow | 04 | - | 08 | 12 |
| 5. | Leveler machine | 01 | - | 02 | 03 |
| 6. | Rotter vetter | 04 | - | 02 | 06 |
| 7. | Trekta | 10 | - | 08 | 18 |
| 8. | Fertilizer spreader | 02 | - | 02 | 04 |
| 9. | Seed drill | 00 | - | 02 | 02 |
| 10. | Disc plough | 05 | - | 08 | 13 |
| 11. | Magari ya utawala | 50 | 05 | 03 | 58 |
| 12. | Magari ya mizigo | 01 | 27 | 00 | 28 |

Sekta ya mifugo na uvuvi imepewa kipaumbele katika mkakati, baada ya kuanzisha ufugaji wa samaki kwa njia ya matangi katika shamba la Chita na vizimba Rwamkoma. Vilevile, kwa kutumia fedha za maendeleo JKT imefufua boti ya uvuvi ya MV Bulombora itakayotumika kuvua samaki Ziwa Tanganyika.

Mpango huo pia unatekeleza mwito wa Serikali wa kilimo cha mazao ya kimkakati na uzalishaji mbegu

bora na miche ya mazao mbalimbali ambayo ni michikichi Bulombora, Kigoma; mikorosho Makutupora, Dodoma na Nachingwea, Lindi; mibuni Rwamkoma, Mara na Itende, Mbeya; mkonge Mgambo na Maramba, Tanga.

Pia, mpango huo unatumika kama nyenzo ya kufundisha Vijana stadi za kazi ili kujitegemea baada ya kumaliza mafunzo, kuongeza uzalishaji na kujitosheleza kwa chakula na kuchangia uchumi wa viwanda.

Hayo yamewezekana kutokana na jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita inayoendelea kuiwezesha JKT kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.



*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,*
*Rais wa Awamu ya Sita.*

SUMAJKT imeimarika zaidi katika uzalishaji mali kupitia ujenzi, kilimo, mifugo, uvuvi, uhandisi na ushauri, viwanda, huduma na biashara. Inachangia kupunguza gharama za uendeshaji wa malezi ya Vijana na Pato la Taifa kwa kutoa gawio serikalini.

Kuanzia mwaka 2013 hadi 2023, ushirikiano kati ya JKT na JKUZ umeimarika zaidi kwa kusaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano wa Kiuchumi katika nyanja za kilimo, ujenzi, uhandisi, biashara, mafunzo na teknolojia.

Hati hiyo ilisainiwa Juni 4, 2015[60] na pande hizo mbili zinaendelea kushirikiana katika mafunzo, michezo, kubadilishana uzoefu, uzalishaji mali, vikao vya uongozi, utamaduni na mengineyo.



***Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele na wa JKUZ, Kanali Makame Abdalla Daima wakiwa JKT Rwamkoma, Mara katika mahafali ya Vijana wa Kundi la Kujitolea 'Operesheni Venance Mabeyo' Machi 2023.***

60 Jeshi la Kujenga Taifa (2012) Mwongozo wa Malezi ya Vijana.

Katika jukumu la ulinzi, JKT imedumisha ushirikiano na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kulinda maeneo muhimu kama ilivyofanyika mwaka 2016, Vijana waliposhiriki uokoaji kwenye tetemeko la ardhi Bukoba, Kagera.

Kuanzia mwaka 2019 hadi 2023, Maafisa na Askari wanaendelea na maandalizi ya ulinzi wa miundombinu ya bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga.

Vilevile, JKT iko tayari muda wote kutoa msaada kwenye maafa na majanga.



*Vijana wa JKT wakishiriki uokoaji katika moja ya ajali za barabarani.*

JKT kama sehemu ya JWTZ hushiriki mazoezi ya medani yanayoratibiwa na Brigedi za JWTZ, kwa mfano, zoezi la 'Miaka 50 ya JWTZ' mwaka 2014, 'Linda Mpaka' na 'Kazi Iendelee'mwaka 2022, 'Kaa Tayari' mwaka 2023 na mengineyo.

## Mawaziri wa Ulinzi na JKT Mwaka 2013 hadi Sasa



*Mhe. Shamsi Vuai Nahodha*
*(2012 – 2014)*



*Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi*
*(2014 – 2020)*



*Mhe. Elias Kwandikwa*
*(2020 – 2021)*



*Mhe. Dkt.Stergomena Tax*
*(2021- 2022)*



*Mhe. Innocent Bashungwa*
*(2022 hadi sasa)*

# Wakuu wa JKT Mwaka 2013 hadi Sasa



*Meja Jenerali Raphael Muhuga*

*(2012 – 2016)*



*Meja Jenerali Michael Isamuhyo*

*(2016-2018)*



*Meja Jenerali Martin Busungu*

*(2018-2019)*



*Meja Jenerali Charles Mbuge (2019-2021)*



*Meja Jenerali Rajabu Mabele (2021 hadi sasa)*

**Mafanikio**

Katika kipindi cha mwaka 2013 – 2023, JKT imepata mafanikio yafuatayo:-

- Kurejesha Vikosi vya zamani vitano; Makuyuni, Luwa, Milundikwa, Itaka na Mpwapwa mwaka 2016 na kuanzisha kimoja Kibiti mwaka 2019.
- Kuboresha mtaala wa mafunzo ya stadi za kazi kwa Vijana wa Kujitolea, kwa kuongeza masomo ya ujasiriamali na muda wa mafunzo hayo kutoka miezi 18 hadi 20.
- Kutoa mafunzo maalumu ya JKT kwa watumishi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa

Afrika Mashariki mwaka 2017 na ofisi za Bunge mwaka 2020.

- Kuanzisha Chuo cha Ufundi Stadi (VET Kasanda) kilichoko Kanembwa, Kigoma mwaka 2022.
- Vikosi kuanzisha miradi ya kibiashara ili kupata faida inayoviwezesha kutekeleza majukumu yanayohitaji rasilimali fedha na kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama za uendeshaji.
- Kupitia mashamba na miradi darasa imesaidia kupunguza gharama za Serikali kwenye bajeti ya chakula kutoka Sh.10,000 hadi Sh. 8,500 mwaka 2015; kutoka Sh. 8,500 hadi Sh.4,500 mwaka 2016 na kutoka Sh. 4,500 hadi Sh. 3,000 mwaka 2020 kwa siku kwa kila Kijana.
- Kuanzisha mpango mkakati wa kilimo kwenye mazao ya chakula na biashara.
- Kujenga miundombinu ya kisasa vikosini kama vile maghala, mabweni ya Askari makapera na Vijana, nyumba za Makamanda Vikosi, ofisi za utawala na zahanati.
- Kujenga Kituo cha Huduma na Burudani kiitwacho Jenerali Venance Salvatory Mabeyo Complex, Dodoma.




*Kituo cha Huduma na Burudani cha Jenerali Venance Salvatory Mabeyo Complex kilichoko Dodoma.*

- Kununua magari na mitambo ya kisasa kama vile 'Combine Harvester', 'planter', 'boom sprayer', 'harrow', 'leveler machine', 'rotter vetter', trekta, n.k.
- Kununua eneo, kujenga MMJKT Chamwino Dodoma mwaka 2017 na kuhamia mwaka 2019.
- Kuongeza idadi ya Vijana wa kujiunga na mafunzo ya JKT.

## Jedwali Na. 8. Vijana Waliofanya Mafunzo 2014 hadi 2023

| Na. | Operesheni | Kundi la Kujitolea | Kundi la Lazima | Mwaka | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Miaka 50 ya Muungano | 8,430 | 31,692 | 2014 | 40,122 |
| 2. | Kikwete | 7,232 | 19,990 | 2015 | 27,222 |
| 3. | Magufuli | 10,665 | 14,865 | 2016 | 25,530 |
| 4. | Mirerani | 11,388 | 19,895 | 2017 | 31,283 |
| 6. | Makao Makuu Dodoma | 10,979 | 20,413 | 2019 | 31,392 |
| 7. | Samia Suluhu | 11,891 | 25,503 | 2021 | 37,394 |
| 9. | Jenerali Venance Mabeyo | 11,358 | 25,171 | 2022 | 36,529 |

- Kupima maeneo ya Vikosi vyote vya JKT kuepuka migogoro ya ardhi.
- Kufufua MV Bulombora.



- Kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) katika Operesheni ya kutengeneza vitambulisho vya Taifa ifuatavyo:
  - Mwaka 2014 Vijana 1,000.
  - Mwaka 2018 Vijana 200.
- Vijana kushiriki utekelezaji miradi ya kimkakati ya Serikali:
  - Ujenzi wa ukuta Mirerani kilometa 24.5.
  - Ujenzi wa ukuta uwanja wa ndegevita Ngerengere, Morogoro.
  - Ujenzi wa bandari kavu Kwala, Pwani.
  - Ujenzi wa Ikulu Chamwino, Dodoma mwaka 2019/23.
  - Ujenzi wa Shule ya Mfano Iyumbu, Dodoma.
  - Ujenzi wa jengo la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), 2019.
  - Ujenzi wa MMJKT Dodoma, mwaka 2018/19.
  - Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa, Kikombo.
  - Ujenzi wa nyumba 41 za makazi ya watumishi wa Ikulu Chamwino, mwaka 2019.

  - Ujenzi wa nyumba 402 Msomera, Handeni, Tanga mwaka 2022. Nyumba 400 ni za makazi ya wananchi waliohama Ngorongoro kwa hiari na nyumba mbili kwa ajili ya Kituo na makazi ya Polisi.
  - Kusafisha eneo la ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP) Rufiji, Pwani mwaka 2020.
- ➢ Kuwa mshindi wa jumla katika maonesho ya biashara (Sabasaba) na kilimo (Nanenane) mara kwa mara.
- ➢ Katika michezo, JKT imefanikiwa ifuatavyo:
  - Kijana Alphonce Simbu (sasa Sajini) alikuwa mshindi wa tatu wa mashindano ya mbio za riadha 'Mumbai Marathon' yaliyofanyika Jijini Mumbai, India mwaka 2017.
  - Mshindi wa jumla mashindano ya Kombe la Mkuu wa Majeshi (CDF Cup) mwaka 2017, 2018 na 2019.
  - Mshindi wa jumla mashindano ya Baraza la Michezo ya Majeshi Tanzania (BAMMATA) mwaka 2017, 2018 na 2023.

- Mshindi wa jumla Michezo ya Majeshi ya Afrika Mashariki mwaka 2017, 2018 na 2023.
- Ujenzi uwanja wa mpira wa miguu wa Meja Jenerali Michael Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam mwaka 2017.
- Ukarabati wa viwanja vya mpira wa mikono na wavu Mbweni, mwaka 2017.
- Timu ya mpira wa miguu ya JKT Tanzania kushiriki mashindano ya Ligi Kuu Tanzania.
- Timu ya mpira wa miguu wanawake ya JKT Queens kutwaa ubingwa wa mashindano ya Ligi Kuu Tanzania mwaka 2017/18, 2018/19 na 2022/23. Pia, kushiriki mashindano ya Majeshi ya Dunia mwaka 2023.
- Kuandaa kwa mafanikio mashindano ya mbio za riadha za JKT Marathon 2023 kwa umbali wa kilometa 5, 10 na 21.1 zilizofanyika Jijini Dodoma na kushirikisha watu zaidi ya 2000 kutoka nchi nzima.



*Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete (katikati) Rais wa Awamu ya Nne akiwa na Mhe. Dkt. Tulia Ackson (kushoto) Spika wa Bunge la Tanzania na Mhe. Innocent Bashungwa (kulia) Waziri wa Ulinzi na JKT wakati wa mbio za JKT Marathon 2023 zilizofanyika Jijini Dodoma.*



***Maafisa, Askari na Vijana wakishiriki michezo na mazoezi ya viungo.***








*Vijana wa JKT wakishiriki katika sanaa na utamaduni.*

**Changamoto**

JKT inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Upungufu wa miundombinu na zana za kisasa za mafunzo na uzalishaji. Hata hivyo, JKT inaendelea kununua zana kadri hali ya uchumi inavyoruhusu.
- Muda mfupi wa mafunzo ya Vijana kwa Kundi la Lazima wa miezi mitatu kwa sasa ambao ni mfupi na unaingiliana na kipindi cha udahili wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu, hivyo kuathiri mafunzo. Licha ya ufinyu wa muda, JKT inahakikisha Vijana hao wanapata mafunzo stahiki kwa kuzingatia mtaala uliopo. Vilevile, Wizara ya Ulinzi na JKT inashirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine kuangalia uwezekano wa kuongeza muda kutoka miezi mitatu hadi mwaka mmoja kama ilivyokuwa awali, ili Vijana wapate mafunzo hayo kwa wigo mpana.
- Upungufu wa maghala ya mazao. Katika kutatua changamoto hiyo, JKT imeanza kujenga maghala ya kisasa kwa awamu vikosini. Kwa mfano, Chita, Milundikwa, Mlale na Makutupora.

- Mabadiliko ya tabianchi yamekuwa changamoto katika kufikia malengo ya uzalishaji wa mazao na kuathiri maeneo ya fukwe za bahari ya Hindi, kwa maji kuvamia maeneo ya Mbweni. Hivyo, JKT inashirikiana na wadau ambao ni taasisi za kilimo, mazingira na TMA na ujenzi wa skimu za umwagiliaji katika baadhi ya Vikosi ili kukabiliana na hali hiyo.

- Upungufu wa wataalamu unaathiri utekelezaji wa kilimo, ufugaji na uvuvi. Ili kuongeza wataalamu, JKT inatoa kipaumbele kwa Maafisa na Askari kusomea fani husika.

- Migogoro ya ardhi kati ya Vikosi na wananchi. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara ya Ulinzi na JKT inaendelea kupima maeneo ya Vikosi ili kupata hati miliki.

- Ukosefu wa viwanja vya mazoezi na uchakavu wa miundombinu iliyopo. JKT imeanza ukarabati na kujenga viwanja vya michezo ukiwamo wa Meja Jenerali Michael Isamuhyo, na vya mpira wa mikono na wavu Mbweni na vya mpira wa kikapu na netiboli Mgulani.

- UVIKO-19 ulioikumba Dunia mwaka 2019-2022, uliathiri ratiba za mafunzo kambini. Hata hivyo, JKT ilichukua tahadhari kama ilivyoshauriwa na wataalamu wa afya na kukinga Vijana dhidi ya maambukizi hayo na mafunzo yakaendelea kama kawaida.

# SURA YA TATU

## MPANGO MKAKATI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

JESHI la Kujenga Taifa limekuwa likiendesha uzalishaji kupitia kilimo, mifugo na uvuvi vikosini kama mashamba na miradi darasa kwa ajili ya mafunzo ya stadi za kazi kwa Vijana.

Idadi ya Vijana imekuwa ikiongezeka na kusababisha wengi kutaka kujiunga. Ongezeko hilo limeongeza mahitaji ya kuzalisha chakula kimkakati kwa matumizi ya Vijana, biashara na uhakika wa chakula nchini.

Mwaka 2019 JKT ilibuni na kuunda kamati chini ya Brigedia Jenerali Hassan Mabena wakati huo akiwa na cheo cha Kanali, iliyoanzisha mpango mkakati wa mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kamati hiyo ilifanya yafuatayo:

- Kupitia takwimu za uzalishaji vikosini na kuchagua maeneo na mazao mkakati ya kusaidia kufikia malengo ya kujitosheleza kwa chakula.
- Kuandaa andiko la kilimo, mifugo na uvuvi mkakati.

- Kusimamia upimaji mashamba ya kimkakati kwa 'GPS' ili kufahamu ukubwa halisi wa mashamba hayo.
- Kuzingatia matumizi ya teknolojia kwenye uzalishaji ikiwamo upimaji wa afya ya udongo, matumizi sahihi ya kanuni za sayansi ya uchumi wa kilimo, zana bora za kilimo, umwagiliaji na kuchakata mazao kibiashara.
- Kusimamia uzalishaji wa tija vikosini, ili kufikia na kuvuka malengo yaliyowekwa kimkakati.



*Mwenyekiti wa kamati ya mpango mkakati wa mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi Brigedia Jenerali Hassan Mabena (kulia) akisisitiza jambo kwa baadhi ya watendaji wa JKT katika shamba la mpunga lililoko Chita, Morogoro.*

## Malengo ya Mkakati

Mkakati huo ulizingatia uchambuzi na mahitaji ya hali halisi ulikuwa na malengo yafuatayo:

- Kuongeza uzalishaji wa mazao kwa tija na kujenga uwezo wa kujitosheleza kwa chakula.
- Kuwapatia Vijana mafunzo ya stadi za kazi na kuwajengea uwezo wa kujiajiri kupitia teknolojia mpya za uzalishaji.
- Uzalishaji wa mbegu bora ili kuongeza uhakika wa chakula nchini.
- Kuchangia uchumi wa viwanda kupitia shughuli za uzalishaji zitakazofanywa na JKT.
- Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na barabara.
- Ujenzi wa maghala.
- Ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao.
- Utoaji mafunzo kupitia mpango mkakati.

## Utekelezaji wa Mkakati

Mpango mkakati huu ulitekelezwa katika awamu mbili ifuatavyo:

**Awamu ya Kwanza**

Utekelezaji huu ulianza kwa dharura mwaka wa kwanza 2019/20 ili kupata uzoefu na kufanya maandalizi ya kina, kwa ajili ya awamu ya pili na uandaaji wa andiko kuonesha dira ya utekelezaji.

Pia, mpango huu ulianza kwa kuchambua na kutenga mashamba mawili ya kuanzia; shamba la Chita zilikolimwa ekari 1,000 za mpunga na la Milundikwa zilikolimwa ekari 1,000 za mahindi na 200 za maharage.



*Vijana wakihudumia shamba la mpunga Chita, Morogoro.*

## Awamu ya Pili

Awamu hii ndiyo inasimamia utekelezaji wa mkakati huu na inafanyika katika kipindi cha 2020/21-2024/25 ambapo mpango uliainisha maeneo tisa yatakayotumika kwenye uzalishaji na yanayofaa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 9: Maeneo na Mazao ya Mkakati**

| Na. | Kikosi | Zao | Eneo linalofaa kwa Kilimo (Ekari) | Eneo litakalolimwa (Ekari) | Maeneo ya umwagiliaji (Ekari) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Chita | Mpunga | 10,305 | 6,000 | 6,000 |
| 2. | Milundikwa | Mahindi | 3,700 | 3,000 | 1,000 |
| 3. | Luwa | Mahindi | 9,000 | 5,000 | 1,000 |
| 4. | Mlale | Mahindi | 3,777 | 2,000 | 2,000 |
| 5. | Oljoro | Maharage | 3,380 | 2,000 | 2,000 |
| 6. | Kanembwa | Maharage | 5,231 | 3,000 | - |
| 7. | Mgambo | Alizeti | 10,000 | 2,500 | - |
| 8. | Maramba | Alizeti | 4,599 | 500 | - |
| 9. | Msange | Alizeti | 5,000 | 2,500 | - |

## Jedwali Na. 10: Maeneo yenye Utekelezaji wa Mazao ya Mkakati

| Na | Kikosi | Zao | Msimu wa kilimo 2020/21 | | | Msimu wa kilimo 2021/22 | | | Msimu wa kilimo 2022/23 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ekari | Mavuno (Tani) | Matarajio (Tani) | Ekari | Mavuno (Tani) | Matarajio (Tani) | Ekari | Matarajio (Tani) |
| 1. | Chita | Mpunga | 1500 | 2,863.3 | 1,500 | 1821 | 955.6 | 1,821 | 3500 | 3500 |
| 2. | Milundikwa | Mahindi | 1500 | 1,629.5 | 1,500 | 1500 | 1,411.5 | 1,500 | 2,000 | 2,000 |
| 3. | Luwa | Mahindi | - | - | | - | - | - | 500 | 500 |
| 4. | Mlale | Mahindi | 1,000 | 1,181.3 | 1,000 | 1,000 | 1,250.6 | 1,000 | 1,222 | 1,222 |
| 5. | Oljoro | Maharage | 600 | 44 | 360 | 970 | 00 | 582 | - | - |
| 6. | Mgambo | Alizeti | - | - | - | 500 | 40.7 | 300 | 500 | 180 |
| | | Mahindi | 1,000 | 58.7 | 1,000 | - | - | - | - | - |
| | | Mkonge | 158 | - | - | 158 | - | - | 158 | |
| 7. | Bulombora | Michikichi | 800 | - | - | 800 | - | - | 800 | |
| 8. | Mtabila | Maharage | - | - | - | - | - | - | 300 | 180 |
| 9. | Makutupora | Alizeti | - | - | - | - | - | - | 700 | |

Utekelezaji wa mkakati huu unahusisha uendelezaji na uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mazao yatakayozalishwa na kuongeza idadi ya Vijana wanaojiunga na mafunzo. Vilevile, utahuisha mbinu za kuandaa Vijana ili kubadilisha fikra zao kuelekea kujiajiri na kuwa na mvuto kwa sekta mbalimbali kuwaajiri baada ya mafunzo yao. Hii itaongeza mchango wa JKT kwa jamii ikiwamo kuchakata mazao ya wakulima wanaozunguka maeneo ya viwanda vitakavyoanzishwa.

**Mafanikio**

Uanzishaji na utekelezaji wa mpango mkakati wa kilimo, mifugo na uvuvi, umeleta mafanikio makubwa hasa katika kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya JKT. Mpango huo umefanikiwa katika mambo yafuatayo:

- Ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Chita yenye uwezo wa kumwagilia takribani ekari 12,000 za mpunga na mahindi.

- Uanzishaji shamba kubwa na la kisasa la ufugaji samaki kwa njia ya matangi na uzalishaji wa vifaranga vya samaki Chita.
- Kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga Chita.
- Kuongeza uzalishaji wa mahindi katika Vikosi vinavyolima zao hilo kwa tija.
- Ununuzi wa zana za kisasa za kilimo. Mfano; matrekta, 'harrow', 'rotter vetter', 'planter', 'combine harvester', n.k
- Ujenzi wa maghala makubwa ya mazao katika Vikosi vya kilimo mkakati.
- Vijana kupata elimu ya kilimo cha kisasa na jinsi ya kutumia na kuifanyia matengenezo mitambo ya kilimo.
- Kuongeza ushirikiano baina ya JKT na taasisi zingine za kiserikali ikiwamo SUA, TARI kwenye utafiti wa mbegu.

**Changamoto**

Pamoja na mafanikio ya mpango mkakati huu, JKT inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

- Ufinyu wa bajeti ya utekelezaji. Hata hivyo JKT imekuwa ikitumia fedha kutoka vyanzo vyake vya ndani, kadri hali inavyoruhusu.
- Mabadiliko ya tabianchi katika baadhi ya maeneo yamechangia ukosefu wa mvua za kutosha, hivyo kuathiri mazao kwa baadhi ya misimu ya kilimo. Changamoto hii inaendelea kutatuliwa kwa kuanzisha skimu za umwagiliaji katika maeneo ya mkakati na kuwasiliana na TMA.
- Upungufu wa wataalamu wa fani za kilimo, mifugo na uvuvi. Katika kutatua changamoto hiyo, JKT imekuwa ikipata wataalamu kutoka JWTZ. Pia, kudhamini Maafisa na Askari wanaojiendeleza katika fani hizo na kushirikiana na taasisi kama TARI, NiRC na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI).

# SURA YA NNE

## SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA JESHI LA KUJENGA TAIFA

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) ni tawi la kiuchumi (Economic Wing) linalojishughulisha na uzalishaji mali kibiashara, ili kusaidia kupunguza gharama kwa Serikali katika kuendesha JKT.

SUMAJKT ilianzishwa Julai mosi, 1981 kwa Sheria ya Uanzishwaji Mashirika ya Kibiashara katika Taasisi za Umma (The Corporation Sole (Establishment) Act, No. 23 of 1974 Cap 119 RE 2002).

Shirika linazalisha mali kupitia sekta za ujenzi, kilimo, mifugo na uvuvi, huduma na biashara na viwanda. Linaendelea kuboresha miradi na kampuni zake, pia kuanzisha miradi mipya ili kuongeza mapato na kutekeleza majukumu yake.

### Chimbuko la SUMAJKT

SUMAJKT ilianzishwa kutokana na wazo la Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere akiwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania.[61] Alitoa wazo hilo mwanzoni mwa miaka ya sabini alipotembelea Kambi za JKT kujionea shughuli za mafunzo, malezi ya Vijana na uzalishaji mali. Moja ya Kambi alizotembelea ni Ruvu.



*Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akizungumza na Vijana alipotembelea Kambi ya Ruvu.*

Wakati huo, Kambi nyingi za JKT zilikuwa zikiathiriwa na uhaba au ucheleweshaji fedha za kujiendesha, hali iliyosababisha kutofikia malengo ya kuanzishwa kwao.

61 JKT (1973) Miaka 10 ya JKT

Ili kutatua tatizo hilo, Mwalimu Nyerere aliona umuhimu wa uzalishaji mali ndani ya JKT kuendeshwa kibiashara, hivyo aliagiza Wizara ya Ulinzi na JKT kulifanyia kazi wazo hilo.[62] Hii ilisababisha kuundwa Tume kuangalia jinsi mashirika na taasisi zingine za umma zinavyoendesha uzalishaji mali kibiashara.

Machi 1981, mawaziri walijadili Waraka wa Baraza la Mawaziri Namba 25 wa mwaka 1980 uliotayarishwa na Wizara ya Ulinzi na JKT, kuhusu kuundwa kwa Shirika la Kiuchumi.[63] Baada ya kuujadili, Rais alikubaliana na mapendekezo ya kuanzishwa Shirika la Uzalishaji Mali ndani ya JKT.

Baadhi ya majukumu yaliyoelekezwa SUMAJKT yalikuwa ni kufuatilia miradi ya uzalishaji mali iliyokuwa ikitegemea fedha kutoka serikalini, kupitia Bajeti ya Serikali, kuliwezesha Shirika kuwa na uwezo mkubwa kifedha wa kukopa na kukopesha, kuiongeza fedha za mitaji miradi iliyoonekana kuwa na uwezo wa kuzalisha zaidi, kuwezesha Shirika kuzalisha mali, kuuza na kutoa huduma kibiashara.

62 JKT (1988) Mika 25 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

63 Waraka wa Baraza la Mawaziri Namba 25, 1980.

Shirika lilitakiwa kufanya Upembuzi Yakinifu wa miradi ya uzalishaji mali iliyokuwa ikiendeshwa katika Kambi za JKT kabla ya kuichukua na kuiingiza kwake.

Upembuzi yakinifu ulitakiwa ufanywe kabla ya kuanzisha miradi mipya. Baada ya upembuzi huo kuonesha kuwa mradi uliolengwa unaweza kuleta faida, jukumu la Shirika lilikuwa kutoa mtaji au mkopo wa kuendesha mradi husika, kununua zana, pembejeo, kuongeza utaalamu wa uzalishaji na kutafuta masoko.

Kifungu cha 3 (1) cha sheria iliyoanzisha Shirika, ilimpa Rais mamlaka ya kutoa amri ya kuundwa shirika la kibiashara katika taasisi za umma.[64]

Shirika lilianzishwa rasmi kupitia Tangazo la Serikali Namba 94 la Julai mosi, 1981 na kuitwa SHIRIKA LA MKUU WA JKT. Tangazo hilo lilitoa orodha ya sekta za uzalishaji mali zitakazosimamiwa na Shirika, ingawa halikueleza madaraka ya Mkuu wa JKT katika muundo wake.[65]

Tangazo hilo lilifutwa, badala yake Amri ya Rais kupitia Tangazo lingine Namba 116 la Septemba 24,

64 The Corporation Sole (Establishment) Act, Cap 119, RE 2002.

65 JKT (2013) Miaka 50 cha Jeshi la Kujenga Taifa.

1982 lilichukua nafasi yake. Pamoja na kutaja sekta za uzalishaji mali zitakazosimamiwa na Shirika lilieleza kuwa Mkuu wa JKT atakuwa ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wake.

Shirika lilianza na vitengo tisa vyenye miradi 25. Ilipofika mwaka 1983 vitengo vingine saba vyenye miradi 14 viliongezwa, hivyo kuwa 16 vyenye miradi 39. Makamanda Vikosi walikuwa mameneja wa miradi iliyokuwa inaendeshwa katika kambi za JKT.

Mwaka 1985, Waziri wa Ulinzi na JKT alitoa mwongozo namba moja ukielekeza jina, anwani, nembo, muundo, watendaji na sifa wanazostahili kuwa nazo. Pia, ulifuta waraka na miongozo mingine ya awali ya uendeshaji Shirika.[66] Kuanzia mwaka huo, jina la Shirika lilibadilishwa na kuwa **Shirika la Uzalishaji Mali la JKT** badala ya Shirika la Mkuu wa JKT. Waziri wa Ulinzi na JKT alitoa miongozo mingine miwili; Namba 2/2003 na 3/2008.


Tangazo la Serikali Namba 116 la Septemba 24, 1982 lilifutwa, badala yake Amri ya Rais kupitia Tangazo la Serikali Namba 326 la Septemba 18, 2009 lilichukua nafasi yake.[67] Tangazo hili liliongeza wigo wa uzalishaji

66 Directive No. 1 of 1985.

67 The Corporation Sole (Chief of National Service) Order No. , 2009.

mali wa Shirika kwenye biashara ya nishati na madini, utalii, ulinzi binafsi, maduka makubwa, usindikaji matunda, uundaji mitambo na magari, huduma za elimu, biashara za magari, mashamba ya kilimo na mifugo na shughuli zingine zenye faida kwa Shirika.

# Muundo wa SUMAJKT



# Wakurugenzi Watendaji SUMAJKT Mwaka 1981 hadi Sasa



*Meja N Rehemtullah*
*(1981 hadi 1984)*



*Luteni Kanali James Luchunga*
*(1984 hadi 1995)*



*Brigedia Jenerali Alistarical Karubi*
*(1995 hadi 2003)*



*Kanali Martin Madata*
*(2003 hadi 2007)*



*Brigedia Jenerali Gerald Kiswaga*
*(2007 hadi 2008)*



*Kanali Ayoub Mwakang'ata*
*(2008 hadi 2013)*



*Brigedia Jenerali Mwanamakala Killo*
*(2013 hadi 2014)*



*Kanali Felix Samillan*
*(2014 hadi 2016)*



*Brigedia Jenerali Charo Yateri*
*(2016 hadi 2018)*



*Brigedia Jenerali Rajabu Mabele*
*(2018 - 2021)*



*Brigedia Jenerali Absolomon Shausi*
*(Mei 2021 hadi Desemba 2021)*



*Kanali Petro Ngata*
*(2022 hadi Sasa)*

## Maendeleo ya Shirika

### Mwaka 1981 hadi 1994

SUMAJKT ilianza kwa kuchukua baadhi ya miradi ya uzalishaji mali iliyokuwa inaendeshwa katika kambi za JKT kwa ruzuku kutoka serikalini, zilizotumika kuboresha miradi iliyopo na kuanzisha mipya. Wakuu wa vikosi hivyo, walikuwa na kofia mbili, yaani licha ya majukumu yao ya kawaida, pia walikuwa ni mameneja wa miradi ya uzalishaji mali katika vikosi vyao.

### Ruzuku ya Serikali

Kuanzia mwaka wa fedha 1981/82 hadi 1986/87, Serikali ilikuwa ikitoa ruzuku kwa Shirika kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:[68]

**Jedwali Na. 11: Ruzuku ya Serikali kwa SUMAJKT 1981/1987**

| Mwaka | Kiasi cha Fedha | Maelezo |
|---|---|---|
| 1981/82 | 6,000,000.00 | Fedha zilizotolewa na Serikali kuanzishia Shirika |
| 1982/83 | 8,320,000.00 | Fedha zilitolewa kuendesha miradi |
| 1983/84 | 7,645,000.00 | Fedha zilizotolewa kuendesha Shirika |
| 1984/85 | 25,501,000.00 | Sh. 18,000,000/= zilitolewa maalumu kwa ajili ya ununuzi wa matrekta 42 ya SUMAJKT. |
| 1985/86<br>1986/87 | 800,000.00<br>1,760,000.00 | Katika kipindi cha 1985/86 na 86/87 Serikali ilipunguza ruzuku kwa imani kwamba Shirika limeanza kujitegemea. |
| 1987/88 | - | Serikali iliagiza Shirika lijitegemee. |

68 JKT (2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Katika kipindi cha 1985/86 na 86/87, Serikali ilipunguza ruzuku kwa imani kwamba Shirika limeanza kujitegemea. Mwaka 1987/88 iliagiza Shirika lijitegemee.

Baada ya kusitisha ruzuku mwaka 1988, Shirika liliendelea kuzalisha mali kwa fedha zake, na kupata mafanikio katika sekta za kilimo, viwanda na ujenzi hadi shughuli za JKT kupitia vijana ziliposimamishwa.

**Mwaka 1994 hadi 2001**

Baada ya shughuli za JKT kusimamishwa, Shirika lilikabiliwa na upungufu wa nguvu kazi katika kuendesha miradi, hususan ya kilimo. Hata hivyo, uzalishaji uliendelea kwa kutumia nguvu kazi ya Maafisa na Askari.

Hali hii iliathiri kiwango cha uzalishaji mali, hivyo kusababisha wananchi waishio jirani na Vikosi kuvamia mashamba ya Jeshi baada ya kuona ardhi haitumiki kikamilifu. Hatua hii iliibua migogoro kati ya JKT na wananchi.

Ufinyu wa bajeti iliyotengwa kuendesha JKT ulisababisha huduma muhimu kwa Askari kupungua, hivyo Vikosi kulazimika kutumia mapato ya miradi ya SUMAJKT kujiendesha na kuathiri mtaji wa Shirika.

Juhudi za kuboresha uzalishaji mali katika sekta hii zilifanywa. Viwanda vilivyokuwapo vililenga kuingia ubia na kampuni za nje ili kuinua mtaji wa Shirika. Hivyo, likabuni mkakati wa kuingia ubia na viwanda vyake, kikiwamo cha ushonaji nguo cha Ruvu na kuanzishwa kingine cha dawa za binadamu cha TANZANSINO.[69]

Katika sekta ya ujenzi, juhudi za kupata miradi ya ujenzi kibiashara ziliongezwa baada ya wahandisi waliopelekwa Bulgaria kurejea nchini. Pamoja na changamoto zilizojitokeza, Shirika liliendelea kutekeleza shughuli zake.

### Mwaka 2002 hadi 2015

Kusimamishwa kwa shughuli za JKT kuliathiri pia uzalishaji mali. Hata hivyo, baada ya mafunzo

69 JKT (2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

kurejeshwa kwa Vijana wa Kujitolea mwaka 2001, SUMAJKT ilianza kustawi.

Mwaka 2001 Kambi za Ruvu na Makutupora zilianza kutoa mafunzo kwa Vijana wa kujitolea.[70] Kuwapo kwa Vijana hao kulifufua uzalishaji mali uliozorota kwa miaka saba. Makutupora ilifufua shamba la zabibu, wakati Ruvu ikiboresha ufugaji kuku.

Utaratibu wa awali wa kuwa na vitengo ndani ya JKT, hasa katika Vikosi na kambi ulibadilishwa. Mwaka 2009, SUMAJKT iligawanywa katika vitengo vikuu vitano vya uzalishaji, ambapo kila kitengo kilijitegemea kukusanya mapato, malipo na kupanga matumizi.[71]

Vitengo vilivyoanzishwa ni:

- Kitengo cha kilimo, mifugo na uvuvi.
- Ujenzi.
- Viwanda na biashara.
- SUMAJKT Guard.
- Mradi wa matrekta.

70 JKT (2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

71 SUMAJKT (2022) Miaka 41 ya SUMAJKT.

**Mwaka 2016 hadi 2023**

SUMAJKT ilianzisha idara mpya, ili kurahisisha utendaji na kuongeza ufanisi ifuatavyo:

- Naibu Mkurugenzi Mtendaji
- Kurugenzi ya Maendeleo, Mipango na Utafiti
- Kurugenzi ya Uhusiano

Ulitayarishwa Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano uliogawa miradi ya Shirika katika sekta nne. Kufikia mwaka 2023 SUMAJKT ilikuwa imegawanyika katika sekta za uzalishaji zifuatazo:[72]

- Ujenzi
- Kilimo, mifugo na uvuvi
- Viwanda
- Biashara na huduma

Miradi ilibadilishwa kuwa kampuni katika mgawanyo wa sekta zake nne ambazo ni:

- Kampuni ndani ya Sekta ya Ujenzi ni:-
    - SUMAJKT Electric Co. Ltd
    - SUMAJKT Consultancy Bureau Co. Ltd
    - SUMAJKT Batching Plant, Dodoma
    - SUMAJKT Kunduchi Stone Quarry Co. Ltd

72 SUMAJKT (2022) Miaka 41 ya SUMAJKT.

- ❖ SUMAJKT Construction Co. Ltd (SCCL) yenye kanda kumi ambazo ni:-
  - Ujenzi Kanda ya Mashariki
  - Ujenzi Kanda ya Kati
  - Ujenzi Kanda ya Kaskazini Magharibi
  - Ujenzi Kanda ya Kaskazini Mashariki
  - Ujenzi Kanda ya Ziwa Mashariki
  - Ujenzi Kanda ya Ziwa Magharibi
  - Ujenzi Kanda ya Magharibi
  - Ujenzi Kanda ya Kusini
  - Ujenzi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi
  - Ujenzi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mashariki

➢ Kampuni na miradi ndani ya Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni:

- ❖ SUMAJKT Agri-business Co. Ltd
- ❖ SUMAJKT Meat Supply Project
- ❖ SUMAPONICS
- ❖ SUMAJKTMngetaPlantation, Morogoro
- ❖ Usa River, Arusha

- Basouto Hanang, Manyara
- Shamba la ng'ombe wa nyama Misenyi, Kagera
- Shamba la ng'ombe wa nyama Oljoro, Arusha
- Shamba la ng'ombe wa maziwa Mafinga, Iringa
- Shamba la ng'ombe wa maziwa Oldonyo-Sambu, Arusha

➢ Kampuni katika Sekta ya Viwanda ni:-

- SUMAJKT Bottling Co. Ltd
- SUMAJKT Garments Co. Ltd
- SUMAJKT Chang'ombe Furniture Co. Ltd
- SUMAJKT ANIT ASFALT Co. Ltd
- SUMAJKT Shoe and Leather Products Co. Ltd. na
- SUMAJKT Mlale Milling Co. Ltd

➢ Kampuni na miradi katika Sekta ya Biashara na Huduma ni:-

- SUMAJKT Guard Ltd
- SUMAJKT Auction Mart Co. Ltd
- SUMAJKT Cleaning and Fumigation Co. Ltd
- SUMAJKT Catering and Services Co. Ltd
- SUMAJKT Insurance Broker Co. Ltd
- SUMAJKT Port and Services Co. Ltd

- SUMAJKT Skyzon Co. Ltd
- SUMAJKT Logistics Co. Ltd
- SUMAJKT Pharmaceutical Co. Ltd
- SUMAJKT Agri Machinery Project
- SUMAJKT Energies
- SUMAJKT Clearing and Forwading Agency.

SUMAJKT imekabidhiwa jukumu la kusimamia na kuendesha kibiashara huduma ya elimu kupitia sekondari za Jitegemee na Kawawa.

**Kazi za SUMAJKT**

Kazi zinazofanywa na Shirika zinalenga kukidhi malengo ya kuanzishwa kwake. SUMAJKT ilianzishwa ikiwa ni chombo maalumu ndani ya JKT kwa lengo la uzalishaji kibiashara, kusimamia na kukuza miradi ili kusaidia uendeshaji wa shughuli za JKT.

Utekelezaji wake umekuwa ni kipaumbele cha kuisaidia Serikali kupunguza matumizi ya kuendesha shughuli za JKT. Pia, hutoa gawio la fedha serikalini kila mwaka, ikiwa ni wajibu wa mashirika yote ya umma kufanya hivyo.

Hata hivyo, SUMAJKT hutekeleza malengo yake kupitia bidhaa zinazozalishwa na kutolewa huduma kwa jamii. Bidhaa na huduma hizo, hutoka sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, ujenzi viwanda, biashara na huduma za wataalamu wake, kwa ustadi na weledi wa hali ya juu.

**Miradi Inayotekelezwa**

Tangu kuanzishwa kwake SUMAJKT inaendelea kubuni, kuanzisha na kukuza uchumi kupitia uzalishaji, mauzo ya bidhaa na huduma kisekta ifuatavyo:

**Sekta ya Ujenzi**

Sekta hii, inaundwa na kutekeleza shughuli zake, kupitia kampuni zifuatazo:-

**Kampuni ya Ujenzi (SCCL)**

Shughuli za ujenzi zilianza mwaka 1969, baada ya JKT kuunda Brigedi ya Ujenzi, iliyokuwa na jukumu la ujenzi wa Kambi na nyumba za kupangisha za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) maeneo ya Magomeni na Kinondoni, Dar es Salaam kuanzia mwaka 1968 - 1973[73]

73 JKT (2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Kazi za ujenzi ndani ya JKT zilitambuliwa rasmi na Wizara ya Ujenzi, baada ya kukidhi sifa za ukandarasi, hivyo kusajiliwa na Bodi ya Ukandarasi (CRB) katika hatua zifuatazo:

- Kubadili jina kutoka Brigedi ya Ujenzi kuwa Idara ya Ujenzi ya JKT (NSCD).
- NSCD kuwa Mkandarasi Daraja la Tatu Januari 1998, baada ya kuanzishwa CRB mwaka 1997.
- Mwaka 2004, NSCD kupata usajili wa ukandarasi wa ujenzi wa barabara na utandazaji umeme daraja la nne.
- Mwaka 2004 baada ya kutekeleza kwa ufanisi mradi wa ujenzi wa nyumba 150 za watumishi wa Serikali Mbweni, Dar es Salaam, idara ilipandishwa daraja kutoka la tatu hadi la kwanza.
- NSCD ilitekeleza ujenzi, ukiwamo wa kitaifa kwa viwango na weledi mkubwa, hivyo ilipandishwa kuwa daraja la kwanza, hatua iliyosababisha kubadili jina na kuanzisha kampuni ya ujenzi ya SUMAJKT Construction Co. Ltd na ilisajiliwa BRELA Novemba 24, 2018.

- Kampuni ya Ujenzi ya SUMAJKT ilipata usajili wa wataalamu washauri katika fani ya usanifu majengo Desemba 22, 2017 kwa namba ya usajili APL 268:306.12/17 na wahandisi washauri Aprili 19, 2018 kwa namba 207 na uhandisi umeme kwa usajili namba E1/73/06/2020 Juni 2020.

Kampuni ya Ujenzi inaongozwa na Mkurugenzi Mwendeshaji (MD), ambaye huripoti kwa Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT.

Shirika linatekeleza ujenzi na uhandisi kupitia kanda zilizo chini ya SCCL. Utekelezaji wa majukumu ya ujenzi na uhandisi unafanikishwa kupitia kanda kumi ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

Pamoja na shughuli za miradi, SCCL inaratibu upatikanaji wa rasilimali ndani ya kampuni; zikiwamo fedha na vitendea kazi. Kwa pamoja kanda hizi za ujenzi zimefanikisha kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi, majengo ya ofisi na biashara, barabara na madaraja na miundombinu ya maji.



*Ofisi za Ikulu ya Chamwino, Dodoma zilizojengwa chini ya ukandarasi wa SUMAJKT.*

**Kampuni ya Ushauri Elekezi katika Majenzi**

Kampuni ya SUMAJKT Consultancy Bureau Co. Ltd. **(SCBCL)** ni mpya iliyotokana na uwepo wa wataalamu wa SCCL waliokuwa wakijihusisha na ubunifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi katika vitengo vitatu vya NSCD Archtects Archtectural Firm, NSCD Consulting Engineering Firm na SUMAJKT Quantity Surveying Firm.

Kampuni hiyo iliyopata usajili wa BRELA Mei 2021 na kufanya mabadiliko ya majina ya vitengo vilivyosajiliwa,[74] ambavyo ni:

- Wasanifu Majengo - Reg. No. APL 268.306.12/17
- Wakadiriaji Majengo - Reg. No. QPL 146.190.9/19
- Wahandisi Ushauri - Reg. No.207

SCBCL inaendelea kufanya kazi na SCCL na kampuni zingine za asasi za Serikali na binafsi.

**Kampuni ya Umeme (SECL)**

Kampuni hii ilianzishwa Juni 2020 kwa kutekeleza majukumu ya ndani ya kampuni ya ujenzi kwa usajili namba E1/73/06/2020. Baada ya kupata uzoefu na wataalamu wa kutosha, iliomba kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB) Daraja la Kwanza, ili kutekeleza usambazaji umeme na mifumo ya umeme.

74 SUMAJKT (2022) Miaka 41 ya SUMAJKT.



*Vijana wa JKT wakishiriki ujenzi wa miundombinu ya umeme wilayani Gairo, Morogoro.*

Januari 2022 ilisajiliwa upya na CRB kwa jina la SUMAJKT Electrical Co. Ltd na kupewa Namba ya Mlipa Kodi (TIN) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) (TIN: 138-235-653) na namba ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VRN:40033439-Y).

Sekta ya ujenzi imefanikisha miradi mingi. Baadhi ya miradi iliyokamilishwa hivi karibuni, ni jengo la Ofisi ya Ikulu ya Chamwino, Dodoma, NEC, ukuta wa Mirerani, ukuta wa kuzunguka Ikulu ya Chamwino, ukuta wa kuzunguka ofisi na makazi ya Waziri Mkuu,

Makao Makuu ya Uhamiaji, makazi ya viongozi wa Serikali, Dodoma na Dar es Salaam.

Kampuni imekuwa ikitumia teknolojia ya kisasa ya Ultimate Building Machine (UBM) kujenga baadhi ya majengo ya Serikali na binafsi. Miradi mingi ya Serikali ilitekelezwa kwa gharama nafuu na hivyo fedha ambazo zingetumika kujenga miradi hiyo kupelekwa kwenye huduma nyingine za kijamii.



*Jengo la kiwanda cha kutengeneza taa lililojengwa kwa teknolojia ya UBM lililoko Makao Makuu ya SUMAJKT Mlalakuwa, Dar es Salaam.*

**SUMAJKT Kunduchi Stone Quarry**

Kunduchi Stone Quarry Company Limited, ilianzishwa kama mradi mwaka 1973. Kipindi hicho mradi ulikuwa chini ya ujenzi Makao Makuu, Lugalo.

Mradi ulianzishwa ili kuzalisha bidhaa za ujenzi kama vile kokoto na matofali aina zote, kama *cubestone, fence louvers, paving block* na nguzo. Pia, ilikuwa kitivo cha mafundi jeshini.

Mradi ulisajiliwa BRELA kuwa kampuni Novemba 2020 na kuanza kazi kama kampuni rasmi Agosti 2021. Kwa sasa unazalisha matofali aina zote kulisha miradi inayotekelezwa na SUMAJKT na jamii kwa ujumla.

**Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

**Shughuli za Kilimo**

Shughuli za uzalishaji kupitia kilimo zilikuwapo na kuendeshwa kwenye Kambi za JKT. Mashamba vikosini yalisimamiwa na Makamanda Vikosi waliokuwa mameneja na chini yao kulikuwa na vitengo vitano; Siasa, Uhasibu, Ugavi, Mauzo na Utawala wa Kijeshi.

Kutokana na ukuaji wa kilimo na uzalishaji vikosini, Shirika limekuwa likitafuta na kumiliki mashamba na kuyahudumia.Mwaka 2021, Serikali ilikabidhi SUMAJKT shamba la ekari 14,000 likijulikana kama

Kilombero Plantation Limited (KPL) na sasa linaitwa SUMAJKT Mngeta Plantation.



*Shamba la mpunga la SUMAJKT Mngeta, Morogoro.*

Uzalishaji wa mpunga na mahindi katika shamba hilo ni wa kiwango kikubwa na hufanyika mwaka wote kutokana na miundombinu ya kisasa ya kilimo cha umwagiliaji, uhifadhi na kuongeza thamani ya mazao.[75]

Katika nyanja za kilimo, SUMAJKT imekuwa ikizalisha aina tofauti za mazao, ikiwamo alizeti na maharage katika shamba la Basoutu na mpunga

75 SUMAJKT (2022) Miaka 41 ya SUMAJKT.

shamba la Chita. Pia, kilimo cha mahindi ya mbegu na maua kupitia mashamba ya Mngeta na Usa River.




*Combine harvester ikivuna mpunga katika shamba la SUMAJKT Mngeta, Morogoro.*

## Mifugo

Shirika lilikuwa likiendesha ufugaji katika baadhi ya Kambi na Vikosi vya JKT kwa uwiano wa asilimia 60 kwa SUMAJKT na asilimia 40 kwa JKT.[76] Kwa awamu tofauti katika kuboresha utendaji wa majukumu bila mwingiliano, mgawanyo wa mashamba ya mifugo ulifanyika mwaka 2017.

76 JKT (2013) Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Sasa SUMAJKT inafuga ng'ombe wa maziwa katika mashamba ya Oldonyo Sambu na Mafinga ambako huzalishwa maziwa na kufanyika biashara ya mitamba.

Hali kadhalika, ng'ombe wa nyama katika Kikosi cha Oljoro na pia katika ranchi ya Misenyi ndani ya kiteule cha Misenyi, Kagera, SUMAJKT inafuga ng'ombe aina ya Boran kwa ajili ya nyama. Ufugaji mbuzi unafanyika katika viteule vya Misenyi na Mafinga.





***Baadhi ya mifugo katika shamba la SUMAJKT Mafinga, Iringa na ranchi ya Misenyi, Kagera.***

**Ufugaji Samaki**

Mwaka 2018 SUMAJKT ilianzisha ufugaji samaki kwa teknolojia ya Recirculating Aquaculture System (RAS) ambapo samaki hufugwa kwenye matangi katika Mbweni, Dar es Salaam kupitia mradi wa SUMAPONICS.

Mradi huu umekuwa mstari wa mbele kuzalisha vifaranga wa samaki na kuwauza kwa wananchi na kutoa elimu ya ufugaji huo kwa jamii, kwa kuwajengea mifumo ya matangi kwa gharama nafuu. Mifumo hii ni rahisi na hivyo kuwezesha vijana kujifunza teknolojia hii na kujiajiri.




*Ufugaji wa samaki kwa njia ya matangi kupitia mradi wa SUMAPONICS ulioko JKT Mbweni, Dar es Salaam.*

**Sekta ya Viwanda**

Uzalishaji bidhaa viwandani kwa ajili ya biashara ni moja ya shughuli kuu zinazoitambulisha SUMAJKT katika tasnia ya viwanda nchini. SUMAJKT imekuwa kichocheo kikubwa cha uzalishaji bidhaa katika sekta ya viwanda, hivyo kushiriki moja kwa moja katika utoaji ajira kwa jamii, sambamba na kukuza uchumi wa viwanda.

SUMAJKT ina viwanda sita vinavyoendelea na uzalishaji nchini; kiwanda cha mabati na misumari (SUMAJKT Roofing Co. Ltd) ukamilishwaji wake unaendelea kwa kupata eneo sahihi.[77]

**Kiwanda cha Samani**

SUMAJKT Chang'ombe Furniture Co. Ltd, iliyosajiliwa Machi 12, 2020, inamilikiwa na SUMAJKT kwa asilimia 100. Mwanzoni mwa miaka ya 1990, kilikuwa kiwanda pekee kilichosalia ndani ya SUMAJKT baada ya mtikisiko wa kiuchumi duniani.

Lengo la kiwanda ni kuzalisha samani bora kwa ajili ya JKT, JWTZ, vyombo vingine vya ulinzi na usalama na taasisi zingine za Serikali. Kiwanda kwa sasa kinatengeneza samani bora kwa ajili ya taasisi za

77 SUMAJKT (2022) Miaka 41 ya SUMAJKT.

Serikali, mashirika ya umma, kampuni binafsi na watu binafsi.



*Baadhi ya samani za ofisini zinazotengenezwa na kiwanda cha SUMAJKT Chang'ombe Furniture Co. Ltd.*

**Kiwanda cha Maji ya Kunywa**

Kiwanda cha Maji ya Kunywa (SUMAJKT Bottling Co. Ltd.) ni miongoni mwa viwanda vipya vilivyoanzishwa na SUMAJKT katika kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

Kiwanda kilizinduliwa rasmi Aprili 17, 2018, kinazalisha maji aina ya Uhuru Peak yenye ujazo tofauti; mililita 350, 500, 600, 1,000, 1,500 na 18,000. Kiwanda kinatoa huduma ya maji sehemu mbalimbali ikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama, taasisi za Serikali na watu binafsi.



*Mitambo ya kujaza maji ya kunywa ya 'Uhuru Peak' kwenye chupa iliyoko Mgulani, Dar es Salaam.*

**Kiwanda cha Ushonaji**

Kiwanda cha ushonaji cha SUMAJKT Garment Co. Ltd kilianza uzalishaji rasmi Aprili 22, 2017 na kusajiliwa kuwa kampuni Februari 27, 2020. Kiwanda

kinajihusisha na ushonaji mavazi kwa ajili ya vyombo vya ulinzi na usalama na kampuni binafsi.

Kiwanda hicho kimepunguza gharama za mavazi ya kijeshi kwa matumizi ya Askari wa JWTZ, JKT na ya Jeshi la akiba.



*Kiwanda cha SUMAJKT Garment Co. Ltd Mgulani, Dar es Salaam.*

**Kiwanda cha Kuchakata Nafaka**

SUMAJKT Mlale Milling Co. Ltd, inajihusisha na uchakataji nafaka za mahindi. Umiliki wa kampuni ulianza kwa ubia kati ya SUMAJKT na Kikosi cha JKT Mlale kwa uwiano wa asilimia 60 kwa 40 mtawalia. Kiwanda cha uchakataji nafaka cha kampuni hiyo kiko

Mlale, Songea. Kiwanda kina uwezo wa kuchakata mahindi takribani tani moja kwa saa.





*Kiwanda cha kuchakata nafaka Mlale, Songea.*

**Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi**

Kiwanda cha bidhaa za ngozi cha SUMAJKT Shoe and Leather Products Co. Ltd kilianzishwa rasmi Julai 13, 2017 na kinaendelea kutengeneza bidhaa za ngozi kwa matumizi ya taasisi za ulinzi, shule, kampuni na watu binafsi, na kiko Mlalakuwa, Dar es Salaam.

Mipango ya baadaye ni kuzalisha bidhaa zaidi za ngozi kama vile mikanda, mikoba na raba kwa ajili ya kuuza ndani na nje ya nchi.



*Mashine za kutengeneza soli za viatu katika kiwanda cha bidhaa za ngozi cha SUMAJKT Leather Product kilichoko Mlalakuwa, Dar es Salaam.*

**Sekta ya Biashara na Huduma**

Sekta ya biashara na huduma inajumuisha miradi na kampuni 12 ifuatavyo:

**Mradi wa Matrekta na Zana za Kilimo**

Mradi huu wa SUMAJKT Agri Machinery ni matokeo ya juhudi za Serikali katika kutekeleza mpango wa kuinua sekta ya kilimo kupitia kaulimbiu ya "Kilimo Kwanza" ya mwaka 2009.

Serikali ilipata mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya India wa dola za Marekani milioni 40.[78] SUMAJKT katika mpango huo, ilipewa jukumu la kupokea na kuratibu usambazaji wa matrekta na zana za kilimo, zinazopatikana kupitia mkopo huo. Hivyo, JKT ilianzisha mradi wa matrekta ili kutekeleza jukumu hilo la Serikali.

Mradi unatekelezwa kwa uuzaji matrekta mapya na vipuri, ikiwa ni pamoja na kuhudumia matrekta ya wakulima na kuagiza vipuri na zana za kilimo.

Umekuwa kimbilio la Watanzania wengi hasa wakulima, tangu kuanzishwa kwake, kwani wengi wamefaidika nao kupitia huduma ya matrekta na zana zake.

Umeuza matrekta na vipuri kwa fedha taslimu na mikopo na hivyo kuwezesha jamii ya wakulima kupata zana hizo kirahisi. Mradi umekuwa chachu nchini katika utoshelevu na uhakika wa chakula.

Wakulima nchini, wamefaidika na kuongeza uzalishaji kupitia mradi huu. Aidha, kwa kuzingatia mahitaji ya wakulima, ulianzisha vituo mikoani, ili kurahisisha

78 SUMAJKT (2022) Miaka 41 ya SUMAJKT.

huduma baada ya mauzo kwa wakulima waliopata zana na vipuri kutoka kwenye mradi.




*Baadhi ya matrekta yanayouzwa katika mradi wa SUMAJKT Mwenge, Dar es Salaam.*

**Kampuni ya Ulinzi**

SUMAJKT Guard Ltd ni kampuni tanzu ya SUMAJKT, inayojishughulisha na ulinzi binafsi. Kampuni ilisajiliwa rasmi Oktoba 20, 2008 na kuanza kazi kwa majaribio Februari mosi 2010, ikiwa na walinzi saba na sasa imepanuka na kuwa na walinzi zaidi ya 15,000.[79]

Malengo ya kuanzishwa kampuni hii, ni kutoa huduma ya ulinzi kwenye taasisi za Serikali, umma na binafsi,

79 SUMAJKT (2022) Miaka 41 ya SUMAJKT.

kutoa ajira kwa Vijana waliohitimu mafunzo ya JKT, mgambo na Askari waliostaafu katika vyombo vya ulinzi na usalama. Makao makuu ya Kampuni yako Mlalakuwa, Dar es Salaam.

Kampuni pia inatoa huduma za ulinzi kama ifuatavyo:

- Ulinzi kwa kutumia askari
- Ulinzi kwa kutumia mbwa
- Ulinzi kwa mifumo ya kielektroniki
- Uzio wa umeme (electric fence)
- Kufunga kamera za ulinzi
- Lango la kutumia umeme
- Mfumo wa kengele ya tahadhari
- Mfumo wa kufuatilia magari
- Ufungaji wa mifumo ya tahadhari
- Zimamoto na uokoaji
- Gari la wagonjwa
- Gari la kusafirishia fedha
- Ulinzi wa matamasha na sherehe
- Ulinzi binafsi



*Walinzi wa SUMAJKT Guard Ltd*




*Gari la zimamoto na uokoaji la SUMAJKT Guard Ltd.*

**SUMAJKT Catering Co. Ltd**

Mradi ulianzishwa Julai 2017 ukijulikana kama SUMAJKT Recreation & Catering Services kabla ya kuwa kampuni. Machi 25, 2020 mradi ulisajiliwa kuwa kampuni kwa jina la SUMAJKT Catering Co. Ltd na Makao makuu ya kampuni hii yako Mwenge, Dar es Salaam.

Kampuni inatoa huduma za kibiashara kwa kukodisha kumbi za sherehe na matukio ya kiserikali na kijamii. Sambamba na huduma hizi kampuni pia inatoa huduma ya mapambo, chakula na vinywaji.




*Moja ya kumbi za SUMAJKT Catering Co. Ltd ulioko Mwenge, Dar es Salaam.*

**Kampuni ya Huduma ya Wafanyakazi wa Kutwa Bandarini**

Kampuni ya SUMAJKT Port & Services Co. Ltd ilianza huduma za kusimamia wafanyakazi wa kutwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) tangu Desemba, 2017. Kipindi hicho ilifahamika kama mradi wa kutoa huduma bandarini (SUMAJKT Port Services).

Mradi ulipata usajili kuwa kampuni Oktoba 2020. Ilianza kwa kutoa huduma bandari ya Dar es Salaam pekee na mwaka huohuo iliingia makubaliano maalumu (MoU) na TPA, kutoa huduma katika bandari zote za bahari na maziwa makuu.[80] Maeneo hayo ni; bandari za Dar es Salaam, Kyela, Tanga, Mtwara, Kasanga, Kemondo, Kigoma na Mwanza. Huduma hii imekuwa kichocheo cha uchumi nchini kwa kuongeza kuaminika kwa bandari zetu ambazo hutumiwa na nchi jirani zisizo na bandari.

80 MoU between TPA and SUMAJKT Port Services, July 2020.



*Baadhi ya wafanyakazi wa kutwa wanaosimamiwa na SUMAJKT Port & Services wakiwa kazini kwenye bandari ya Dar es Salaam.*

**Kampuni ya Usafi na Unyunyiziaji Dawa**

Shughuli za usafi na unyunyiziaji dawa hufanywa na SUMAJKT Cleaning and Fumigation Company Ltd. Huduma zinazotolewa ni pamoja na huduma ya usafi na upuliziaji dawa za kuua wadudu waharibifu, utengenezaji na utunzaji wa bustani na utengenezaji wa mapambo ya bustani. Kampuni hii ilianzishwa kama kitengo cha usafi ndani ya SUMAJKT Guard Co. Ltd Septemba, 2018 ikiwa ni huduma saidizi ya kiusalama kwa wateja ikiwemo mabenki na taasisi zingine za kibenki.

Machi 14, 2020 kitengo kilisajiliwa kuwa kampuni. Tangu kuanzishwa kwake, imekuwa ikijishughulisha na majukumu yake mama ya kutoa huduma ya usafi katika ofisi ya Serikali, mashirika, kampuni, kwa watu binafsi, majiji na miji nchini.




***Baadhi ya wafanyakazi wa SUMAJKT Cleaning and Fumigation, wakifanya usafi katika barabara ya Sam Nujoma, Dar es Salaam.***

**Kampuni ya Udalali wa Bima**

Kampuni ya SUMAJKT Insurance Broker Co. Ltd ilianzishwa mwaka 2019 kwa lengo la kusaidia Shirika

na JKT kuongeza mapato kwa kutumia fursa kubwa ya wateja wa ndani na nje ya JKT na JWTZ.

Kampuni inaendelea kujenga uwezo wa kufanya kazi za bima jeshini, miradi na kampuni zenye ubia na SUMAJKT. Pia, inajikita kutanua soko kwa kutafuta kazi za nje ya Jeshi, hasa kwenye taasisi, kampuni na watu binafsi, na kazi zinatekelezwa kwa gharama

iliyopangwa na Kamishna wa Usimamizi wa Bima nchini kwa ufanisi mkubwa. Lengo ni kuwa Kampuni kamili ya bima badala ya uwakala.

**Kampuni ya Udalali na Minada**

Kampuni ya SUMAJKT Auction Mart Co. Ltd ilianzishwa kama mradi Februari 21, 2018 na kusajiliwa kuwa kampuni inayokusanya ushuru, madeni na udalali wa minada Juni 11, 2019. Kampuni hii ni mahsusi katika kusadia Serikali na taasisi binafsi kusimamia na kukusanya madeni, kufanya minada na kukusanya ushuru.

Wateja wakubwa wa kampuni hii ni Serikali Kuu, serikali za mitaa, taasisi za kifedha, mashirika madogo ya kifedha, watu binafsi na kampuni.

**Kampuni ya Lojistiki**

Kampuni ya SUMAJKT Logistics Co. Ltd ilianzishwa kama mradi mwaka 2013 uliojulikana SUMAJKT Clearing and Forwarding, kwa lengo la kurahisisha uondoshaji na usafirishaji mizigo ya SUMAJKT kutoka bandarini na viwanja vya ndege.

Mradi ulianza kwa kupata kibali cha uwakala wa ndani, kilichotumiwa kuondosha matrekta ya SUMAJKT Agri-Machinery. Desemba 2021 kampuni ilisajiliwa na kuwa SUMAJKT Logistics Co. Ltd kwa lengo la kupanua wigo wa huduma.

SUMAJKT Logistics Co. Ltd inatoa huduma ya uwakala wa forodha na usafirishaji mizigo kwa JWTZ, JKT, SUMAJKT, mashirika ya umma, binafsi, uuzaji na usafirishaji wa nishati yakiwamo mafuta ambapo kimeanzishwa kituo cha kuuza mafuta jamii ya petroli kilichoko Mlalakuwa, Dar es Salaam.




*Kituo cha mafuta cha SUMAJKT Energies kilichoko Mlalakuwa, Dar es Salaam.*

**Kampuni ya Dawa na Vifaa tiba**

SUMAJKT Pharmaceutical Co. Ltd (SPCL) ni kampuni iliyoanzishwa mwaka 2020 ikiwa na malengo ya kutoa huduma katika tasnia ya afya. Kampuni inatoa huduma katika sekta ya afya, ikiwamo; huduma za dawa na vifaa tiba.

Kampuni inalenga kujenga kiwanda cha dawa na maduka nchini na kusambaza vifaa tiba katika vituo vya afya na maduka ya dawa.




*Duka la dawa la SUMAJKT Pharmaceutical Co. Ltd lililoko Mwenge, Dar es Salaam.*

**SUMAJKT Meat Supply**

Mradi huu ni wa kununua, kunenepesha, kuchinja na kuuza nyama yenye ubora kwa bei nafuu katika Vikosi vya JKT na maeneo yaliyo katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Ulianza kazi Mei mosi 2017 katika Vikosi vya Ruvu, Mgambo na Mafinga.

Mradi unaendelea kufanya vizuri ili kufikia malengo uliojiwekea, ikiwa ni pamoja na kutafuta masoko nje ya Vikosi. Matarajio ya baadaye, ni kuanzisha kiwanda cha nyama ili kuiongeza thamani na kuiuza ndani na

nje ya nchi. Pia, mradi unapanga kuchakata ngozi na kuziuza.

**Huduma ya Elimu**

**Jitegemee Sekondari**

Sekondari ya Jitegemee ni ya kutwa na bweni kwa wavulana na wasichana na wenye mahitaji maalumu, kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.

Chimbuko la shule hii, ni Sera ya Elimu ya Watu Wazima ambapo mwaka 1974 ilisajiliwa kama Kituo cha Elimu ya Watu Wazima kikitoa elimu ya sekondari kwa Maafisa na Askari. Wakati huo, iliitwa Mgulani (JKT) Sekondari.

Baada ya ongezeko kubwa la Maafisa na Askari wasomi kujiunga na Jeshi lengo la kuwandeleza likabadilika na kuwa fursa kwa familia za Maafisa, Askari na jamii. Mwaka 1985, shule ilisajiliwa kutoa elimu ya sekondari kwa wanafunzi wote na mwaka 2019 ilikabidhiwa SUMAJKT.



*Baadhi ya wanafunzi wa Sekondari ya Jitegemee wakiwa ndani ya ukumbi wa mikutano shuleni hapo.*

**Kawawa Sekondari**

Sekondari ya Kawawa ilianzishwa mwaka 1994 kutoa elimu kwa Maafisa, Askari, familia za Askari na raia wa maeneo jirani na shule. Ujenzi ulianza Agosti 1992, ukifanywa na Maafisa, Askari wa Kikosi cha Mafinga.

Shule ni ya mchanganyiko na hutoa huduma ya bweni na kutwa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita, ni ya mchepuo wa kilimo, kwa vidato vya kwanza hadi nne.

Mwaka 2008 ilipata kibali cha kuanzisha kidato cha tano na sita. Tahasusi zinazotolewa ni HGK, HGL, HKL, HGE, PCB, PCM, CBG, CBA, PGM na EGM.



*Baadhi ya wanafunzi wa sekondari ya Kawawa wakiwa darasani na mwalimu.*

**Shule ya Awali na Msingi Kawawa**

Shule ya awali na msingi ilianzishwa mwaka 2022 ikiwa na darasa la kwanza hadi la tatu. Kwa sasa iko mpaka darasa la nne, ikiwa na wanafunzi 243 na ni ya kutwa. Uwepo wa shule hio umepunguza ombwe la shule ya ngazi hiyo Mafinga ambapo huduma hii ya kijamii imesogezwa karibu na wananchi.



*Baadhi ya wanafunzi wa shule ya msingi Kawawa wakiwa darasani.*

**Mafanikio**

Umuhimu wa kuwa na Shirika la Uzalishaji Mali ndani ya JKT, ni kuchochea uzalishaji mali unaolenga kusaidia uendeshaji wa JKT na ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Kwa ujumla, Shirika limebuni na kuanzisha miradi mipya inayotoa fursa za ajira kwa jamii. Sehemu ya faida inayotokana na uzalishaji mali, imekuwa ikisaidia uendeshaji wa JKT.

Shirika limepata mafanikio katika nyanja zinazoshabihiana na lengo la kuanzishwa kwake ifuatavyo:-

**Kuongeza Kanda za Ujenzi**

Shirika limeongeza kanda tatu za ujenzi ili kuleta ufanisi katika sekta hiyo kama ifuatavyo:

- Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mashariki
- Kanda ya Kaskazini Mashariki
- Kanda ya Ziwa Magharibi

**Kuchangia Uendeshaji wa Shughuli za JKT**

Shirika limechangia gharama za uendeshaji wa JKT ikiwamo mafunzo na malezi ya Vijana.

Vijana kupata fursa ya kujifunza stadi za kazi kupitia kampuni na miradi ya ushonaji nguo, ufundi seremala, ushonaji viatu, ufugaji samaki na ujenzi.

**Kuchangia Pato la Taifa**

Shirika linachangia Pato la Taifa kupitia uzalishaji mali na kulipa kodi stahiki.

**Kuongeza Ajira**

Shirika limeongeza ajira kwa Vijana wa kitanzania kupitia kampuni zake tanzu, viwanda na miradi. Mfano, SUMAJKT Guard Ltd hadi mwaka 2021 imeajiri Vijana zaidi ya 15,000. Kampuni ya Cleaning and Fumigation imetoa ajira kwa Vijana 1,344 tangu kuanzishwa kwake.

**Mafunzo kwa Vitendo**

Shirika kupitia kampuni zake tanzu linatoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wanaosoma na waliohitimu vyuo. Kwa mfano, mafunzo hayo hutolewa kupitia kampuni ya ujenzi, mifugo na kilimo.

**Kuongezeka kwa Viwanda**

Katika kutekeleza mpango mkakati unaoendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Shirika limeboresha viwanda vilivyopo na kuanzisha vipya ili kufikia uchumi shindani wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Uwepo wa viwanda hivi unaliwezesha Shirika kuzalisha bidhaa zenye ubora zinazokidhi mahitaji ya soko na kuongeza mapato.

**Kuongezeka Miradi ya Huduma na Biashara**

Shirika limeanzisha miradi ya huduma na biashara. Limetoa huduma kwa viwango vinavyokubalika, hivyo kujenga imani kwa jamii na kutanua wigo wa masoko na biashara.

**Mradi wa Uwekezaji SUMAJKT House**

Shirika limejenga jengo la kitega uchumi eneo la Medeli East, Dodoma linalojulikana kama 'SUMAJKT House'. Jengo hilo linatumika kibiashara kwa kukodishwa kwa taasisi, mashirika na watu binafsi, na linasaidia Shirika kuongeza mapato.




*Jengo la SUMAJKT House lililoko Medeli East, Dodoma.*

## Ununuzi wa Vitendea Kazi

Shirika limeendelea kujiimarisha kwa kununua vitendea kazi kupitia faida linazopata kutoka kampuni zake tanzu na miradi yake. Lengo ni kuongeza tija na kurahisisha shughuli zake ikiwamo huduma ya ulinzi, viwanda na ujenzi.

Baadhi ya vitendea kazi vilivyonunuliwa ni mitambo na mashine za ujenzi, magari ya utawala na kazi, pikipiki za doria, silaha kwa ajili ya ulinzi, zana za kilimo na mitambo ya kielektroniki ya ulinzi.






*Baadhi ya vitendeakazi vya SUMAJKT.*

## Kutekeleza Miradi Mikubwa

Shirika kupitia SCCL limetekeleza miradi ya kawaida na kimkakati kwa weledi na gharama nafuu. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na:

- Ujenzi wa nyumba 150 za Watumishi wa Serikali Mbweni, Dar es Salaam mwaka 2004.
- Ujenzi wa nyumba 250 za Watumishi wa Serikali, Mwangaza, Dodoma.
- Ujenzi wa Makao Makuu ya JKT Chamwino mwaka 2017.
- Ujenzi wa ukuta kuzunguka mgodi wa madini ya tanzanite Mirerani wilayani Simanjiro, Manyara wenye urefu wa kilometa 24.5 mwaka 2017/18.
- Ujenzi wa Ikulu mpya ya Chamwino Dodoma na uzio wenye urefu wa kilometa 27, mwaka 2019 hadi 2023.
- Ujenzi wa nyumba 41 za makazi ya Watumishi wa Ikulu ya Chamwino, mwaka 2020.
- Ujenzi wa majengo ya wizara sita katika Mji wa Serikali, Dodoma mwaka 2020.
- Ujenzi wa Jengo la NEC Makao Makuu Dodoma mwaka 2020.
- Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Uhamiaji mwaka 2020.
- Ujenzi katika taasisi za kutolea huduma kwa jamii zifuatazo:
    - Ujenzi wa wodi za watu mashuhuri katika Hospitali Kuu ya Taifa Muhimbili, wodi za wajawazito katika Hospitali ya Rufaa Mbeya na

Ujenzi wa Hospitali ya Uhuru, Chamwino, Dodoma.

- ❖ Ujenzi wa madarasa na mabweni katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo cha Ualimu cha Kabanga, Kigoma na maabara mtambuka katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

- ➢ Ujenzi wa bandari kavu Kwala, Pwani. Ujenzi wa bandari hii utaongeza kasi ya upakuaji na upakiaji wa bidhaa zinazopita bandari ya Dar es salaam, hivyo kuchochea uchumi wa Taifa.
- ➢ Ujenzi wa vituo vya umahiri vya madini katika Wilaya za Chunya, Mbeya; Songea, Ruvuma; Handeni, Tanga; Chuo cha Madini Dodoma, Mpanda, Katavi; Bariadi, Simiyu; Musoma, Mara na Bukoba, Kagera. Vituo hivi vimesaidia kuzuia utoroshaji wa madini nje ya nchi hivyo kuongeza pato la Taifa.

- ➢ Ujenzi wa ofisi za Serikali zikiwamo ya Mkuu wa Mkoa Katavi, Mkuu wa Wilaya Ruangwa, Mkuu wa Mkoa Simiyu, TEMESA, Dodoma na za walimu mkoa wa Mbeya, za wakuu wa Wilaya za Siha, Nanyumbu na Chato.

- ➢ Ujenzi wa ofisi za Chama cha Walimu Tanzania (CWT) katika mikoa yote Tanzania Bara.

- ➢ Kushiriki katika zoezi la utengenezaji wa madawati 65,000 mwaka 2016.

- Ujenzi wa ukuta Mirerani, Manyara mwaka 2018.
- Kufanikisha maonesho ya bidhaa na huduma zinazotolewa na Vikosi, SUMAJKT, Shule na Vyuo vya Ufundi Stadi yaliyofanyika kuanzia tarehe 1 hadi 9 Julai 2023 katika eneo la SUMAJKT House Medeli East, Dodoma.
- Ukarabati wa jengo la Urithi wa Ukombozi wa Afrika.



*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango (aliyeshika kiatu) akipata maelezo katika Banda la Maonesho ya wiki ya Miaka 60 ya JKT yaliyofanyika viwanja vya Medeli East Jijini Dodoma.*

**Kupunguza Nakisi ya Bajeti**

Shirika limesaidia kupunguza nakisi ya bajeti katika kukamilisha miradi ya muda mfupi na ya kimkakati kwa mfano, ujenzi wa ukuta wa Mirerani.

**Changamoto**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Shirika limepitia changamoto ambazo zimekuwa zikitatuliwa ifuatavyo:

**Mabadiliko ya Tabianchi**

Mabadiliko ya tabianchi huathiri shughuli za kilimo na ufugaji, unaosababisha kuathirika kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Katika kukabiliana na changamoto hii, Shirika limwekeza katika kilimo cha umwagiliaji na utunzaji chakula cha mifugo kwa matumizi ya baadaye.

**Bei za Bidhaa Kupanda**

Shirika linaathiriwa na kupanda mara kwa mara kwa bei za bidhaa, zikiwamo pembejeo za kilimo, vifaa vya ujenzi na malighafi za viwanda. Hali hii huathiri bajeti na mipango ya utekelezaji wa miradi katika sekta za ujenzi, kilimo na mifugo, viwanda, biashara na huduma.

Katika kukabiliana na changamoto hii, Shirika hufanya ununuzi wa malighafi kwa kiwango kikubwa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji, ili kukabiliana na mabadiliko ya bei.

**Kupanda na Kushuka kwa Bei za Mazao**

Bidhaa za kilimo zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya kushuka kwa bei. Hali hii imesababisha miradi kupata faida ndogo tofauti na malengo yaliyokusudiwa.

Hata hivyo, Shirika limekuwa likibuni mbinu za kupambana na mabadiliko hayo kwa kujenga maghala ya kuhifadhi mavuno katika kipindi ambacho bei ya soko inakuwa chini na kuuza inapopanda. Pia, Shirika limeanza kilimo cha mkataba na wanunuzi ili kukabiliana na changamoto ya masoko.

**Madeni**

Shirika linadai madeni makubwa kutokana na kutolipwa kwa wakati madai ya fedha ya huduma na bidhaa zilizotolewa kwa wateja. Kwa upande wa sekta ya ujenzi, hali hiyo huchelewesha miradi ya ujenzi, hivyo kuongezeka muda na gharama.

Shirika linafuatilia madeni kwa wateja wake. Inaposhindikana, hutumia SUMAJKT Auction Mart Co. Ltd kuyakusanya.

**Mabadiliko ya Teknolojia**

Teknolojia za kisasa katika sekta za uzalishaji, umelazimu Shirika kufanya mabadiliko ya vitendea kazi na wataalamu ili kuendana na kasi ya mabadiliko hayo.

Mfano, katika sekta ya viwanda, mabadiliko haya yameongeza ushindani katika soko kwa vigezo vya ubora wa bidhaa na huduma. Shirika linaendelea kukabiliana na changamoto hii kwa kununua vitendea kazi vya kisasa, kuboresha miundombinu na kutoa mafunzo kwa watendaji.

**Mitaji**

Kutokana na kukosa mitaji ya kutosha na uhakika, Shirika limekuwa na kasi ndogo ya kuboresha miradi ya uzalishaji na kutekeleza mikubwa ya kimkakati kama ujenzi, viwanda, kilimo na biashara. Hata hivyo, Shirika linaendelea kufanya jitihada za kuongeza mitaji kwa kutumia vyanzo vyake vya mapato ya ndani na mikopo kutoka taasisi za kifedha.

# SURA YA TANO

## MIPANGO YA BAADAYE

Mipango ya baadaye katika taasisi ya Serikali na isiyo ya kiserikali, ndio mwongozo muhimu katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku, ukionesha vipaumbele, utoaji uamuzi, tathmini na njia sahihi za kufikia malengo.

JKT ikiwa ni moja ya taasisi za Serikali, ina mipango mikakati ya baadaye inayoongozwa na Dira na Dhima, ili kutekeleza majukumu ya msingi ya malezi ya Vijana, uzalishaji mali na ulinzi. Mipango ya baadaye ya JKT ni:

**Kuboresha Mafunzo**

Vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT wamekuwa mabalozi wazuri na chachu ya mafanikio kwa Taifa. Kukua kwa Sayansi na Teknolojia kumesababisha haja ya kuboresha mafunzo ya Vijana, ili kwenda na wakati, hasa ikizingatiwa utandawazi umechangia mmomonyoko wa maadili katika jamii ulioathiri kizazi cha sasa.

Hata hivyo, JKT limejipanga kukabiliana na athari hizo kwa kuboresha mtaala wa mafunzo ya Vijana kwa kufanya yafuatayo:

- Kuwasiliana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine ili kuongeza muda wa mafunzo ya Vijana wa Kundi la Lazima kuwa mwaka mmoja, badala ya miezi mitatu ya sasa.
- Kushirikiana na wadau kutoa vyeti vitakavyotambuliwa na NACTE na VETA.
- Kuongeza wakufunzi wenye taaluma za sayansi ya jamii, stadi za kazi, ujasiriamali na saikolojia.
- Kuendelea kutoa elimu kwa Maafisa, Askari, Vijana na Watumishi wa umma kuhusu sheria za kijeshi.
- Kuongeza matumizi ya TEHAMA kwa kuwezesha Vikosi kuboresha matumizi ya teknolojia katika malezi, uzalishaji na ulinzi.
- Kutumia zana za kisasa kwenye mashamba na miradi darasa.
- Kuongeza nafasi za Vijana wa kike watakaojiunga na JKT ili kuleta usawa wa kijinsia katika mafunzo, sambamba na kuwapatia fursa sawa kutumikia Taifa.

- Kuimarisha CUJKT, kuandaa Maafisa na Askari kwa ajili ya malezi ya Vijana.

**Kuwezesha Vijana Kuwa Wazalendo na Kujitegemea**

JKT inalea Vijana, kwa lengo la kuwafunza kufanya kazi pamoja, kuwajengea uzalendo, kukuza mwamko wa kitamaduni, kijamii, kuwapa ujuzi wa stadi za kazi na maisha ikizingatiwa kuwa siku za hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la ukosefu wa ajira, mmomonyoko wa maadili na kupungua kwa uzalendo kwa Vijana.

Kuna ongezeko la ukosefu wa ajira, kupungua kwa uzalendo na mmomonyoko wa maadili kwa Vijana. Hivyo, JKT limejipanga kuboresha mafunzo yake, ili kuwapa Vijana mafunzo yanayowawezesha kuwa wazalendo na kujitegemea.

- Kuboresha mafunzo ya ukakamavu kwa Vijana.
- Kurithisha Vijana mila, sanaa na utamaduni wa Taifa.
- Kuwasiliana na wadau kuona uwezekano wa kukopesha mitaji Vijana wanaohitimu mafunzo.
- Vijana kushiriki ujenzi wa miradi ya kitaifa.

- Kuimarisha ushirikiano na wadau wa taasisi za Serikali na zisizo za Serikali.
- Kutoa ujuzi wa ujasiriamali kwa Vijana kuwawezesha kujiajiri.
- Kuboresha miundombinu na kuongeza idadi ya Vikosi.
- Kujenga Chuo kikubwa cha mafunzo ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi Kongwa, Dodoma.

JKT imekuwa ikitoa mafunzo kwa Vijana wa kitanzania kwa lengo la kuhimiza uzalendo na kujitegemea. Hata hivyo, yamekuwa yakitolewa kwa wachache kutokana na ufinyu wa bajeti. Wizara ya Ulinzi na JKT imepanga kuendelea kufanya maboresho yafuatayo:

- Kuboresha miundombinu ya Vikosi vya JKT na kuanzisha kambi mpya ili Vijana wote wanaohitimu kidato cha sita wapate fursa ya kufanya mafunzo Kundi la Lazima.
- Ununuzi wa magari ya Utawala.

**Kujitosheleza kwa Chakula**

JKT inapokea fedha za chakula cha Vijana kutoka serikalini. Juhudi za kupunguza utegemezi huo zinaendelea kufanyika kwa kupunguza kiwango cha fedha ya chakula kutoka Sh. 10,000 hadi Sh. 3,000 kwa Kijana kwa siku.

JKT pia imepanga kuendelea kupunguza gharama hizo kwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na bidhaa kwa kufanya yafuatayo:

- Kuendeleza kilimo, uvuvi na ufugaji kimkakati.
- Matumizi ya zana na mitambo bora ya kilimo.
- Kuanzisha kitengo cha utafiti wa kilimo, ufugaji na uvuvi.
- Kuwa mzalishaji wa mbegu bora za mazao ndani na nje ya nchi.

**Kudhibiti Vihatarishi vya Magonjwa**

UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza bado ni janga kwa Maafisa, Askari, Vijana na Watumishi wa umma. Hali hiyo inadhoofisha nguvu kazi na kupunguza ufanisi wa JKT.

Hivyo, JKT imepanga kutoa kipaumbele kudhibiti maambukizi ya VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza kwa kufanya yafuatayo:

- Kutoa ushauri nasaha na matibabu kwa Maafisa, Askari, Vijana na Watumishi wa umma walioathirika.
- Kubaini Vijana wa Kundi la Lazima wenye VVU na magonjwa yasiyoambukiza na kuwapa mafunzo na huduma stahiki.
- Kuongeza idadi ya warsha na semina za kupambana na maambukizi ya UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza.
- Kuhimiza Maafisa, Askari, Vijana na Watumishi wa umma kuendelea kufanya mazoezi ya viungo.
- Kuhimiza Maafisa, Askari, Vijana na Watumishi wa umma kujenga tabia ya kupima afya mara kwa mara.

**Kudhibiti Vihatarishi vya Rushwa**

Rushwa ni adui wa haki. Kwa ufanisi, JKT imepanga kuendelea kufanya yafuatayo:

- Kuhakikisha watakaobainika kutoa na kupokea rushwa wanachukuliwa hatua za kisheria.
- Kusimamia maadili miongoni mwa Maafisa, Askari, Vijana na watumishi wa umma.
- Kuwezesha Kamati ya Maadili kutoa elimu kuhusu athari za rushwa.
- Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji kwa kuzifanyia kazi taarifa za ukaguzi na mapendekezo ya kamati za maadili na nidhamu ili kubaini na kufichua kasoro za kiutendaji.

**Kuwezesha SUMAJKT kuwa Shirika Linalotoa Bidhaa na Huduma Bora Ndani na Nje ya Nchi.**

- Shughuli za uzalishaji mali zinazofanywa na SUMAJKT ni ujenzi, viwanda, kilimo, mifugo, uvuvi, biashara na huduma. Ili kuongeza ufanisi, mipango ya baadaye ya SUMAJKT ni kukuza uzoefu kupitia ushiriki katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa nchini ifuatavyo.

**Kuongeza Wigo wa Huduma za Ushauri**

Shirika limejipanga kuongeza wigo wa huduma zinazotolewa na Kampuni ya Ushauri Ujenzi. Huduma hizo, ni ardhi (mipango miji, upimaji na uthamini), TEHAMA na nyinginezo.

**Kukua Kibiashara**

Shirika linapanga kuanza kutekeleza miradi ya ujenzi, uhandisi na ushauri ndani na nje ya nchi, hususani kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi jirani. Vile vile, Shirika limebaini fursa ya masoko ya mahitaji ya bidhaa katika nchi za Afrika, Ulaya na Asia. Mahitaji hayo ni mchele, soya, mahindi, mboga mboga na matunda.

Pia, Shirika limepanga kushirikiana na Wizara za Viwanda na Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Chama cha Wakulima wa Mbogamboga na Matunda (TAHA) kupata fursa ya kuuza mazao nje ya nchi.

**Kuzalisha Mbegu Bora za Mazao**

Shirika limepanga kutumia mashamba kwa weledi zaidi kuzalisha mbegu bora kupitia Kampuni ya Kuzalisha Mbegu. Katika kutekeleza lengo hilo, Shirika litashirikiana na TARI, TOSCI na SUA.

**Kutumia Teknolojia ya Kisasa**

Shirika limejipanga kutumia teknolojia ya kisasa katika miradi ya kilimo, mifugo na uvuvi. Mitambo ya kisasa ya kilimo itatumika katika mashamba yake.

Mazao yatazalishwa na kuchakatwa kwa kutumia teknolojia za kisasa bila kuathiri ubora. Shirika linatarajia pia kuongeza ubora wa mazao ya mifugo katika mashamba ili kuongeza uzalishaji na mapato kwa teknolojia za kisasa.

Uboreshaji utahusisha uandaaji majengo, kiwanda cha chakula cha mifugo, udhibiti wa magonjwa na utunzaji mazao ya mifugo. Ufugaji utakuwa wa kondoo, ng'ombe wa maziwa na nyama, mbuzi, nguruwe, kuku na samaki.

Pia, Shirika linatarajia kununua zana za kisasa za uvuvi zikiwamo boti na nyavu zitakazotumika katika

uvuvi wa bahari kuu na maziwa bila kuathiri mazingira.

**Uboreshaji Viwanda**

Shirika limejipanga kuboresha viwanda ili kuongeza uzalishaji kulingana na ukuaji wa teknolojia. Uboreshaji utajumuisha upanuzi wa majengo ya uzalishaji na uhifadhi, vyombo vya usafiri, kuongeza wataalamu na mifumo ya uzalishaji.

Viwanda hivyo ni cha samani, maji, bidhaa za ngozi na ushonaji.

**Kuanzisha Viwanda Vipya**

Shirika litaanzisha viwanda vipya vya kimkakati kutokana na mahitaji yaliyopo. Mpango huo unalenga kiwanda cha vyakula vya mifugo, dawa za binadamu na maziwa.

Kuboresha viwanda vya nguo na maji, Mgulani; nafaka, Mlale; samani, Chang'ombe na bidhaa za ngozi, Mlalakuwa na uanzishaji viwanda vipya vya dawa na maji tiba, maziwa, korosho na mbolea ifikapo Juni 2026.

**Kuboresha Biashara na Huduma**

Kuboresha biashara na huduma zilizopo na kuanzisha mpya kadri fursa zitakavyojitokeza. Mfano, kuagiza, kuuza na kusafirisha mafuta na gesi.

# HITIMISHO

JKT kwa miaka 60 tangu kuasisiwa kwake imefanikiwa kutekeleza malengo yake kwa ufanisi. Malengo hayo yamefanikiwa kuwajenga Vijana kuwa wazalendo na kujitegemea ili kupenda Taifa lao na kuchangia Pato la Taifa. Katika kutekeleza majukumu hayo, JKT imetoa mafunzo kwa Vijana wengi wa kitanzania na wengine kuwa viongozi wa kitaifa.

JKT ni mahali salama ambapo Vijana hupata fursa ya kujengewa uzalendo, kujifunza kwa vitendo halisi na kutumikia Taifa. Vijana walioandaliwa na Taasisi yenye dhamana ni hazina ya Taifa isiyotiliwa shaka ikizingatiwa kuwa Ulimwengu unakumbana na changamoto za utandawazi na mazingira yasiyompa mzazi/mlezi nafasi ya kutosha kulea Kijana kwa misingi ya kitanzania, hivyo umuhimu wa JKT kuongezeka.

Kwa kipindi chote hicho, Serikali imekuwa ikitenga bajeti ambayo imesaidia kuongeza idadi ya Kambi na Vijana wanaojiunga na JKT. Katika kuhakikisha JKT inachukua Vijana wengi, imeanzisha mpango wa kilimo

mkakati ili kuweza kupunguza gharama za chakula kwa Vijana wanaojiunga na JKT. Mpango huo utasaidia kuipunguzia Serikali bajeti ya chakula.

JKT kupitia Shirika lake inaendelea kuanzisha miradi na kampuni nyingi za kibiashara kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kuongeza uzalishaji, hivyo kuchangia Pato la Taifa na kutoa ajira zaidi kwa Watanzania.

JKT kupitia SUMAJKT imetekeleza miradi ya kimkakati ambayo imesaidia kupunguza nakisi ya bajeti ya Serikali kwa kutekeleza miradi hiyo kama huduma kwa kutumia wataalamu wa ndani.

JKT inatoa mwito kwa jamii kuwa Vijana wanaofanya mafunzo wanakuwa wamejifunza mambo mengi ya ziada ambayo huwasaidia kimaisha, hivyo ni vema wazazi na walezi kuruhusu Vijana wao kujiunga na mafunzo ya JKT  mara nafasi zinapotangazwa.

# ORODHA YA OPERESHENI ZILIZOFANYWA NA JKT TANGU 10 JULAI 1963 HADI 2023

| NA. | OPERESHENI | KUANZA | KUMALIZA |
|---|---|---|---|
| 01. | 1 JLC | 10 JULAI 1963 | 28 SEPTEMBA 1963 |
| 02. | 'A' COY | 01 OKTOBA 1963 | 15 NOVEMBA 1963 |
| 03. | 'B' COY | 15 NOVEMBA 1963 | 31 DESEMBA 1963 |
| 04. | 'C' COY | 17 JANUARI 1964 | 28 FEBRUARI 1964 |
| 05. | 1000 | 03 MACHI 1964 | 15 APRILI 1964 |
| 06. | KUJENGA | 04 AGOSTI 1964 | 17 SEPTEMBA 1967 |
| 07. | 700 | 14 SEPTEMBA 1964 | 10 NOVEMBA 1964 |
| 08. | MAENDELEO | 13 NOVEMBA 1964 | 13 NOVEMBA 1966 |
| 09. | TYL | 05 MACHI 1965 | 31 MEI 1965 |
| 10. | MOTOMOTO 'A' | 07 MACHI 1965 | 15 MACHI 1967 |
| 11. | MOTOMOTO 'B' | 25 JUNI 1965 | 24 JUNI 1967 |
| 12. | JAMUHURI | 14 OKTOBA 1965 | 10 OKTOBA 1967 |
| 13. | UMOJA | 15 NOVEMBA 1965 | 14 JANUARI 1967 |
| 14. | SABASABA | 18 JULAI 1966 | 17 JULAI 1968 |
| 15. | UJAMAA | 01 JANUARI 1967 | 31 DESEMBA 1968 |
| 16. | UTII | 01 APRILI 1967 | 31 MACHI 1969 |
| 17. | JITEGEMEE | 01 JULAI 1967 | 30 JUNI 1969 |
| 18. | AZIMIO | 24 JUNI 1967 | 23 OKTOBA 1969 |
| 19. | USHIRIKA | 24 OKTOBA 1967 | 24 SEPTEMBA 1967 |
| 20. | KAZI 'A' | 24 OKTOBA 1967 | 24 FEBRUARI 1968 |
| 21. | KAZI 'B' | 24 FEBRUARI 1968 | 07 JANUARI 1970 |
| 22. | MWENGE | 24 FEBRUARI 1968 | 24 MEI 1968 |
| 23. | KILIMO | 10 FEBRUARI 1968 | 24 FEBRUARI 1968 |
| 24. | MAPINDUZI | 24 JUNI 1968 | 23 JUNI 1970 |
| 25. | ULINZI | 24 JUNI 1968 | 29 SEPTEMBA 1968 |
| 26. | VIJIJINI | 24 OKTOBA 1968 | 23 JANUARI 1969 |
| 27. | NGUVU | 24 OKTOBA 1968 | 23 OKTOBA 1970 |
| 28. | ELIMU | 24 JANUARI 1969 | 23 JANUARI 1971 |
| 29. | UTAMADUNI | 24 JUNI 1969 | 23 JUNI 1971 |
| 30. | UTUMISHI | 24 OKTOBA 1969 | 23 OKTOBA 1971 |
| 31. | UFUNDI | 21 JANUARI 1969 | 23 APRILI 1969 |
| 32. | MAJIMAJI | 24 MACHI 1969 | 23 JUNI 1969 |
| 33. | IMANI | 24 JUNI 1969 | 23 SEPTEMBA 1969 |
| 34. | UONGOZI | 24 OKTOBA 1969 | 23 JANUARI 1970 |
| 35. | MIKOA | 24 FEBRUARI 1970 | 23 JULAI 1972 |
| 36. | NGUMBARU | 24 JUNI 1970 | 23 JUNI 1972 |
| 37. | MWANGAZA | 26 DESEMBA 1970 | 25 DESEMBA 1972 |
| 38. | URAFIKI | 24 FEBRUARI 1970 | 23 MEI 1970 |
| 39. | MIPANGO | 24 JUNI 1970 | 23 SEPTEMBA 1970 |
| 40. | VITENDO | 01 NOVEMBA 1970 | 22 JANUARI 1971 |
| 41. | TEKELEZA 'A' | 01 MAY 1971 | 30 APRILI 1973 |

| NA. | OPERESHENI | KUANZA | KUMALIZA |
|---|---|---|---|
| 42. | MWONGOZO | 01 JANUARI 1971 | 31 MACHI 1971 |
| 43. | UCHUMI | 01 MEI 1971 | 31 JULAI 1971 |
| 44. | TUMAINI | 01 FEBRUARI 1972 | 31 JANUARI 1974 |
| 45. | MADARAKA | 01 JULAI 1972 | 30 JULAI 1974 |
| 46. | MABADILIKO | 15 AGOSTI 1972 | 14 AGOSTI 1974 |
| 47. | JIKOMBOE | 15 JANUARI 1973 | 14 JANUARI 1975 |
| 48. | MIAKA KUMI | 01 MEI 1973 | 30 APRILI 1975 |
| 49. | TANU MIAKA 19 | 01 NOVEMBA 1973 | 31 OKTOBA 1975 |
| 50. | UKOMBOZI | 01 JANUARI 1974 | 31 DESEMBA 1975 |
| 51. | TANU MIAKA 20 | 01 JUNI 1974 | 30 MEI 1976 |
| 52. | TIMIZA | 01 SEPTEMBA 1974 | 31 AGOSTI 1976 |
| 53. | MWAKA MMOJA | 15 JANUARI 1975 | 14 JANUARI 1977 |
| 54. | MUUNGANO | 01 AGOSTI 1975 | 31 JULAI 1977 |
| 55. | MAPAMBANO | 19 JANUARI 1976 | 19 JANUARI 1978 |
| 56. | CHAMA KIMOJA | 10 AGOSTI 1976 | 10 AGOSTI 1978 |
| 57. | TUJISAHIHISHE | 25 JANUARI 1977 | 25 JANUARI 1979 |
| 58. | UCHAGUZI | 15 AGOSTI 1977 | 14 AGOSTI 1979 |
| 59. | USAFI | 15 JANUARI 1978 | 14 JANUARI 1980 |
| 60. | MAZOEZI | 14 AGOSTI 1978 | 14 AGOSTI 1980 |
| 61. | KAGERA | 15 JANUARI 1979 | 14 JANUARI 1982 |
| 62. | USHINDI | 15 JULAI 1979 | 14 JUNI 1982 |
| 63. | UJENZI | 15 JANUARI 1980 | 14 JANUARI 1983 |
| 64. | TIJA | 15 JULAI 1980 | 14 JULAI 1983 |
| 65. | JUHUDI | 15 JANUARI 1981 | 14 JANUARI 1984 |
| 66. | IMARISHA | 15 JULAI 1981 | 14 JULAI 1984 |
| 67. | TEKELEZA 'B' | 15 JANUARI 1982 | 15 JANUARI 1985 |
| 68. | KUJIHAMI | 15 JULAI 1982 | 15 JANUARI 1985 |
| 69. | SAFISHA | 15 JANUARI 1983 | 15 JANUARI 1985 |
| 70. | NGUVU KAZI | 15 JULAI 1983 | 15 JULAI 1986 |
| 71. | MSHIKAMANO | 15 JANUARI 1984 | 14 JANUARI 1 987 |
| 72 | WAJIBU | 15 JULAI 1984 | 14 JULAI 1987 |
| 73. | VIJANA | 14 JANUARI 1985 | 15 JANUARI 1986 |
| 74. | OKOA | 15 JUNI 1985 | 14 JUNI 1986 |
| 75. | AWAMU YA PILI | 15 JANUARI 1986 | 14 JANUARI 1987 |
| 76. | NIDHAMU | 15 JUNI 1986 | 14 JUNI 1987 |
| 77. | CCM MIAKA 10 | 15 JANUARI 1987 | 14 JANUARI 1988 |
| 78. | MIAKA 20 YA AZIMIO LA ARUSHA | 15 JANUARI 1987 | 14 JANUARI 1988 |
| 79. | KIZOTA | 15 JANUARI 1988 | 14 JANUARI 1989 |
| 80. | MIAKA 25 YA JKT | 15 JUNI 1988 | 14 JUNI 1989 |
| 81. | MPITO | 15 JANUARI 1989 | 14 JANUARI 1990 |
| 82. | PROGRAMU YA CHAMA | 15 JUNI 1989 | 14 JUNI 1990 |

| NA. | OPERESHENI | KUANZA | KUMALIZA |
|---|---|---|---|
| 83. | MAFURIKO | JANUARI 1990 | JANUARI 1991 |
| 84. | KAMBARAGE | JUNI 1990 | JUNI 1991 |
| 85. | MAGEUZI | JANUARI 1991 | JANUARI 1992 |
| 86. | MIAKA 30 YA UHURU | JUNI 1991 | JUNI 1992 |
| 87. | MAZINGIRA | JANUARI 1992 | JANUARI 1993 |
| 88. | VYAMA VINGI | JUNI 1992 | JUNI 1993 |
| 89. | MAFURIKO LUSHOTO | JANUARI 1993 | JANUARI 1994 |
| 90. | MIEZI SITA | JULAI 1993 | JULAI 1994 |
| 91. | OLJORO | 01 JANUARI 1994 | JANUARI 1995 |
| 92. | MKAPA | 01 OKTOBA 2001 | OKTOBA 2003 |
| 93. | MIAKA 40 YA JKT | 15 FEBRUARI 2003 | 14 FEBRUARI 2005 |
| 94. | UTANDAWAZI | 01 APRILI 2004 | 30 MACHI 2006 |
| 95. | JIAJIRI | 01 MACHI 2006 | MACHI 2007 |
| 96. | KASI MPYA | 26 JUNI 2006 | JULAI 2008 |
| 97. | MAISHA BORA | JULAI 2007 | JULAI 2009 |
| 98. | UADILIFU | 02 JUNI 2008 | 01 JUNI 2010 |
| 99. | KILIMO KWANZA | 01 JUNI 2009 | 30 JUNI 2011 |
| 100. | UZALENDO | 01 JUNI 2010 | 30 JUNI 2012 |
| 101 | MIAKA 50 YA UHURU | 01 JUNI 2011 | 30 JUNI 2013 |
| 102. | SENSA | 13 AGOSTI 2012 | 30 JUNI 2014 |
| 103. | MIAKA 50 YA JKT | 04 MACHI 2013 | 30 MACHI 2015 |
| 104. | MIAKA 50 YA MUUNGANO | 01 APRILI 2014 | 30 MACHI 2016 |
| 105. | OPERESHENI KIKWETE - LAZIMA | 20 JUNI 2015 | 20 SEPTEMBA 2015 |
| 106. | OPERESHENI KIKWETE - KUJITOLEA | 20 JUNI 2015 | 30 JUNI 2017 |
| 107. | OPERESHENI MAGUFULI - LAZIMA - I | 01 JUNI 2016 | 4 SEPTEMBA 2016 |
| 108. | OPERESHENI MAGUFULI - LAZIMA - II | 19 DESEMBA 2016 | 08 SEPTEMBA 2017 |
| 109. | OPERESHENI MAGUFULI - KUJITOLEA | 19 DESEMBA 2016 | 30 JUNI 2019 |
| 110. | OPERESHENI TANZANIA YA VIWANDA - LAZIMA | 12 JUNI 2017 | 08 SEPTEMBA 2017 |
| 111. | OPERESHENI MIRERANI - LAZIMA | 25 JUNI 2018 | 24 SEPTEMBA 2018 |
| 112. | OPERESHENI MIRERANI - KUJITOLEA | 18 DESEMBA 2017 | 30 DESEMBA 2019 |
| 113. | OPERESHENI MAKAO MAKUU DODOMA -LAZIMA | 17 JULAI 2019 | 14 SEPTEMBA 2019 |
| 114. | OPERESHENI MAKAO MAKUU DODOMA -KUJITOLEA | 15 OKTOBA 2019 | 27 SEPTEMBA 2022 |
| 115. | OPERESHENI UCHUMI WA KATI -WATUMISHI WA BUNGE | 17 AGOSTI 2020 | 18 SEPTEMBA 2020 |

| NA. | OPERESHENI | KUANZA | KUMALIZA |
|---|---|---|---|
| 116. | OPERESHENI UCHUMI WA KATI - LAZIMA | 01 JULAI 2020 | 25 SEPTEMBA 2020 |
| 117. | OPERESHENI SAMIA SULUHU - LAZIMA | 01 JULAI 2021 | 02 SEPTEMBA 2021 |
| 118. | OPERESHENI SAMIA SULUHU - KUJITOLEA | 06 OKTOBA 2021 | 04 OKTOBA 2023 |
| 119. | OPERESHENI JENERALI VENANCE MABEYO -LAZIMA | 27 JUNI 2022 | 27 SEPTEMBA 2022 |
| 120. | OPERESHENI JENERALI VENANCE MABEYO -WABUNGE NA WATUMISHI WA BUNGE | 05 JULAI 2022 | 05 AGOSTI 2022 |
| 121. | OPERESHENI JENERALI VENANCE MABEYO -KUNDI MAALUMU LA WAHANDISI NA WATAALAMU WA TIBA | 22 AGOSTI 2022 | 13 OKTOBA 2022 |
| 123. | OPERESHENI JENERALI VENANCE MABEYO - KUJITOLEA | 28 NOVEMBA 2022 | 28 NOVEMBA 2024 |
| 124. | OPERESHENI MIAKA 60 YA JKT - LAZIMA | 19 JUNI 2023 | 16 SEPTEMBA 2023 |

# MAREJEO

Alma Persson and Fia Sundeval, (2019), "Conscripting Women: Gender, Soldiering and military Service in Sweeden 1965 – 2018" in the women History Review, 28:7, 1039 – 1056, DOI: 10. 1080/09612025. 2019.1596542.

Azimio la Arusha, 1967.

Bala Achi (1988), Arms and Armor in the Warfare of Pre-Colonial Hausaland. The Center for African Area Studies, Kyoto University.

Directive No. 1 of 1985.

Hornby, Albert Sydney, Oxford Advanced Learners Dictionary of Current English, Oxford University Press. 1995.

Hotuba ya Amiri Jeshi Mkuu kwa Makamanda wa JWTZ katika Ukumbi wa Makamanda Msasani Beach Club Novemba 25, 1986.

Hotuba ya Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere akiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi katika Mkutano Mkuu wa TANU wa Taifa wa 15 Mwaka 1971.

Hotuba ya J.K. Nyerere aliyoitoa kwa Vijana wa JKT Mgulani Machi 31, 1964, Dar es Salaam.

JKT (1973), Miaka 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

JKT (1988), Miaka 25 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

JKT (2012), Mwongozo wa Malezi ya Vijana.

JKT (2013), Miaka 50 ya Jeshi la Kujenga Taifa.

JWTZ (2014), Maadhimisho ya Miaka 50 ya JWTZ.

MoU between TPA and SUMAJKT Port Services, July 2020.

Patricia Ebrey etal (eds), (2006), *Pre – Modern East Asia: To 1800 : A cultural, Social and Political History*, Houghton Mifflin Company, Boston and New York.

Paul Bjerk,(2015) Building A Peaceful Nation; Julius Nyerere and Establishment of Sovereignty in Tanzania, 1960-1964.

Plutarch, (1992), "Plutarch's life of Coriolanus", plutarch's lives, Vol I (Dryden translation ed), Random House.

Robert Leenhard, (2006), *Elightened Defense: The National Security Policy of Thomas Jefferson*, West Virginia University, West Virginia.

Rwamkoma Daima (2017), Toleo Na. 1

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (2007), Sera ya Maendeleo ya Vijana, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Dar es salaam.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (2022), Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi, Ofisi ya Takwimu ya Taifa, Dodoma.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Chimbuko, Misingi na Maendeleo, Mkuki na Nyota Publishers Ltd, 2022.

Sheria ya JKT Namba 16 ya mwaka 1964

SUMAJKT (2022), Miaka 41 ya SUMAJKT.

Thomas Hippler, (2008), *Citizens, Soldiers and National Armies: Military Service in France and Germany, 1789 – 1830* (*War, History and Politics*), Routtledge, New York, www.amazon.com

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (2013), Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la 3. Oxford University Press, East Africa Limited, 2013. Nairobi, Kenya.

Tanganyika Rifles Mutiny of 1964, Tanzania. Peoples Defence Force (1993), Tanganyika Rifles Mutiny: January 1964. Dar es Salaam University Press.

The Corporation Sole (Chief of National Service) Order No. 326, 2009.

The Corporation Sole (Establishment) Act, Cap 119, RE 2002.

The Government of Tanganyika, (1963), Tanganyika National Service Directives

The National Service Act, Cap 193 RE 2002.

United Kingdom National Service (Armed Forces) Act, 1939.

Waraka wa Baraza la Mawaziri Namba 25, 1980.

Historia ya kuanzishwa JKT inaanzia mwaka 1958 wakati wa ziara ya viongozi wa Taifa nchini Ghana, ambapo Baba wa Taifa Mwl. Nyerere na Mhe. Rashid Kawawa (Simba wa Vita) walikwenda kuhudhuria sherehe za kuadhimisha mwaka mmoja wa uhuru wa nchi hiyo.

Wakiwa nchini humo, Mhe. Kawawa alialikwa chakula cha jioni pamoja na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Israel, Bi. Golda Meir. Mhe. Kawawa alipata fursa ya kuzungumza na kiongozi huyo, ambaye alitanabaisha namna Taifa la Israel linavyoandaa vijana wake kutumikia Taifa lao kwa moyo wa uzalendo.

Aliporejea hotelini walikofikia na Mwalimu Nyerere, Mhe. Kawawa alimweleza juu ya mazungumzo yake na Bi. Meir, ambayo yalimvutia na kumwagiza ayafanyie kazi watakaporejea nchini.

Waliporejea, Mhe. Kawawa aliyawasilisha mawazo hayo kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama cha TANU (TYL), Joseph Kizurira Nyerere, aliyekuwa anasaidiwa na Nangwanda Lawi Sijaona. Wazo hilo liliendelea kufanyiwa kazi hadi lilipoidhinishwa rasmi na Baraza la Mawaziri Aprili 1963 na ilipofika Julai 10, 1963 Taasisi ya kuandaa Vijana kuwa wazalendo iliyoitwa Jeshi la Kujenga Taifa, ilianzishwa rasmi.

Majukumu ya msingi ya JKT ni Malezi ya Vijana wa Kitanzania, Uzalishaji Mali na Ulinzi kwa ajili ya ustawi wa Taifa. Aidha, Vijana waliofanya mafunzo ya JKT ni wazalendo, wana nidhamu, ni wastahimilivu, wanapenda kufanya kazi na wanajali muda hivyo, ni fursa adhimu kwa kila Kijana kufanya mafunzo haya muhimu.

Kwa kipindi cha miaka 60, JKT imeendelea kuwa chombo adhimu cha malezi ya Vijana kuwaandaa kuwa wazalendo na viongozi wa baadaye wenye uwezo wa kuchochea maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa
Sanduku la Posta 2963
Dodoma - Tanzania.
Simu: +255 26 2962078
Nukushi: +255 26 2962080
Tovuti: www.jkt.go.tz

ISBN 978-9912-41-253-8